

Mashairi ya diwani hii yametengwa katika matapo mbalimbali kudhihiri- sha dhamira na maudhui ya utunzi:

1. Tungo za Uzalendo: Ni mashairi yanayoonyesha na kuhimiza wajibu wa raia mwema na hasa kila mzaledo kwa taifa lake. Kwani “Mvunda nti ni mwananti na mjenga nti ni mwananti vile vile”. Na raia wema ni yule anayefahamu wajibu wake katika nchi yake.
2. Tungo za Nasaha: Hutoa maaso, tahadhari, makanyo na mawaidha kwa wanadamu ghalibu katika dunia hii iliyosheheni bughdha, balaa na belua ili kwamba tujinusuru kungali mapema.
3. Tungo za Malimwengu: Kumjuvya mja kuhusu mengi ya dunia pamoja na mambo chungu nzima yanayomsakama na kumzingira katika maisha yake ya unyumba, mahaba, wivu na chuki, uchumi na maendeleo, furaha, dhiki n.k.
4. Tungo za Zinduko: Haya ni mashairi ya kuamsha na kutanabahisha ili mtu ajue apaswalo kujua lakini kwa ajili ya kughafilika au hamnazo huwa amepitikiwa. Baada ya kuzinduliwa, basi, mtu hufunikwa macho na akili akajua la kufanya.
5. Tungo za Maliwazo: Tangu mwanzo wa uhai mwandamu amejawa na maaffa na misiba. Ili aburudike na kuyasahau madhila yake, ni bora afarijiwe angalau kwa maneno ya mbawazi. Na hiyo pia ni dhima ya mshairi tangu enzi za Muyaka na Fumo Liongo.
6. Tungo za Vijembe: Mashairi ya sehemu hii yana uketo kimaudhui kwa sababu hulka na kadhia za wanadamu zimesawiriwa kwa kutumia istiara za viumbe anuwai. Aidha ni tungo za kupigia mifano, mafumbo, kufunga nyama na kejeli za kuzamisha kiini. Akili na busara nyingi zinahitajika katika kuyacha mbua mashairi ya aina hii.
7. Tungo za Umalenga: Tungo hizi zimegawanyika katika matapo mawili: Kwanza ni kutetea na kuhimiza Sanaa ya ushairi. Pili ni kuonyesha umbuji na kuhitim kwa kiwango Fulani kigezo cha umalenga. Sehemu hii imeandamana na swali kuhusu umalenga (kufu ya umalenga) ambalo jibu lake litatokana na hukumu za mashairi yenyewe yaliyomo kitabunia humu. Mimi binafsi ukiniuliza kama kweli ninashtahiki kuitwa malenga nitakupa majibu ya namna mbili: Kwanza nitakushauri uyasome mashairi yangu haya kwa makini mno kisha unihukumu kwayo kama kweli umalenga ni kufu yangu au la. Pili, nitakwambia uende ukayasome mashairi ya hao unaowaita ‘malenga’ kisha urudi unieleze wamenishinda nini hata nisilaiki kuitwa malenga?

Tete za karne hii:

Hayati Shaaban Robert alifichua ghamidha zake kuhusu tungo mbovu kwa kusema “Ushairi wa karne hii hunakisika kwa sababu ya matumizi maovu ya lugha. Mungu bariki, mimi si mmoja wa wahariri. Ningekuwa mhariri, mstari hata mmoja wa shairi la matumizi maovu ya lugha usingepata nafasi katika gazeti langu. Astahabu kuwa kati ya kitali waweza akunusurika na jeraha wakati mwingine kuliko kusoma mashairi ya siku hizi. Huwezi kunusurika na karaha zake. Uharabu huu hautakiwi na mara ukiachwa ushairi wetu utaa jabiwa sana”.

Nami naomba Mungu anibariki nisiwe mmoja wa wenye mashairi ya kukirihi. na endapo ni mumo, basin a omba radhi ya awali kwa kuyakinia kuwa si gharadhi Yangu kutunga karaha badala ya furaha.

Diwani hii imekua na kukusanya bahari nyingi sana za ushairi kama utakavyosoma kutoka kwenye ISTILAHİ. Licha ya bahari za kawaida za Tarbia, Takhmisa, Tenzin a Pindu, pia mna Tathnia, Tashlita, Kikwamba, Mkararaguni, Msuko, Gungu, Sabilia, Upeo, Ngonjera na Ukawafi.

Kutabaruku:

Bila shaka magambera waliowahi kuandika vitabu vikasomwa wataniunga mkono nikisema kuwa uandishi si masihara bali ni sulubu haswa kama si kondo. Aidha ni kazi ya ujima inayoundwa kwa mawaidha na mchango wa fikra kutoka kwa jamaa ya jamii – Kinga na kinga ndipo moto uwakapo. Kwa mintarafu hiyo, ninawashukuru wote walioniwezesha kufika hapa nilipofika pa jivu la bongo kuzaa moto huu wa kitabu cha Malenga wa ziwa kuu. Msaada wao si haba wa kubeza ingawa baadhi yao walinisabilia pasipo wao kujua kwamba wanankuza.

Ndedah J. Wallah (Warrah)

(Wallah Bin Wallah)

Nyakach Kadiang'a. Desemba, 1986

### 3. Istilahi katika Taaluma ya Fasihi na Ushairi wa Kiswahili

Ifuatayo ni orodha ya ISTILAHİ (majina ya kitaalam au kielimu) zinazotumiwa mara nyingi katika kufunza ama kuchambua fani za ushairi na fasihi katika Kiswahili. Ni muhimu sana kwa

msomi wa fasihi ya Kiswahili na mashairi kujifunza na kuelewa barabara istilahi hizi ili kwamba aepuke vikwazo na vizuizi vya kufahamu na kutamalaki taaluma ya mashairi na fasihi.

#### SHAIRI:

Shairi (mashairi) ni mtungo wenye maudhui maalum yanayomhusu mwanadamu na hulka yake katika mazingira anayoishi; tena maudhui hayo yawe yameelezwa kwa hisia za ndani Zaidi ambazo zinaathiri moyo na kutoa funzo zito. Na utungo wenyewe uwe umetungwa kisanaa na kwa lugha teule ya mkato kwa kufuata kanuni na mpangilio maalum unaokubalika (Kishairi) kama vile urari wa mizani, vina, muwala, utoshelezi na dhamira dhamirini.

#### UBETI (BETI)

Ni kifungu kimoja kamili cha shairi kinachoundwa kwa idadi ya mishororo iliyopangwa kwa mizani na vina. Tena sharuti sharuti ubeti utoe ujumbe kamili.

#### MSHORORO (MISHORORO)

Ni mstari wa ubeti. Idadi ya mizani. Kila kipande huwa na kina chake. Endapo mshororo umewanywa katika vipande viwili hadi vitatu, basi vipande hivyo huitwa UKWAPI, UTAO na MWANDAMIZI.

#### UKWAPI

Ni kipande cha kwanza cha Mshororo.

#### UTAO

Ni kipande cha pili cha mshororo.

#### MWANDAMIZI

Ni kipande cha tatu cha mshororo.

#### MWANZO

Ni mshororo wa kwanza katika ubeti.

#### MIOTO

Ni mshororo wa pili, unaofuata mwanzo katika ubeti.

## MLEA

Ni mshororo wa tatu, unaofuata molto kwenye ubeti huo huo.

## MUWALA

Mtiririko na mpangilio wa mwazo au fikra kutoka ubeti hadi ubeti – ni jinsi fikra zinavyopokezana kwa kufutiliza kisa au tukio katika shairi. Muwala ni kipimo cha upevu na ujuzi wa mtunzi anavyopanga mawazo.

## NATHARI

Ni lugha ya mjazo lugha ya riwaya ambayo ni maelezo tu wala si ya kishairi. Kutumia nathari ni kutoa maelezo bila kupanga maneno kishairi – ni kuhadithia.

## URARI

M pangilio na ulingano wa mizani, mistari ya ubeti na nsawa wa vina. Yaani mistari lazima ipangwe sawasawa kwa ufuatano wa habari inayotajwa. Mizani ipangike kwa idadi mwafaka. Na vina viwiane kisanaa na kidhamira bila kulazimisha neno.

## UHAKIKI (TAHAKIKI)

Pia huitwa Uhariri au Tahariri. Ni uchambuzi wa maandishi yoyote, ama ya vitabu au majarida kwa kufafanua nje ndani tathmini yake. Ni kukosoa na kusahihisha maandishi au tungo hizo. Ni kubainisha bayana kwa tafsili undani kwa kupekua, kuchungua na kudadisi mbinu zilizotummika, maudhui, lugha na ufasaha, ukweli na uongo uliomo ndani ya hayo maandishi pamoja na kutoa maoni yoyote yawayo kuyahusu – huo ndio uhakiki au uchambuzi wa makini na hali ya juu Zaidi.

## LAKABU

Jina la kujipa kutokana na sifa Fulani. Kama ni mshairi, basi hujiita kutokana na sifa zake za utunzi. Kwa mfano: Jitukali, Jinamizi, Nyamaume, Mchelea Jiji, Sura mbaya n.k.

## USTADH

Maana yake ni mwalimu. Kama ni mshairi, basi jina hilo hutumiwa kwa maana ya mwalimu wa ushairi kama vile Ustadh Fulani kwa maana ya Mwalimu Fulani. (Asili ya neno hili ni Kiarabu).

## BAHARI

Maana ya kwanza ni aina za tungo, yaani tanzu za mashairi. K.m. Bahari ya Tarbia, bahari ya Msuko, bahari ya Tathlitha n.k. Maana ya pili ya BAHARI ni mshororo wa mwisho wa shairi la UTENZI. Yaani ni kibwagizo cha ubeti wa utenzi. Kwa kawaida vbwagizo vyta beti za utenzi huishia kina cha aina moja ambacho hutanda na kutawala shairi zima. Na huko kutamalaki shairi loto ndiko kunakosababisha kibwagizo hicho kuitwa BAHARI. Wakati mwengine vina pekee vyta vituo vyta utenzi pia huitwa BAHARI.

## DIWANI

Ni kitabu cha mashairi. (Diwani ya Junamizi, Diwani ya Masamba, Diwani ya Akilimali, Diwani ya Nyamaume n.k.)

## JAZANDA (ISTIARA)

Ni mfano, picha au taswira ya kufananisha kiumbe chochote au kitu na binadamu kwa kukipa sifa ai nafsi ya kibinadamu. Au pia ni kumfananisha binadamu na kiumbe ama kitu kingine kwa maana ya kuwa sifa zao ni moja. Kwa mfano: Kumwita mtu mkali ‘simba’, mrefu ‘twiga’, mrembo ‘malaika au ua’; ‘Nakukanya jicho Jangu, mbona hukanyiki?; ‘Maskini tangawizi, mbona unaangamizwa?’.

## JARIBUSI (JARIBOSI)

Ni mhusika mkuu katika kisa chochote au cha kitabu, riwaya, tamthilia, shairi ama ngano. Ni msimuliwa mahususi ambaye ndiye kiini cha masimulizi. Hadithi kamili imetungwa juu yake, na mafunzo au dhamira ya kitabu inatokana nay eye katika nyendo zake, sifa zake, tabia zake na kadhia zake zote. Hata hativyo, si lazima kitabu au kisa kuwa na jaribusi mmoja tu.

## GUNI

Ni shairi lililolemaa, lenye kasoro, lililotungwa bila ukamilifu wa Sanaa ya ushairi, yaani halikufuata kanuni za ushairi za kupanga mizani au vina; umbo na mwundo si kamili. Lakini huwa na beti zenye ujumbe na maudhui.

## MKARARAGUNI

Ni shairi ambalo kila ubeti una vina vyake tofauti kivyake. Tazama shairi la Uzalendo kutoka diwani hii.

## KIKWAMBA

Ni shairi ambalo kila ubeti huanza kwa neno moja linalorudiwa. Tazama: Ukubwa Jaa.

## PINDU

Ni shairi lililotungwa kisanaa ili kwamba kipande cha mwisho cha mshororo kinatumia kuanzisha mshororo unaofuata au ubeti unaofuata. Tazama:

## JTENZI (TENZI)

Ni shairi ambalo beti zake ni fupi fupi zenyenye mizani isiyozidi kumi na mbii katika kila mshororo. Nani lazima mshororo uwe ni kipande kimoja tu, basi. Mifano ya tenzi katika diwani hii ni kama Viungo vyangu Azizi na hata nawe!

## KITUO

Mstari wa mwisho wa kila ubeti ambao aghalabu hurudiwarudiwa huitwa kituo, kipokeo, kiitikio, kibwagizo, mkarara, kimalizio au pambio. Lengo la kituo ni kutila nguvu au kusisitiza dhamira na maudhui ya shairi. Katika shairi lenye vituo tofauti kila ubeti, kituo huwa ni cha kutilia mkazo dhamira au ujumbe unaotajwa ndani ya ubeti.

## UTOSHELEZI

Ni ukamilifu wa wazo au jambo katika ubeti. Ni kwamba kila ubeti wa shairi ujitosheleze kwa kusimulia au kuelezea jambo kamili au tukio halisi ndani yake. Maana yake ni kuwa, kila ubeti uwe na ujumbe kamili unaoeleweka na kujisimamia bila kutegemea kukamilishwa katika ubeti unaofuata. Ni kama aya katika riwaya.

## TABDILA

Asili ya neno hili ni “badili”. Na maana yake ni kubadili irabu au vokali; au kubadili sliabi katika neno ili kuleta tamko au umbo Fulani analolidhamiria mtunzi kusudi atosheleze urari wa mizani

au kina anachohitaji kwenye shairi lake bila kupotosha maana halisi ya neno lililobadilishwa. MIFANO ya Tabdila: ‘sahibu’ kuwa ‘swahiba’; tumekaa kuwa tukele; dunia kuwa duniya; adhabu kuwa adhaba; timamu kuwa tamima; has ante kuwa has anta n.k.

### MAZIDA

Asili yake ni “zidi” au “ziada”. Ni istilahi inayotumika kwa maana ya kuongeza au kuzidisha silabi katika jina au kiarifa ili kuchukuana sawasawa kisanaa na kina u kutosheez mizani bila kupoteza maana ya asili ya neno lenyewe. Kwa mfano: Kilele kuwa kileleta; funga kuwa fungata; mwengine kuwa mwenginewe; keti kuwa ketile; kukatika kuwa kukatikile; nenda kuwa enenda; jaza kuwa jaaza n.k.

### INKISARI:

Asili yake ni mukhtasari. Ni kukata au kufupisha neno kitaalam bila kupoteza asili ya undani wake ili litumike sawasawa kwa utashi wa mtunzi. Mifano ya inkisari ni: sikasiri badala ya sikasiriki; sikiza badala ya sikiliza; samawi badala ya samawati; mana badala ya maana; jinale badala ya jina lake; watakani badala ya unataka nini; uza badala ya uliza; alo badala ya aliye n.k.

### VITUSHI

Matukio madogo madogo yanayojitokeza katika kisa, hadithi, tamthilia au riwaya ili kuendeleza masimulizi ama kuwajenga wahusika.

### VITUKO

Matendo makubwa makubwa yenyeye uzito kulingana na dhamira ya masimulizi yanayotokea katika kisa, hadithi, riwaya au tamthilia yanayowasilisha ujumbe, mafunzo au maudhui. Aghalabu ni dhama na vitendo vinavyomlega jaribusi.

### UMALENGA

Utaalam uliokamilika wa kutunga na kuimba mashairi. Na malenga ni bingwa kamili mwenye taaluma ya ushairi kwa kuhifadhi kunga na miiko ya ushairi. Aidha ya gwiji na kuyaimba mashairi licha ya kutarunga.

### MANJU

Stadi wakutunga na kuimba nyimbo – hasa katika ngoma. Pia huitwa mngoi (wangoi).

## MIZANI

Ni idada ya silabi katika mstari wa ubeti. Ni kipimo cha urefu wa mshororo na kukadiri mapigo (lahani) ya sauti. MFANO: ‘Malenga’ ni mizani (silabi) tatu: Ma-le-nga.

## VINA

Kimoja ni KINA. Vina ni silabi za maana moja au zenyenye matamshi mamoja zinazopatikana mwisho wa kila kipande au mwisho wa kila mshororo. Licha ya kuwa vina nip ambo la ubeti, pia ni ishara ya upeo wa ubingwa wa msanii wa shairi kwa kusadifisha maneno yanayosawazisha miishilio ya sauti.

## TATHINIA (UWILI)

Ni shairi la mishororo miwili tu katika ubeti. Mfano wa Tathnia katika Diwani hii ni Utalemewa na Mwananchi na Mzalendo.

## MSUKO

Ni shairi ambalo kibwagizo chake kimefupishwa. Tazama; Asaso, Nahodha, Kumbe, Yetu Macho, Ufukara ni wa Akli, Ngonjera.

## TATHILITHA (UTATU)

Ni shairi lenye mistari mitatu kwenye ubeti mmoja. Kila mshororo umetengwa katika vipande vinacyomalizika kwa vina sawa. Tazam: Tenda Haki, Tangawizi.

## TASHILITA (USITA)

Pia huitwa TASDISA. Ni shairi lenye mishororo sita katika kila ubeti wake. Tazama: Mwanadamu Alitoka Wapi?

## UKAWAFI

Ni shairi ambalo kila mshororo wa betizake una vipande au vina vitatu. Tazama: Siwi Nao, Kimba, Kina cha Uchungu, Chemichemi.

## TARBIA (UNNE)

Ni shairi lililo ubeti wenyе mishororo mine. Na mshororo hugawanyika katika vipande vilivyopambwa kwa vina. Mfano wa TARBIA: Tufanye Kazi, Mkataa Pema, Tutukuze Kiswahili, Simtukane Mamba, Kesho Wewe.

## GUNGU

Shairi lenye mishororo mirefu iliyo na mizani mingi (Zaidi ya mizani kumi na mbili) na kila mshororo una kina kimoja tu cha mwisho. Aghalabu mashairi ya GUNGU yalitumiwa sana na waswahili kama nyimbo katika ngoma zao. Mashairi ya bahari hii yanapatikana katika kitabu cha David Michuki Mawaidha ya Wamuchuthe na pia katika tungo za Fumo Liongo.

## NGONJERA AU MALUMBANO

Ni utungo au shairi la majibzano au majadiliano ambalo kwalo wahusika wawili au Zaidi hushiriki hadharani ama jukwaani kutoa rai zao kwa kujibizana au kulumbana. Tazama: Mwanachi na Mzalendo; Ngonjera.

## UPEO

Ni shairi ambalo kwalo mishororo ya ubeti mmoja huzidiana kwa mizani. Ni mizani yenye we imepangwa kwa urari na upeo wa juu Zaidi kiasi cha kudhiriri Sanaa ya kipekee. Tazama shairi la Afrika Ina Homa.

## SABILIA

Shairi hili lina vibwagizo vinavyotofautiana katika kila ubeti. Mradi ni kwamba kila ubeti utoshelezewe na kibwagizo chake. Asili ya neno hili ni kuachia huru; kwa hiyo kila ubeti umeachiwa huru kujitegemea kwa kiiptio chake.

## TAKIMISA (UTANO)

Ni shairi lenye ubeti ulioundwa kwa mistari mitatu. Kila mstari umegawanyika katika vina. Tazazm: Kizazi cha Fedheha; Kamange.

## KISARAMBE

Ni wimbo usio na mpangilio sawa wa mizani wala vina. Pengine hata beti zake hazina mwundo kamili wa ulinganifu wa umbo kila mmoja. Kisarambe ni karibu sawa na GUNI.

## MATHNAWI

Ni shairi ambalo kila mshororo wake una vina viwili. Shairi la bahari yoyote laweza kuwa Mathnawi ilimrdia tu mishororo yake iwe imegawanyika katika vipande viwili vyeye vina vyakati na vya mwisho. Mashairi mengi hutungwa kwa mkondo huu wa Mathnawi.

## TIWAYA

Hadithi ndefu ya kubuni ilitoandikwa kwa maandishi ya nathari agahalabu kueleza ukweli Fulani wa maisha katika jamii.

## TAMTHILIA

Ni mchezo wa kuigiza au utungo wa kisanaa unaoweka wazo Fulani katika matendo na mazungumzo ili kuonyesha ujumbe na dhamira.

## WIMBO (NYIMBO)

Ni maneno ya lahani, yanayotamkwa kwa sauti ya muziki. Nyimbo ni za aina nyingi k.m. nyimbo za mashairi, kwaya, dansi, nataki, taarabu, kasida sala, kanisa, ndaraia n.k.

## MUKTADHA

Ni jambo au habari inayozungumzwa; Ni sehemu ya mazungumzo au habari inayoendelea.

## KUFUNGA NYAMA

Ni kuuliza swalii au kutoa fumbo linalohitaji kufumbuliwa kishairi. Mtindo huu ulitumiwa tangu azali na malenga waliokubuhu walipokutana kwenye halaiki. Endapo nyama yake iliwashinda mabingwa wenzake kudungua, basi, walimpa mji ili awafungulie nyama (awafumbulie). Kikwetu tamthilia hiyo iliitwa NGERO na Mfunga Nyama (JANGERO) alipewa msichana ili kufungua nyama yake. Waluhya waliita MFUMBI.

## **UZALENDO**

*Mwananchi mzalendo  
Ni Mtu mwenye upendo  
Anayefaa mwenedo  
Kwa usafi wa vitendo  
Desturi zenyе haki*

## **KIKOWA**

*Mambo ni kikowa, kubali  
Kama hujajuwa, ni kweli  
Si kulia ngowa, bahili  
Pewa na kutowa, halali  
Ni kikowa*

*Si uwa ulip, kwa mali  
Alokupa mpe, sijali  
Kwa moyo mweupe, wa kweli  
Katu simtupe, kwa mbali  
Ni kikowa*

*Mtu mwenye wema, ni ghali  
Huapata heshima, kamili  
Sifa zikavuma, umbali  
Kutowa mtima, si mali  
Ni kikowa*

*Mambo Hayaendi, sahali  
Pasipo uundi, aali  
Wa kubwa kikundi, mahali  
Kuchanga utendi, amali  
Ni kikowa*

*Dunia ni watu, asili  
Na wala si vitu, saili  
Thamani ni utu, si mwili  
Kutowa sifutu, ni hali  
Ni kikowa*

### GANDA JEUSI

Nahamu tunda, lenye ganda jeusi  
Ama napenda, rangiye mahususi  
Yenye kulinda, jadi yake halisi  
Pendo langu halisi

Lisilopinda, ni ganda letu sisi  
Bora kushinda, launi ya tausi  
Si la madonda, ambayo hulighasi  
Pendo langu halisi

Vaa utunda, na Ufange kigesi  
Thama uwinda, kivazi xha weusi  
Anza kuranda, na kujawa muasi  
Pendo langu halisi

Mimi hukonda, moyo huenda kasi  
Kwa wanopenda, kitu chake kutusi  
Kiwe chavunda, ndicho cha asasi  
Pendo langu halisi

### UZALENDO

Kukipenda kitu chako, huo ndio uzalendo  
Mtu anapenda chake, japo hakina thamani  
Hatamani cha mwenzake, na kukitia rohoni  
Chake ni furaha yake, kingakuwa kitu duni

Kuipenda nchi yako, huo ndio uzalendo  
Kuwa atayari daima, taifa utumikia  
Uzukapo uhasama, haraka kupigania  
Adui kuwasakama, mbali kuwatupilia

Kuwapenda watu wako, huo ndio uzalendo  
Uzalendo ndio ngao, ni silaha kamilifu  
Tuwe nao moyo huo, tusiwe nyoyo dhaifu  
Wale wakilinda kwao, nasi tuwe timilifu

Kuipenda kazi yako, huo ndio uzalendo  
Kazi tusitegee, ni uhai ni afia

Mzalendo jitolee, hasa shamba kulimia  
Fanya kazi harambee, kwa uchumi kuinua

Kuipenda lugha yako, huo ndio uzalendo  
Tupendane kwelikweli, hakuna kubaguana  
Ukabila tusijali, sisi sote twafanana  
Tutumie Kiswahili, rahisi kuelewana

Kupenda taifa lako, huo ndio uzalendo  
Uzalendo ni upole, mapenzi kwa nchi yako  
Si ubishi wa kelele, vituko na maudhiko  
Nchi haisongi mbele, uzaledo sipoweko

#### TUFANYE KAZI

Kila kiongozi wetu, amesema waziwazi  
Kazi iwe raha yetu, masika na kiangazi  
Wala pasiwe na mtu, anayefanya upuzi  
Mzembe katika kazi, huyo ni adui yetu

Huyo ni adui yetu, asotaka fanya kazi  
Japo ana kila kitu, elimu pia ujuzi  
Kuwa naye sithubutu, huyo sawa na pwaguzi  
Mzembe katika kazi, huyo ni adui yetu

Ni hasidi si mwenzetu, kamwe hatumpongezi  
Kapotea lengo letu, kwani halitekelezi  
Harambee wito wetu, maana yake ni kazi  
Mzembe katika kazi, huyo ni adui yetu

Awe mshona viatu, jozi baada ya jozi  
Anawafaidi watu, nyumbani na matembezi  
Akishona jozi tatu, hujipatia ghawazi  
Mzembe katika kazi, huyo ni adui yetu

Dereva mbeba watu, nahodha mwenye jahazi  
Tabibu na siha zetu, pamoja na viongozi  
Hao tegemeo letu, sio kama majambazi  
Mzembe katika kazi, huyo ni adui yetu

Walimu ni nuru yetu, kwa masomo na malezi  
Hasarifu njia zetu, kuwapinga hatuwezi  
Wafunze tupate utu, maarifa na ujuzi  
Mzembe katika kazi, huyo ni adui yetu

Ukulima hapa petu, ndiyo kazi ya malezi  
Kilimo ni haki yetu, kunde chai na viazi  
Tulime tupate vitu, chakula na matumizi  
Mzembe katika kazi, huyo ni adui yetu

Tama siongezi kitu, kuhusu wito wa kazi  
Nawaaga wanakwetu, mwende fanya upekuzi  
Itikeni wito wetu, wa Amani na mapenzi  
Mzembe katika kazi, huyo ni adui yetu

#### TUMEHIARI

Ni wito umetolewa, kila mtu kusikia  
Hima bila kuchelewa, tuanze kujitolea  
Madarasa yangojewa, wana wetu kusomea  
Kenya tumeitikia, tamko lako Rais

Twamshuru Rabuka, Mola mwenye kujalia  
Amjalie Baraka, Baba Moi twaringia  
Rais ametamka, shule zote kupanua  
Kenya tumeitikia, tamko lako Rais

Jenga darasa la nane, na elimu kuinua  
Wazalendo tuungane, hakuna wa kukawia  
Madarasa yaonekane, wanafunzi kusomea  
Kenya tumeitikia, tamko lako Rais

Rais ametusihi, mengi tumeyasikia  
Tuamke asubahi, tufanye kazi kwa nia  
Jambo bora ni kuwahi, siyo nyuma kubakia  
Kenya tumeitikia, tamko lako Rais

Kinara wetu asema, taratibu kwa hatua  
Miaka nane kusoma, tuje kujitegemea  
Elimu ndiyo huduma, bindamu htumia  
Kenya tumeitikia, tamko lako Rais

Mlezi anena kweli, darasa kuongezea  
Mtoto huwa kamili, la nane akifikia  
Ili aweze himili, matatizo ya dunia  
Kenya tumeitikia, tamko lako Rais

### UTAMADUNI

Ndugu zangu wasifika, nimefika uwanjani  
Mzigi nimejitwika, niutue hadharani  
Nitangaze kwa haraka, sifa za utamaduni  
Utamaduni shikeni, kielelezo cha jadi

Utamaduni muhimu, kwayo maisha juweni  
Hufanya mamabo yadumu, hadi siku za usoni  
Haifai kushutumu, chombo hiki asilani  
Utamaduni shikeni, kielelezo cha jadi

Utamaduni msingi, wa jadi zetu jamani  
Faida zake ni nyingi, na muhimu masihani  
Huleta sifa kwa wingi, kwa watu wenye Imani  
Utamaduni shikeni, kielelezo cha jadi

Ni ishara mathubuti, ya kueleza undani  
Na ndicho chombo thabiti, kielezacho u nani  
Tukitunze kwa dhati, kwa mapenzi na Imani  
Utamaduni shikeni, kielelezo cha jadi

Hufanana na ramani, kueleza masikani  
Hutumika ugenini, kulieleza baini  
Tangu China na Japani, tamaduni wathamini  
Utamaduni shikeni, kielelezo cha jadi

'Tamaduni ni jumla, ya mambo yote ya ndani  
Mifano yake ni mila, destrui na Imani  
Hayo yote kwa jumla, ndo hasa utamaduni  
Utamaduni shikeni, kielelezo cha jadi

Elimu lugha sharia, Sanaa ngoma na dini  
Ndiyo mambo asilia, yaitwayo tamaduni  
Na mtu kutasusia, amepotoka juweni  
Utamaduni shikeni, kielelezo cha jadi

Mshika mambo ya jadi, hapotei utumwani  
Mila zake hakaidi, hazioni kuwa duni  
Kila mara hujinadi, kwayo mambo ya nyumbani  
Utamaduni shikeni, kielelezo cha jadi

Hayo niliyotamka, yawatosheni jamani  
Msijefanya dhihaka, kupoza mambo ya ndani  
Msibeze Afrika, na kusifu marekani  
Utamaduni shikeni, kielelezo cha jadi

Lilipata ushindi wa kwanza katika mashindano ya Sanaa ya Kiswahili ya shule za upili za Nairobi, 1977.

#### KILA MUACHA SAMBOYE

Kamwe ni muelewa, mtambuzi ujuwaye  
Siku zote hebu kuwa, na maliyo utumiye  
Usibali kukemewa, na hadhi wakuvunjiya  
Kwa chako taheshimiwa, ukinyeta wasikiye  
Kila muacha samboye, huwa sawa baharia

Usitupe arihami, akraba kuwa naye  
Huyo ndiye yako nyemi, kaa umfikiriye  
Dhilani atakuhami, huwa mtu na nduguye  
Dunia hii nyangumi, hutaka mwenye samboye  
Kila muacha samboye, huwa sawa baharia

Siku si namna moja, kila siku ni sikuye  
Kukosa leo si hoja, jikunyate utuliye  
Barakazo zinakuja, za wendo sisafiriye  
Hivo ndivo wavotaja, wahenga ufikiriye  
Kila muacha samboye, huwa sawa baharia  
Kila mtu ni rubani, ni nahodha wa seraye  
Hakuna bora machoni, kuliko wewe nay yeye  
Kigongo chako si duni, cha yule sikimbiliye  
Mwenda juu na chini, si mkata maishaye  
Kila muacha samboye, huwa sawa baharia

### USAWA

Weume msiudhike, swali nawaulizia  
Wala msibabaike, hadhi yeti natetea  
Kuwatweza wanawake, hamuoni mwakosea?  
Wanawake wawe sawa, na waume duniani

Si vizuri kuwatesa, wanawake kuonea  
Kuwapinga pasi kosa, kwa hatika ni hatia  
Nyote mna sawa hisa, katika hii dunia  
Wanawake wawe sawa, na waume duniani

Mngakaa mfikiri, lau kwa miaka mia  
Na muwache ujabari, wanawake si ngamia  
Sidanganywe na mahari, msambe ni kununua  
Wanawake wawe sawa, na waume duniani

Madharau huwa mengi, kwa waume narudia  
Huwawekea vingi, wanawake kila njia  
Kwa waume hawasongi, fikira zao kutoa  
Wanawake wawe sawa, na waume duniani

Usawa tunautaka, siyo hivi kubagua  
Tufanye mambo shirika, hakuna wa kubakia  
Kubaki nyuma twachoka, waume kutangulia  
Wanawake wawe sawa, na waume duniani

Kila alo mwandamu, kwa Muumba katokea  
Kwani wote wana damu, ni wamoja wa hisia  
Bora wote kuheshimu, bila umbo kutengua  
Wanawake wawe sawa, na waume duniani

Usawa tunaotaka, si wa umbo na kuva  
Wala si wa kugeuka, kuota ndevu vifua  
Ni ule wa kutukuka, kwenye utu na tabia  
Wanawake wawe sawa, na waume duniani

Wengine wana shutuma mabibi kushambulia  
“Roho zao ni Tamima, ni Wepeso wa kulia  
Hawawezi kusimama, vita vinapotokea”  
Wanawake wawe sawa, na waume duniani

Waume vuta akili, nguvu si kujivunia  
Mnapaswa kubadili, dhana zenu na tabia  
Hakuna mtu dhalili, elimu yetu sawia  
Wanawake wawe sawa, na waume duniani

Nimeutaja usawa, nadhani mumesikia  
Kama sahani na kawa pima utu na hisia  
Kwa ujenzi twatakiwa, kina mama na raia  
Wanawake wawe sawa, na waume duniani

Shairi hili nilixhukua kama risala changamoto kwa ajikia ya mkutano mkuu wa MUONGO WA KINA MAMA Mwezi Julai, 1985, Jijini Nairobi. Na kwa mara ya kwanza lilighaniwa kuadhimisha mwaka wa kina mama 1983 na Wanaza binti mutual wa misyani kangundo.

#### MWANANCHI NA MZALENDÖ

MWANANCHI  
Ingawa ni nchi yangu, mie siipendi sana  
Ina tando la ukungu, kadha mawimbi mapana

MZALENDÖ  
Wewe u mwana wa wapi, ni bora kujulishana  
Msimamo wako upi, imara uloshikana?

**MWANANCHI**

Hayo ni maswali gani, au tunataniana?  
Hunijui toka lini, mzawa mjulikana!

**MZALENDÖ**

Sura yako naijua, ila kadhai hapana  
Vile navyokutambua, sivyo ninavyokuona

**MWANANCHI**

Mimi usinitazame, angalia kila kona  
Si wake na si waume, vile wavyozongeana

Ni vurugu na hujuma, si wazee si vijana  
Hatokezi mti mwema, msafi aso laana?

Watoto waliosoma, si watu ni subuhana!  
Pa kutolea huduma, wanaenda kujivuna

**MAZLENDÖ**

Kweli unanishangaza, ni kama tunagombana  
Ama tunazungumza, bayana kuambizana?

**MWANANCHI**

Unakwea na kuwanda, wengine wakondeana  
Unachuma usopanda, kuhemera usovuna

**MZALENDÖ**

Nakuona una nyingi, tafakuri za maana  
Maneno yenyé msingi, bali doa ni la jana

Asubuhi na mapema, nuru ipotanzukana  
Giza jekundu kuhama, jeusi likatandana

Kwa Imani za welewa, nchi yetu ingapona  
Tungawenza kuokowa, namna unavyonena

### MWANANCHI

Hujawa kindakindaki, mzalendo mwungwana  
Abadi sikuafiki, koma kunidonadona

Jukwaani mpenda uma, huko chemba ndiwe ngwena  
Watafunu watu nyama, vijikongwe na watwana

Umesoma kitu gani, taaluma za kulana?  
Nchi yetu taabani, na shahada umebana!

Sije kwangu kunitubu, niko macho ninaona  
Damu yako ina tabu, osha utoea laana

Ati wewe mzalendo, mwenye tumbo limenona!  
Na madole yenygando, ya kuhujumu mchana!

Mimi ninakuachia, nisije nikajichuna  
Kemi zangu najutia, sitaki kutatizana

### NGONJERA: MISINGI YA MAENDELEO

#### MDADISI

Haya shime wananchi, la mgambo linalia  
Abadani sijifichi, mambo yamenilemea  
Kuwauliza siwachi, mwenye jibu nangojea  
Tujengeje Kenya Yetu?

Rais wetu kasema, kila mtu kusikia  
Wakenya tusiwe nyuma, nchi yetu kuinua  
Viongozi wa heshima, nao wito wametoa  
Tujengeje Kenya Yetu?

#### MTAMBUZI

Swali lako mwanakwetu, lanitoa kwenye ua  
Hilo swali la kiutu, lataka jibu murua  
Kuijenga Kenya yetu, nijaribu kujibia  
Na sasa ela sikia

Waziwazi nakweleza, ili upate elea  
Kenya kuiendeleza, si uchawi wala dua

Ni wajibu kutimiza, muongozo kufatia  
Viongozi wakitoa

#### MDADISI

Sijaelewa lakini, wajibu unonambia  
Nieleze kwa makini, name nipate sikia  
Siniache gizani, nikazidi kupotea  
Heri nionyeshe njia

#### MTAMBUZI

Takwambia mzalendo, ingawa nayarudia  
Mosi uwe na UPENDO, upende kila raia  
Moyo usiwe na fundo, taifa kutumikia  
Hakuna kujibagua

Sijafikia mwishoni, majibu kukupatia  
Kuna jambo la thamani, ni la pili zingatia  
Na kuishi kwa AMANI, bila kero na ghasia  
Kila mtu kutulia

#### MDADISI

Naomba kutaja moja, na mim kuongeza  
Ni ya kweli ulotaja, kwa nchi kujengea  
Bali muhimu UMOJA, kuunganika kwa nia  
Kama kichwa na mapua

Wananchi kutengana, si kujenga kubomoa  
Ni vigumu kupambana, adui akivamia  
Umoja nguvu mabwana, kwa taifa la huria  
Ni silaha kushindia

#### AJUZA

Wajukuu hamjambo  
WOTE: Hatujambo. Shikamoo  
Hoja zenu nasikia  
Ni kilio cha kitambo, mbali mlikoanzia  
Umoja kweli ni chombo, kwenye nchi kujengea  
Lakini nitawambia

Tukitaka kuungana, kila mtu na raia  
Lazima kuelewana, lugha moja kutumia  
Kenya tuna heri sana, Mungu ametujalia  
Kiswahili ndiyo njia

Tutumie Kiswahili, viongozi na raia  
Kwenye dhima mbalimbali, lugha hii inafaa  
Kisemwa kila mahali, watoto kufundishia  
Lugha ndiyo jumuia

Hayo mambo si ya mwisho, mengine nawatajia  
Lazima kutoka jasho, ili nchi kuinua  
Tatizo leo na kesho, uzembe kujitakia  
Fanya kazi kishujaa

Maendeleo tukitaka, kazi tuwe twakazia  
Maofisi tukifika, tuhakikishe twakaa  
Sio koti kutundika, kwenye kitu kuachia  
Uvivu huleta njaa

Mkulima shika jembe, shambani kupalilia  
Mazazo mengi tusombe, wanetu kuhudumia  
Tule mlo lembelembi, tupate nyingi afia  
Na watoto kuwale

Watoto wote wasome, ujuzi kujipatia  
Na wasiende kinyume, adabu wakakosea  
Walimu wafanye shime, watoto kuwapa njia  
Ya nidhamu kupidia

#### MDADISI

Nashukuru waungwana, tata unitatulia  
Mwangaza nimeuona, na wajibu kutambua  
Wakenya wote ungana, taifa kuhudumia  
Nyuma tutafurahia

### KISWAHILI NAIROBI

Nilifika Nairobi, jiji bora na mufti  
Palipojaa shababi, wazee na mabenati  
Nikasalimu kibibi, kanijibu eti fiti!  
Vijana na mabenati, kipi Kiswahili hiki?

Kibibi kasonga kwangu, nimpe kitit asiti  
Nikaona mbele yangu, kwa mapozi kajiseti  
Sikupatwa na uchungu, wala chembe kibuhuti  
Vijana na mabenati, kipi Kiswahili hiki?

Kumwuliza wenda wapi, kanijibu marikiti  
Kwenye kazi au vipi, jibu lake nina deti  
Ana majibu mafupi, na taimu hawesti  
Vijana na mabenati, kipi Kiswahili hiki?

Mtu huyu hushangaza, lugha yake sijageti  
Hataki kunisikiza, ati mimi sina senti  
Bila doo aeleza, yu tayari kunibuti  
Vijana na mabenati, kipi Kiswahili hiki?

Punde dakika kidogo, nikaanza utafiti  
Naona ana mikogo, na haogopi umati  
Hawataki wa ushago, wenyet koti bila noti  
Vijana na mabenati, kipi Kiswahili hiki?

Ni kibibi maridadi, ila mambo tofauti  
Asema mboga si fudi, bwana kunipa donti  
Chuma mobu sina budi, kujaza langu poketi  
Vijana na mabenati, kipi Kiswahili hiki?

Ana fujo hatulii, sijaonapo laity  
Arifu hunibaii, kamsosi hata switi  
Ebu acha uchalii, uchi homu kwa kufuto  
Vijana na mabenati, kipi Kiswahili hiki?

Na kutaka kualee, akawasha sigareti  
Hamuogopi madhee, asije kumripoti  
Pegi mbele ya fadhee, mkali kama ghosti  
Vijana na mabenati, kipi Kiswahili hiki?

Alipozidi udhi, nikaanza kumsweti  
Naye akaniwevia, kuniona simfati  
Sistee kaingia, kwa motii kalosti  
Vijana na mabenati, kipi Kiswahili hiki?

Nikabaki kudangana, la kusema silipati  
Lugha zetu kulingana, hakuna japo katiti  
Ndipo hatukwelewana, hadi kuenda benati  
Vijana na mabenati, kipi Kiswahili hiki?

Kudadisi kwa makini, tabia na harakati  
Za vijana wa mijini, zina nyingi atiati  
Tafadhali jikanyeni, ni huu ndio wakati  
Vijana na mabenati, kipi Kiswahili hiki?

Hunishangaza jamani, tuelezane kwa dhati  
Nairobi mitaani, pa watu watanashati  
Panasemwa lugha gani, na kanuni haifati!  
Vijana na mabenati, kipi Kiswahili hiki?

#### TUTUKUZE KISWAHILI

Kwa heshima nasimama, kujificha sikubali  
Ntiamke himahima, mambo yaliyo ya kweli  
Bayana neno nasema, tutukuze Kiswahili  
Kiswahili kitukuzwe, kwani lugha ya Taifa

Baba mama na vijana, ndugu zangu waadhma  
Lugha kitu cha maana, kila nchi ni hashima  
Watu wanapokutana, bila lugha watakwama  
Kiswahili kitukuzwe, kwani lugha ya Taifa

Mungu asiye na chuki, karama zake kafanya  
Afrika mashariki, lugha bora ikapenya  
Kwa nini nyuma tubaki, lugha hii kutawanya  
Kiswahili kitukuzwe, kwani lugha ya Taifa

Kitukuzwe Kiswahili, wala tusikidharau  
Ghana mpaka Somali, kizungumzwe falau  
Kikasemwe kwelikweli, kisikie angalau  
Kiswahili kitukuzwe, kwani lugha ya Taifa

Kiswahili kiwe chombo, kipige mbio za gari  
Kivuke kifike ng'ambo, huko nyuma ya bahari  
Na huko ndugu wa kambo, wapate kukikariri  
Kiswahili kitukuzwe, kwani lugha ya Taifa

Tukiseme Kiswahili, kwa fasaha na nahau  
Tuandike kwa fasili, tukitunze sidharau  
Si muda wa siku mbili, tuwe tumekisahau  
Kiswahili kitukuzwe, kwani lugha ya Taifa

Kifanyiwe mapinduzi, kila tulipoptoka  
Walimu na wanafunzi, uzi' moja tungeshika  
Tufanya kubwa panuzi, kila pembe kutumika  
Kiswahili kitukuzwe, kwani lugha ya Taifa

Wakhatabahu tamati, muda umenipungua  
Jambo kubwa na la dhati, lugha yetu kuinua  
Na sote tujizatiti, Kiswahili kupanua  
Kiswahili kitukuzwe, kwani lugha ya Taifa

Shairi hili nililitunga nikwa mwanafunzi wa kidato cha kwanza. Lilimbwa kwa mara ya kwanza na Fatma Abdallah wa Kenya High (Nairobi) 1976 katika Masshindano ya kwanza ya Sanaa ya Kiswahili katika shule ya pangani (Nairobi). Na hivi sasa ahairi hili linatumwiwa na sauti ya Kenya kuanzisha vipindi vyta Sanaa ya Kiswahili radioni na katika televisheni.

### AFRIKA MAMA YETU

Amkeni kila pembe, sasa kumepambazuka  
Twanyanyaswa kama ng'ombe, hali giza latoweka  
Damu moto tujisombe, sote wana Afrika  
Bara zima tuungane, tukomboe Afrika

Kwenye heri au shari, ukombozi tunataka  
Bara lote liwe huri, Afrika kutukuka  
Ubaguzi ni hatari, ni unyama wa tabaka  
Bara zima tuungane, tukomboe Afrika

Tukomboe bara letu, viongozi wasifika  
Dumisha umoja wetu, nchi huru Afriak  
Umoja ni ngao yetu, hatutaki kutengeka  
Bara zima tuungane, tukomboe Afrika

Sote tunajua vyema, mama yetu Afrika  
Tena tumpe uzima, kubwa usiopimika  
Kwa kuondoa unyama, wa kusi na vibaraka  
Bara zima tuungane, tukomboe Afrika

Vijana tangulieni, mbele bila kugeuka  
Misiri hadi Kusini, Mulikeni Afrika  
Kaburu na mahaini, kuwatia hekaheka  
Bara zima tuungane, tukomboe Afrika

Ukoloni- mamboleo, na ubwana tumechoka  
Wenyeji na wengineo, ni mabomu kufyatuka  
Maovu si marejeo, tusirudi tukotoka  
Bara zima tuungane, tukomboe Afrika

### MIAKA KUMI YA CHAMA CHA KISWAHILI

Napenda kusimulia, kisa hiki cha kweli  
Vile kiliviyotukia, miaka kumi awali  
Walimu kuitikia, kubuni chama kamili  
Chama chetu Kiswahili, kimetimu myaka kumi

Myaka kumi yatimia, walipokata kauli  
Wakufunzi wenyе nia, kutetea Kiswahili  
Ndipo walipoamua, chama kiwa jiji hili  
Chama chetu Kiswahili, kimetimu myaka kumi

Madhumuni nawambia, chama hiki kusabili  
Kuunganisha waria, walimu wa Kiswahili  
Waweze kuipanua, lugha hii ya asili  
Chama chetu Kiswahili, kimetimu myaka kumi

Na katika kupanua, wadhifa wa Kiswahili  
Walimu waliamua, Chama chao kusajili  
Kwa Mkuu wa sharia, wakapata ikibali  
Chama chetu Kiswahili, kimetimu myaka kumi

Tangu chama kuanzia, hadi leo kuwasili  
Kina mengi manufaa, kwa wasomi wa skuli  
Mitihani kutungia, na shindano kama hili  
Chama chetu Kiswahili, kimetimu myaka kumi

Ni nguzo ya kuringia, umoja wa Kiswahili  
Walimu twawasifia, waanzishi wa awali  
Na wanaoshikilia, kuziongoza shughuli  
Chama chetu Kiswahili, kimetimu myaka kumi

Mwisho wangu ninatua, tutukuze Kiswahili  
Kenya tunashangilia, twapongeza serikali  
Kiswahili kutambua, na kuwa somo kamili  
Chama chetu Kiswahili, kimetimu myaka kumi

Shairi hili lilitungwa kwa heshima ya mwenyekiti wa chama cha walimu wa Kiswahili, Nairobi bwana Josephat Mshanga (Don Bosco) kwa ajili ya mashindano ya Sanaa ya Kiswahili ya maadhi misho ya miaka kumi ya chama cha kiswahili Nairobi 1975-1985.

MIAKA ISHIRINI YA UHURU

Rabana namshukuru, Rahimu mwenye Baraka  
Mola ndiye muamuru, wa furaha na mashaka  
Katufanya tuwe huru, na madhila kuepuka  
Shangwe kutimu miaka, ishirini ya uhuru

Tulieni tudhukuru, ya nyuma tulikotoka  
Kusema sijakufuru, jinsi tulivyoteseka  
Alipotawala beberu, na heshima kutoweka  
Shangwe kutimu miaka, ishirini ya uhuru

Tulilia chururu, chozi tele kumwaika  
Wakatoka barubaru, Wakenya wasoshituka  
Wakaudai Uhuru, kwa mapanga na mashoka  
Shangwe kutimu miaka, ishirini ya uhuru

Wakasema haidhuru, vita kufa kuponyeka  
Toka pande za limuru, hadi mara kwenye nyika  
Wazee wenyе mararu, na vijana kutimka  
Shangwe kutimu miaka, ishirini ya uhuru

Punde kukurukukuru, za vita kali kuzuka  
Wakenya kama kifaru, wakoloni kuwasaka  
Wakenda hadi Nakuru, mashamba wakayateka  
Shangwe kutimu miaka, ishirini ya uhuru

Mzungu kujinusuru, alianza tetemeka  
Akili zikamduku, hakujua taokoka  
Akaona haidhuru, Kenya nitapatoweka  
Shangwe kutimu miaka, ishirini ya uhuru

Tamaa ilimdhuru, Beberu kudanganyika  
Akatoza na ushuru, apate kutajirika  
Wakenya watu, sin guru, kuuza kwenye maduka  
Shangwe kutimu miaka, ishirini ya uhuru

Baada ya kuwa huru, tukapata madaraka  
MZEE twamshukuru, angawa ametutoka,  
Ni wa kwanza kuamuru, na Wakenya kukomboka  
Shangwe kutimu miaka, ishirini ya uhuru

Hatutaki paruparu, wala mambo ya dhihaka  
Anoleta varuvaru, tu tayari kumbaka  
Voi, Nandi na Ruiru, sote tumeunganika  
Shangwe kutimu miaka, ishirini ya uhuru

BWANA MOI ndiye nuru, taa ya kutumulika  
Kila kona anazuru, hadi nje ya mipaka  
Atuone twafuturu, chakula tunatosheka  
Shangwe kutimu miaka, ishirini ya uhuru

Wakenya tusikufuru, utumwa umetoweka  
Tujione tuko huru, wazalendo watukuka  
KANU mama wa uhuru, ndiyo nguzo ya kushika  
Shangwe kutimu miaka, ishirini ya uhuru

Furahini Kenya huru, mwisho wangu nimefika  
Turuke kama kunguru, kwa umoja na kucheka  
Waluhya hata wameru, Kenya moja tunataka  
Shangwe kutimu miaka, ishirini ya uhuru

**HONGERA RAIS MOI**  
Kwa uwezo wa Rabuka, Mola aliye mbinguni  
Katujazia Baraka, bara hadi baharini  
Ametupa msifikasi, Baba Moi Mhisani  
Rais Moi hongera, uongoze Kenya yetu

Ni mengi tumeyaona, alotenda Mhisani  
Nchini ajulikana, ni mwenezi wa Amani  
Mola ampe mwawana, aendelee nchini  
Rais Moi hongera, uongoze Kenya yetu

Rais Moi aishi, aushike usukani  
Jemadari wa majeshi, kiongozi wa vitani  
Kenya hatuna ubishi, twamfata kwa Imani  
Rais Moi hongera, uongoze Kenya yetu

Tumfate baba Moi, maneno yake shikeni  
Mtukufu habagui, hupenda wote nchini  
Ukabila haufai, ni adui maishani  
Rais Moi hongera, uongoze Kenya yetu

Ameyafuta magendo, na ujisadi kazini  
Anahubiri upendo, umoja pia Amani  
Nasi tufatenu nyendo, za Raisi Mhisani  
Rais Moi hongera, uongoze Kenya yetu

Binadamu hatosheki, hilo pia twabaini  
Apewe nyama na keki, bado haan shukurani  
Lakini Moi kwa haki, hana choyo asilani  
Rais Moi hongera, uongoze Kenya yetu

Hufanya kazi kwa nia, wala hakai nyumbani  
Kila pembe hupitia, miji hadi mashambani  
Kusudi kusaidia, wananchi taabuni  
Rais Moi hongera, uongoze Kenya yetu

Mkarimu Baba Moi, kwa huruma hafanani  
Kusamehe hakatai, japo uwe gerezani  
Chuki kwake ni adui, haifai abadani  
Rais Moi hongera, uongoze Kenya yetu  
Uongozi wake mwema, toka Kenya hadi Gini  
Umoja kwenda mrاما, wan chi huru barani  
Ni Moi alisimama, Africka kuauni  
Rais Moi hongera, uongoze Kenya yetu

Ashara beti natua, mshairi wa ziwani  
Nyayo nimemmsifia, kwa ukweli si utani  
Mengi ametutendea, tunayaona machoni  
Rais Moi hongera, uongoze Kenya yetu

**KENYA TUNAYOTAKA**  
Hapa tulipofikia, tumshukuru Manani  
Taifa latungojea, tasahau ya zamani  
Jambo la kuzingatia, tuunganeni nchini  
Kenya tunayoitaka, sisi sote kuungana

Tusikumbwe na dunia, tukaingia vitani  
Ni bure kujichukia, ni maisha ya mashakani  
Wakenya wote sawia, na tusihi furahani  
Kenya tunayoitaka, sisi sote kuungana

Raisi kahutubia, tupendaneni nchini  
Tena ametuambia, ubaguzi kitu duni  
Shida haitotokea, ukimpenda jirani  
Kenya tunayoitaka, sisi sote kuungana

Umoja nguvu sikia, ni kinga ya kuamini  
Nchi yetu kuinua, bora tuwe na Amani  
Ndipo tutatendelea, tusitwe masikini  
Kenya tunayoitaka, sisi sote kuungana

Aliye mwema raia, si mvivu si haini  
Hufanya kazi kwa nia, mijini hata shambani  
Kenya nchi ya mbolea, bara hadi baharini  
Kenya tunayoitaka, sisi sote kuungana

Beti sita naishia, kuhusu wito nchini  
Wanafunzi nawambia, msome sana shulenii  
Kenya inawangojea, viongozi wa usoni  
Kenya tunayoitaka, sisi sote kuungana

**VIVA KRISMASI**  
Rabana ulete heri, kila pembe ya janibu  
Tuepushe yenyeshari, tusipate masaibu  
Dunia ni maghururi, mambo yake ni dharubu  
Krismasi karibu, na mwaka uwe na heri

Tujivue na hatari, za maovu na aibu  
Kila mwenye tafakuri, afanye wema gahlibu  
Kenya ni taifa zuri, wazalendo mahabubu  
Krismasi karibu, na mwaka uwe na heri

Mungu ametunusuri, vijana na kina babu  
Hadi mwaka kusafiri, kwa sahali na sulubu  
Tama mbele ya Jabari, pasi janga kutusibu  
Krismasi karibu, na mwaka uwe na heri

Yalopita sifikiri, kwetu hayana tulubu  
Tujenge Kenya ya shwari, ya udugu masahibu  
Mola ametusetiri, faraka tusijaribu  
Krismasi karibu, na mwaka uwe na heri

Siku hiyo mashuhuri, tutekeleze wajibu  
Tufanye mambo mazuri, sio chuki na ghadhabu  
Tuwe mbali na kiburi, maisha ni taratibu  
Krismasi karibu, na mwaka uwe na heri

Krismasi kujiri, iwe siku ya kutubu  
Tusijidai hodari, mafahali wa vilabu  
Furaha si uchakari, na uchafu wa harabu  
Krismasi karibu, na mwaka uwe na heri

Mwakani tuwe tayari, matatizo kutanibu  
Kazi inatushubiri, kuona tumeratibu  
Kila dhima kwa kadiri, kufatia taratibu  
Krismasi karibu, na mwaka uwe na heri

## MASWALI YA MAREJERO

Dhamira kuu ya maswali haya ni kumwongoza na kumwelekeza msomi wa mashairi ya diwani hii ili kuweza kutandua pazia la gubiko la mtunzi naye abakie kuta wala maudhui, madunzo, mwelekwo, msimamo, miundo na mikondo mbalimbali ya Sanaa zilizotumika katika ushairi huu. Licha ya kuwa ni maswali yenye manufaa kwa mwanalugha na mwanafasihii, pia yatamfaa vikubwa msomaji mchambuzi na mhakiki yejote wa tungo za mashairi kwa jumla.

## KIKOWA

1. Taja mbinu zilizotumika katika kulitunga shairi hii.
2. Nini maana ya “KIKOWA”? Eleza kwa nini mtunzi ameliita shairi hili KIKOWA?
3. Eleza kwa tafsili ujumbe unaojitokeza katika kila ubeti.
4. Methali gani ya Kiswahili ambayo hisia zake zinapatikana kwenye ubeti wa 3?
5. Eleza kwa fasaha maana halisi ya mafungu haya ya maneno:
  - a) Mambo ni kikowa
  - b) kulia ngowa
  - c) kutoa mtima
  - d) kuchanga utendi
  - e) dunia ni watu

## GANDA JEUSI

1. “Ganda Jeusi” lipi ambal mtunzi analizungumzia?
2. Mtunzi anatoa sababu zipi katika kulipenda ‘Ganda Jeusi’?
3. Fichua hisia ya kizalendo iliyofichwa katika shairi hili.
4. Taja Sanaa iliyotumika kulitunga shairi hili.
5. Eleza vivazi hivi huvaliwa na watu gani katika nchi yako:
  - i. utunda
  - ii. kigesi
  - iii. uwinda

## UZALEENDO

1. (a). Mzalendo ni nanni? (b). Taja kinyume cha mzalendo.
2. Taja sifa na majukuu ya mzalendo kuhusu nchi yake.
3. Kisanaa shairi hili huitwa MKARARAGUNI. Fafanua.
4. Eleza hawa ni kina nani? Kisha utaje ni wepu katika yao ni wazalendo na wepi si wazalendo, na kwa nini si wazalendo.  
Kibaraka, barakala, jasusi, kikaragosi, msaliti, mlangazi, bepari, kabilia, jemadari, tabibu, mkalimani, lifuoto, mkulima, malenga na mwalmi.

### TUFANYE KAZI

1. Kwa nini tunahimizwa tufanye kazi? Taja masaibu yanayoweza kuleta na uzembe nchini.
2. Nchi yakeo huchukua hatua gani kwa wafanya kazi wazembe? Eleza kwa kirefu.
3. Kwa nini ukulima umeitwa ‘Kazi ya Malezi’ (ubeti wa 6)
4. Jadili maana ya kauli hizi za wahenga:
  - i. kazi ni uhai
  - ii. uvivu ni nyumba ya njaa
  - iii. mvunda nti ni mwanati
  - iv. kilimo ni utu wa mgongo wa uchumi wa taifa letu.
5. Eleza jinsi wito wa Harambee unavyosiadi kuinua hali ya masiha ya wazalendo wa Kenya.

### TUMEHIARI

- 1) Taja umuhimu wa wito unaoonagelewa katika shairi hili na ulezee jinsi wazelendo wa Kenya walivyopokea.
- 2) Simulia manufaa makubwa yanayopatikana kutokana na mfumo wa elimu ya NAKE NNE NNE.
- 3) Eleza dhamira ya beti mbili za mwisho.
- 4) Fafanua msamiati huu:
- 5) Kwa nini mtunzi amekiuka kanunia ya sarufi na kuandika “Miaka nane..” baadala ya “Miaka minane...”?

### UTAMADUNI

- 1) Nini maana ya ‘Utamaduni’? Fafanua.
- 2) Taja mambo ambayo ni msingi wa utamaduni kama yanavyodokezwa na mtunzi.
- 3) Taja athari na mambo makubwa yanayotatiza utamaduni wan chi xa kiafrika.
- 4) Je, nchi ya Kenya inachukua hatua gani za kudumisha utamaduni wa wazalendo? Dokeza matatizo yanayokabili juhudhi hizo.
- 5) Eleza kwa jinsi gani utamaduni umefananishwa na rramani? (ubeti wa 5)

### KILA MUACHA SAMBOYE

- 1) Taja lengo la beti za shairi hili.  
Hawa ni kina nani? arihami, akraba, wendo, rubani, ndhodha na mkata.
- 2) Taja methali moja maarufu inayochukuana kimaudhui na?
- 3) Chungua maneno yaliyoendelezwa katika mbinu za tabdila, mazida na Inkisari kisha uyaandike katika mbinu za kawaada za lugha ya Kiswahili.

### USAWA

- 1) Jambo gani lililomkera mtunzi hata akaamua kulituinga shairi hili?

- 2) Watu wanaokataa kuwa wanawake si sawa na wanaumw wanatoa hoja zipi?  
Je, hizo hoja zao ni za kweli? Jadili.
- 3) Taja msingi mine ya usawa wa binadamu duniani.
- 4) Msemaji wa shairi hili anatoa rai zipi katika kujibu madai ya wanaume?
- 5) Kwa nini wanawake walikutana Nairobi mwaka 1985?

#### MWANANCHI NA MZALENDÖ

- 1) Taja mikondo miwili ya usanii iliyotumika kulitunga shairi hili.
- 2) Taja madhumuni ya malumbani kati ya Mzalendo na mwanachi katika shairi.
- 3) Unadhani ni kwa nini mzalendo ameshindwa kuendelea Zaidi kujadiliana na mwenziva mwanaxhi? Fafanua kwa nathari kauli za mzalendo katika beti zake tatu za mwisho.
- 4) Tumia masmiati ufuatao kudhihirisha maana halisi. kadhia, mzawa, zongeana, hujuma, kuwands, tazukana, kindakindaki.

#### NGONJERA

- 1) Je, tunataka Kenya ya aina gani? Eleza jinsi tunavyoweza kujenga nchi inayopendeza kwa kila raia.
- 2) Upendo, Amani na umoja yametajwa kama mambo muhimu katika ujenzi wa taifa leat. Thibitisha ukweli huu.

#### KISWAHILI NAIROBI

- 1) Taja lengo kuu la kulitunga shairi hii.
- 2) (a) Taja mambo mahususi yanayoathiri Kiswahili cha Nairobi.  
(b). Ni mbinu gani zinazokabili kutumiwa ili kuondolea mbali hatari na athari zinazokabili lugha ya Nairobi na miji mingine kwa jumla?  
(c). Andika kila ubeti kwa lugha sanifu ya nathari.
- 3) Mtunzi amefaulu vipi katika kusawiri dhamri yake kwenye shairi hili? Taja tamthilia iliyomo ndani ya shairi hili.
- 4) Jahili hoja zifuatzao: (i) Vijana wa siku hizi ndio wanaochafua na kuharibu utamu wa Kiswahili kwa kukuchanganyachanganya na lugha za kigeni. (ii) Mtu anayeongea kwa kuchangangya lugah hana lugah rasmi anayoimudu.

#### TUTUKUZE KISWAHILI

- 1) Taja njia tunazoweza kutumia kutuuza na kukuza lugha ya Kiswahili.
- 2) Eleza jinsi Kiswahili ‘kilivyopenya’ Afrika mashariki.
- 3) Mtunzi adokezea kuwa tabu gani inetukabili lau tungkuwa hatuna lugha?
- 4) Eleza jinsi lugha ya Kiswahili inavyotoa mchango mkubwa katika umoja watu.
- 5) Fafanua ubeti wa sita kwa lugha ya riwaya.

### AFRIKA MAMA YETU

- 1) Eleza ujumbe wa kila ubeti.
- 2) Taja wito wa aina tatu unaotolewa na msahiri. na kila wito ni wa watu gani?
- 3) Taja jazanda iliyotumika kwenye shairi hili.
- 4) Eleza vifungu hivi:
  - i. damu moto tujisombe
  - ii. umoja ni ngao yetu
  - iii. maovu si marejeo

### MIAKA KUMI YA CHAM CHA KISWAHILI

- 1) Taha huduma za xama kinachotajwa kwenye shairi.
- 2) Taja faid za kuwa na chama cha Kiswahili nchini.
- 3) Je, mna chama cha kswahili shulen i kwenu? Eleza harakati zake na jinsi kinavyoendelea kuwashudumia.
- 4) Simulia jinsi serikali yako inavyosaidia kukuza Kiswahili.

### MIAKA ISHIRINI YA UHURU

- 1) Taja juhud za wazalendo katiak kuikombo Kenya.
- 2) Taja dhuluma walizotendewa wanachi hata wakaamua kupigania uhuru.
- 3) Fafanua ubeti wa 8 na 10 kwa nathari.
- 4) Taja silaha kubwa iliyosaidia sana katika kuleta ukombozi wa Kenya.
- 5) Nini maana, ya: tudhukuru, beberu, chururu, baruharu, mararu, paruparu, kukurukuru, varurvaru, duru.

### HONGERA RAIS MOI

- 1) (a). Eleza wasifu wa Rais Moi.  
(b). Taja huduma ambazo ametolea Kenya katika harakati zake za kuinua hali ya maisha ya wazlendo.
- 2) Dondoa mamaboa maalum yanayodhahirisha kwamba Rais Moi anawahu dumia wanachi kwa dhati ya moyo wake.
- 3) “Usiulize Kenya imekusadia nini bali jiulize wewe umeitendea nini au umeisaidia vipi”?  
Jadili kauli hii ya kizalendo.

### VIVA KRISMASI

- 1) Mshairi anatupa mawaidha ggani kutoka Shairi Lake?
- 2) Anatakanya tujiepushe na mambo yapi wakti wa krismasi?
- 3) (a). Kwa nini ghasia, ajalo na maafa mengi hutokea wakati wa Krismani?  
(b). Toa maoni kuhusu “Krismasi Njema”.

- 4) Mizani ni nini katika shairi? Kubwagizo cha shairi hili kina mizani ngapi?
- 5) Nakili vina vya MLEA wa ubeti wan nne.

#### MASWALI YA MSETO

- 1) Eleza jinsi tungo za sehemu hii zinavyofungamana na Uzelendo.
- 2) Simulia namna babu zetu walivyowafunza watoto wao zamani kabla ya elimu ya shulenii kutamalaki nchini kwetu. Linganisha njia walizotumia na za kisasa kisha utoe maoni yako.
- 3) “Mwacha mila ni mtumwa” Eleza maana ya msemo huu.
- 4) Eleza kwa nini lugha huitwa kioo cha utamaduni?
- 5) Kwa nini serikali ya Kenya inahimiza matumizi ya Kiswahili? Na inachukua hatua zipi kuhakikisha kuwa Kiswahili kinakua na kuimarika? Je, hatua hizo zinatosheleza azma kuu ya kukikuza Kiswahili nchini? Toa maoni yako.
- 6) Taja vikwazo na matatizo yanayoikabili lugha ya Kiswahili katika kukua na kuenea kwake kisha dokeza mbinu tunazoweza kutatatua matatizo hayo.
- 7) Je, fasihi ni nini? (a). Eleza vipengele vya fasihi. (b). Taja aina mbili kuu za fasihi.
- 8) Jadili msemo huu: “Ukitaka kuua utamaduni wa jamii Fulani, kwanza angamiza fasihi yao”. Kisha dokeza jinsi mbinu hii ilivyotumiwa na wakoloni katika nchi yako.

## NASAHA NA MAASO

*Watani wetu jamaa*

*Leo tupate wasaa*

*Tabirizi na kukaa*

*Tukanyane yasofaa*

*Tujiepusha na chuki*

## TENDA HAKI

Tenda haki

Ni mapendo yake Mungu, Jabari

Alotugawa mafungu, tayari

Akatupa ulimwengu, fahari

Tenda haki

Usijitie tewengu, suduri

Ukaja pata uchungu, jibari

Siandame walimwengu, ayari

Tenda haki

Ushike wasia wangu, hodari

Sipite kwenye ukungu, hatari

Pitia penye uchengu, wa shwari

Tenda haki

Kuna watu nungunungu, fikiri

Wenye miiba michungu, hanjari

Jiambaze ja kulungu, hadhari

## ULIMI

Ulimi salama yako, chombo cha kukuongoza  
Huleta faida kwako, hasa ukiwelekeza  
Katika kila tamko, na katika kueleza  
Tumia ulimi wako, kwa akili na kuwaza

Hadhari kinywani mwako, hutoshya kutengeneza  
Mapito na nyendo zako, jina lako kupendeza  
Na watu wakaja kwako, sufufu kukupongeza  
Tumia ulimi wako, kwa akili na kuwaza

Katika uneni wako, nena nyuma ya kuwaza  
Usijezua chafuko umati ukakubeza  
Ulimi hasidi yako, hasa unapoteleza  
Tumia ulimi wako, kwa akili na kuwaza

Chuja sana matamko, unayotaka tangaza  
Yasilet machafuko, mawazo ya kuchukiza  
Ulimi una vituko, ni nyama ya kushangaza  
Tumia ulimi wako, kwa akili na kuwaza

Ulimi hatari yako, dawamu huangamiza  
Huvyaza msukosuko, hasara usiyoweza  
Akapatwa na kimako, na mwili ukalegeza  
Tumia ulimi wako, kwa akili na kuwaza

Maneno ni siri yako, hayatoki ukimeza  
Na kama jema haliko, afadhalii kunyamaza  
Tumia ulimi wako, kwa akili na kuwaza

Neno lina chokochoko, ni muhimu kuchunguza  
La uchungu likiwako, halikosi la kupoza  
Usitowe matapiko, duni katika baraza  
Tumia ulimi wako, kwa akili na kuwaza

### KESHO WEWE

Utendayo ni mabaya, yananikera niliko  
Amefikwa na hekaya, mwenzio ana sumbuko  
Badala kushika taya, ati kwak furahiko  
Wacha kucheka mwenzako, usije kupata haya

Kuna siku utagwaya, jihadhari na kicheko  
Usiseme haleluya, kuruka huku na huko  
Furaha ni kama ruya, haikosi badiliko  
Wacha kucheka mwenzako, usije kupata haya  
Sio utu ni umbeya, na haliwi burudiko  
Mtu kuwa ana maya, kwa Rabuka ni udhiko  
Utu mwema ni hidaya, aso nao nana koko  
Wacha kucheka mwenzako, usije kupata haya

Maisha kama unyoya, na dunia mzunguko  
Leo wamcheka moyo, kumbe kesho siku yako  
Sisi kwetu ni vibaya, kuchekana huwa mwiko  
Wacha kucheka mwenzako, usije kupata haya

Cheko sifa ya wabaya, wasojali pujuliko  
Tena ni yao wadoya, wanopenda machafuko  
Waendao kila kaya, kufanya vyao vituko  
Wacha kucheka mwenzako, usije kupata haya

Mwenzako awaywaya, hana hata pa mashiko  
Amefikwa na manaya, were kwako ni chereko  
Hata kama ni kinaya, mimi kwangu ni kimako  
Wacha kucheka mwenzako, usije kupata haya

Nimefika kwenye koya, na wewe koma kicheko  
Usije pata hizaya, jiulize uendako  
Jifunze kushika taya, atesekapo mwenzako  
Wacha kucheka mwenzako, usije kupata haya

Shairi hili limewahi kutumiwa katika mashindano ya Sanaa ya Kiswahili, Nairobi kwa miaka miwili mfululizo (1985 na 1986)

### ASASI

Jenga msingi bora  
Msingi wa kila jambo, muhimu kulik mwisho  
Ndio huleta mapambo, imara ya ukumbusho  
Ukianza kombokombo, hatima kuna vitusho

Jenga msingi bora  
Uteuzi wa awali, hufikisha mwisho mwema  
Kuteleza sikubali, chanda ukaja kiuma  
Uteue kwa akili, iliyojaa hekima

Jenga msingi bora  
Hili nimelibukua, kwa waliopaprika  
Hatua wakachukua, kwa vishindo na haraka  
Pasipo na kuchungua, wakaikosa Baraka

Jenga msingi bora  
Si kwa ndoa si kwa kazi, mwanzo ndio ufanisi  
Bora mwema uteuzi, sivyo hivyo kwa upesi  
Msingi uwe azizi, si mbovu wa wasiwasi

Jenga msingi bora  
Asasi dufu harara, aghalabu hujutisha  
Wala hakuna tijara, ni mayonzi kuzindisha  
Kujiasa ndiyo bora, dhila halijakutisha

### KIBURI

Pulika nikupe siri, njema sana ya kufata  
Nikuepushie shari, awali yawe kuguta  
Uadili si dosari, kuwa nao si ukata  
Kiburi si uungwana, jiepushe na kiburi

Mengi yanakusubiri, ya furaha na kujuta  
Tuza yako tafakuria, teua ya kukomata  
Ndueo ina hatari, jitanibu kuambata

Kiburi si uungwana, jiepushe na kiburi

Nakusihi ujibari, wacha njia ya salata  
Uraufu na kiburi, sawa maji na mafuta  
Kupatana havijiri, kama aridhi na nyota  
Kiburi si uungwana, jiepushe na kiburi

Bali suiwe jeuri, Kiburi kina matata  
Njia njema usawiri, usiwe mpenda vita  
Ndaro mama wa kaburi, hutia kwenye kiduta  
Kiburi si uungwana, jiepushe na kiburi

Ungawa mti fakiri, huna kuku wala bata  
Muradi uwe basiri, utang'ara kama nyota  
Wengi watakuhongeri, hapana wa kukusuta  
Kiburi si uungwana, jiepushe na kiburi

Siandame uayari, ukweli ukaubeta  
Ukajidai hodari, hakuna wa kukupita  
Dunia bwana la shari, waogao wanatweta  
Kiburi si uungwana, jiepushe na kiburi

Namaliza kuhubiri, nataraji utafata  
Uungwana una heri, alo nao si mkata  
Mithili yakwe dinari, utakacho utapata  
Kiburi si uungwana, jiepushe na kiburi

### SIMTUKANE MAMBE

Uwe mkali wa moto, na Jabari lenye gimba  
Au longo la ufito, mgumu japo mwembamba  
Unali ng'ambu mto, sithubutu kujigamba  
Usimtukane mamba, nawe hujavuka mto

Huna budi kuwa mato, domo lako ukafumba  
Upeskue ka uketo, magambo ya kuyagamba  
Mamba yumo mwenye mto, usimwite kikaramba  
Usimtukane mamba, nawe hujavuka mto

Shik nikiulezato, au atakula ngwamba  
Sijitie paramoto, watafuta kuwa kimba  
Subiri uvuke mto, pita pasi kumchimba  
Usimtukane mamba, nawe hujavuka mto

Uyastahi mapito, yake mwenye kuyapamba  
Sema naye kwa mvuto, kana kwamba wajikomba  
Akidai mpe koto, toa pasi na kulumba  
Usimtukane mamba, nawe hujavuka mto

#### NIDHAMU SHULENI

Furaha ya mwanadamu, ni heshima duniani  
Ungawa huna ilimu, adabu iwe makini  
Watu wote kuheshimu, utapendwa kwa yakini  
Mwananfunzi wa shuleni, adabu ni taa yako

Adabu ni kama mali, hutumiwa maishani  
Ndiyo sifa ya awali, kwa mwanafunzi shuleni  
Uwe nayo hulihali, ndipo wende masomoni  
Mwananfunzi wa shuleni, adabu ni taa yako

Usiwe mwana jeuri, kwa ndugu na majirani  
Ujerui ni hatari, ni majuto ya usoni  
Utaoona na hukiri, kama si leo mwakani  
Mwananfunzi wa shuleni, adabu ni taa yako

Uwaheshimu wazazi, na waalimu shuleni  
Siwabere wanafunzi, mnosoma darasani  
Pamopja muwe wapenzi, kama wana wa tumboni  
Mwananfunzi wa shuleni, adabu ni taa yako

Mkosefu wa adabu, haan raha ya uzoni  
Hali yake agahalabu, wasiwasi na huzuni  
Kufu yake ni adhabu, hafafulu mtigani  
Mwananfunzi wa shuleni, adabu ni taa yako

Hata kaam ndiwe bingwa, namba moja darasani  
Hapatikani mwanangwa, kukuweka kisongoni  
Adabuyo ikipingwa, huna bei wewe duni  
Mwananfunzi wa shuleni, adabu ni taa yako

Beti hizo naishia, kalamu nalaza chini  
Nadhani umeshika, nidhamu ina thamani  
Kadha inasaidia, sana kuliko mapeni  
Mwananfunzi wa shuleni, adabu ni taa yako

#### SIWANIE UKUU

Sioni ulichoshika, upande ule na huu  
Sipokuwa kuzunguka, ukitafuta ukuu  
Ni makuu unasaka, utavunjika maguu  
Siwanie kwenda juu, hata chini hukafika

Mpanda ngazi hushuka, kumbuka usemi huu  
Na pengine huanguka, asibukue nafuu  
Mbonawe Hujazinduka, mchana na mashekuu  
Siwanie kwenda juu, hata chini hukafika

Umaarufu wataka, ili uwe juu juu  
Bali nikikumulika, hukwi hata chuguu  
Kwenye ngazi taanguka, kwa kishindo chini puu!  
Siwanie kwenda juu, hata chini hukafika

Ungetaka faidika, ujaze lako bunguu  
Usiende kwa haraka, papara zina makuu  
Chembe chembe humuka, huleta tija shafuu  
Siwanie kwenda juu, hata chini hukafika

#### WASHAIRI HUPENDANA

Mhariri muadhma, wewe ndiwe muamuzi  
Mapatanishi wa umma, hakimu msimamizi

Naja kwako kwa heshima, kitabuni tubarizi  
Pandaneni watunzi, msiandame hasma

Uhasama sio mwema, na mshari hapendezi  
Shairi ni taaluma, ya dhukura na tambuzi  
Tumia kalmia njema, hasa nyingi wapambizi  
Pandaneni watunzi, msiandame hasma

Washairi tangu zama, za usuli wa wangozi  
Sio mno kusimama, kwa ghamidha za gombezi  
Matusi wakayasema, pasi kuwa na kinyezi  
Pandaneni watunzi, msiandame hasma

Nimeshtuka mtima, niliposoma majuzi  
Kwamba pana uhasama, dhidi chombo na Hijazi  
Nabaki kushika tama, shairi si uchokozi  
Pandaneni watunzi, msiandame hasma

Nyie nyote watu wema, vile ninavyomaizi  
Mu watunzi wa hekima, kale hadi siku hizi  
Leo vije mwasusuma, kwa ghamu za shambulizi?  
Pandaneni watunzi, msiandame hasma

Tafuteni usalama, myazike machukizi  
Khamisi chombo tuama, umsamehe Hijazi  
Mpe muda kuyapima, alonena ya upuuzi  
Pandaneni watunzi, msiandame hasma

Wasalamu nimekoma, tena kitu siongezi  
Bwana chombo akrama, usijali wachafuzi  
Vita siyo lelemama, vaa moyo wa mbawazi  
Pandaneni watunzi, msiandame hasma

### PAMBANO

Nakuletea mfano, ulo wazi wa busara  
Chomde zingatia mno, usijepata hasara  
Bora ufunge kiuno, wakati wa kurukara  
Ukiwa huna kitara, usuwanie pambano

Halina ndugu pambano, na tena halina dira  
Ni zogo na vurugano, machukivu na hasara  
Hapawi uelewano, usiende kama jura  
Ukiwa huna kitara, usuwanie pambano

Usifanye mnong'ono, shika haya madhukura  
Vita siyo kongamano, hutaka zana imara  
Shika japo msumeno, ukiwa huna kombora  
Ukiwa huna kitara, usuwanie pambano

Kondo ina mauano, na lukuki ya madhara  
Mumo mna machinjano, na mengi yanayokera  
Utakuja toka meno, ubakie kudorora  
Ukiwa huna kitara, usuwanie pambano

Usilale kama pono, sana anga linang'ara  
Si muda wa mabishano, tutakayo ni fikira  
Si ndaro na majivuno, tendo jema la tijara  
Ukiwa huna kitara, usuwanie pambano

Afadhalii konokono, apitaye akichora  
Humshiki kwa mkono, ute wake unakera  
Njia yake ndiyo hino, kinga kwake ilo bora  
Ukiwa huna kitara, usuwanie pambano

Yakabili mapambano, kwa adharusi imara  
Twaa japo ndoano, ama rungu na bakora  
Au ulale unono, kama huna cha kudara  
Ukiwa huna kitara, usuwanie pambano

### UNAFIKI

Tafutani usalama:  
Kunyamaza sitoweza, naona bora kusema  
Niketile nikawaza, fitina si mtu mwema  
Wengi wamejipoteza, husalia kulalama  
Hakuna haja kuzoza

Tafutani usalama:  
Leo nitawadokea, nanywi mpate yapima

Fatani ahilikiza, ni mbaya hana mema  
Kama wapinga uliza, masheha waliosoma  
Hakuna haja kuzoza

Tafutani usalama:  
Uwache kumpongeza, hasidi hana hashima  
Wengi wameteketeza, kwa maneno nyuma nyuma  
Ni bora kumfukuza, aondoke hima hima  
Hakuna haja kuzoza

Tafutani usalama:  
Basi fitina punguza, uwaze mbele na nyuma  
Dunia ni mageuza, tego hili utakwana  
Kwa janga ulilovskyanza, ukidhani unachuma  
Hakuna haja kuzoza

Tafutani usalama:  
Nia yangu si kuzoza, wala sitaki lawama  
Tangazo ninatangaza, tuishi pasi hasam  
Fitina haina jaza, ni ujinga si ulama  
Hakuna haja kuzoza

Tafutani usalama:  
Tama hapa nanyamaza, kwenda mbele kwanilema  
Fatani hela sikiza, kuna siku utahema  
Mno unajiumiza, upoteze na uzima  
Hakuna haja kuzoza

**MKATAA PEMA**  
Msambe naja kuteta, nina wema wa kalima  
Moyo wanikatakata, maini yangu yachoma  
Ili nipate takata, ukweli wote tasema  
Anayekataa pema, pabaya panamuita

Muacha pema hujuta, anedapo si salama  
Bahati ni kama nyota, humemeta na kuzima  
Sikimbilie mafuta, ukatate kula sima  
Anayekataa pema, pabaya panamuita

Haraka zina matata, angaza mbele na nyuma  
Tenda mambo kwa kusita, usije ukalalama  
Keti pako ukipata, kwa muradi wa uzima  
Anayekataa pema, pabaya panamuita

Pema si penye mafuta, au pa wali na nyama  
Pema watu hutafuta, utulivu na hekima  
Si hoja penye ukata, pa watu hali ya nyuma  
Anayekataa pema, pabaya panamuita

Mahali pema ambata, kwa vitendo na huduma  
Sikae penye matata, palipojaa hasama  
Lau kama pamemeta, hapafai kwa daima  
Anayekataa pema, pabaya panamuita

Bendera yangu nakita, pepea mahali pema  
Wenye macho wakipita, waoile na kutazama  
Mja moyo kutakata, usiishi penye njama  
Anayekataa pema, pabaya panamuita

#### KIJUNGU JIKO

Ninenay nimeona asilani si kuota  
Ni anagamizi bayana, kwetu sisi kutuseta  
Watu wanafumukana, asubuhi hujivuta  
Si kazi, sitirihali, tufanyazo waungwana

Pato zimetupungua, hali zetu huzorota  
Kupata hiso rupia, mahitaji yakung'uta  
Majumba kuyalipia, baki huwa za mafuta  
Si kazi, sitirihali, tufanyazo waungwana

Wapo wanaofaidi, wanaokula mafuta  
Wenye nyama za baridi, jorafuni zimenata  
Wanovaa maridadi, kwa lebasi za kumeta  
Si kazi, sitirihali, tufanyazo waungwana

Haya ninayoyasema, ni ya kweli ya kufata  
Kwenu wana mnosoma, msambe raha tapata  
Afadhali kwenda lima, kufuga kuku na bata

Si kazi, sitirihali, tufanyazo waungwana

Isiwajae huzuni, mimi yameshanipata  
Nimesoma kwa makini, mitihani nikapita  
Na kuingia mijini, kazi njema sikupata  
Si kazi, sitirihali, tufanyazo waungwana

Ninatamani kugura, nende shamba kutafuta  
Mijini kunanikera, nikalimie mbatata  
Kujibari ndiyo bora, ningali bado kujuta  
Si kazi, sitirihali, tufanyazo waungwana

Ijara yanagu si haba, bali sawa na mkata  
Nachelea kina baba, kuishi jiji kwatata  
Mahitaji hutukaba, na nauli siku sita  
Si kazi, sitirihali, tufanyazo waungwana

Tama fanyeni hadhari, watoto mnaofata  
Msije kutahayari, mkabakia kubwata  
Maisha siyo buheri, ni mazonge tena vita  
Si kazi, sitirihali, tufanyazo waungwana

### SIWINAO

Washari siwi nao, siwi nao sini, sendi waliko  
Sipendi wenyе ndweo, wasoona soni, wala kimako  
Ghalibu waringao, mbele hadharani, kwangu hawako  
Hawamo moyoni, wenyе vituko, siwi nao

Hata na wezi nao, wenyе kutamani, kila mfuko  
Wanopatwa na mwao, usio kifani, na mishituko  
Wapiga dafurao, vibeti njiani, wapate shiko  
Hawamo moyoni, wenyе vituko, siwi nao

Siwi na walewao, ulevi na shani, wenyе udhiko  
Watu mithjili hao, wana kisirani, hawana mbeko  
Wanaleta kilio, kwao jitengeni, mwende mwendako  
Hawamo moyoni, wenyе vituko, siwi nao

Usiwe bambalio, jama mna mboni, mbone mbonako  
Mapana masikio, kunasa halani, wacha vituko  
Msiwe wapuzao, onyo na maoni, bila mashiko  
Hawamo moyoni, wenye vituko, siwi nao

Sikai kwenye kao, lake mjivuni, mwenye matuko  
Endaye kwa matao, kokote kundini, hawi kitako  
Kinadi vifaa, vya kwake nyumbani, bila shtuko  
Hawamo moyoni, wenye vituko, siwi nao

Watw wabaguo, kabila nchini, kwangu ni mwiko  
Ndiwo wachafuao, ya kwetu Amani, raha na cheko  
Na wote wabebao, kinyongo moyoni, siwi waliko  
Hawamo moyoni, wenye vituko, siwi nao

### KINYWA

Kinywa chako mwanadamu, ndilo langa la kauli  
Na kauli ina sumu, ikitoka kwa fidhuli  
Watw wakakushutumu, kwa maneno ya ukali  
Kinywa uponza muili, kwa tamko lenye sumu

Ni kinywa hutakadamu, maudhi kuyasabili  
Kwa rai za kuhujumu, zinazozusha kitali  
Wendo wakakulaumu, kwamba wewe ni jahili  
Kinywa uponza muili, kwa tamko lenye sumu

Kinywa kibi ni haramu, ni heri tia kufuli  
Huchemsha watu damu, maneno ya pilipili  
Si mazuri si matamu, nakwambia ya ukweli  
Kinywa uponza muili, kwa tamko lenye sumu

Wengi watakuheshimu, benati na marijali  
Ukijua kukalimu, kinywa chako kulahali  
Wakwite mtaalamu, muungwana kwelikweli  
Kinywa uponza muili, kwa tamko lenye sumu

Japo wewe ni hakimu, bali ndumilakuwili  
Hupewi njema isimu, sifa zako ni dhalili  
Wengi watakujugumu, waseme huna fadhili  
Kinywa huponza muili, kwa tamko lenye sumu

Kinywa chenye tabasamu, hakiwi dufu ni ghali  
Hutumiwa kwa nidhamu, kwa maneno maadili  
Muradi kujikirimu, kwa watu na serikali  
Kinywa huponza muili, kwa tamko lenye sumu

Kauli ikiwa tamu, huvusha kufika mbali  
Sasa kwako kujihimu, sitamke yenye feli  
Utakuja kuhusumu, bura huo wako mwili  
Kinywa huponza muili, kwa tamko lenye sumu

**MWANADAMU SI MTU**  
Leo nitakuzindua, pulikiza kwa makini  
Ungakaa ukatua, uyatie akilini  
Mwanadamu twamjua, mtu ni kiumbe gani?  
Wanadamu sio watu, wenye utu ndio watu

Mwanadamu kung'amua, si muhali asilahi  
Mambo yake si murua, ana kingi kisirani  
Ni wengi nimegundua, tu mumo humo kundini  
Wanadamu sio watu, wenye utu ndio watu

Mwanadamu huonea, mchuje haan hisani  
Huwa tayari kuua, hana hisia za ndani  
kwani huyo kapotea, mwenye UTU si haini  
Wanadamu sio watu, wenye utu ndio watu

Mwenye utu narudia, ndiye mtu kwa yakini  
Asiyeleta udhia, kila mja huthamini  
Moyo wake maridhia, hana chuki abadani  
Wanadamu sio watu, wenye utu ndio watu

Aso utu nawambia, yuko sawa hayawani  
KWA Adamu kutokea, sisi sote twaamini  
Na utu kujipatia, ni dhima yetu duniani  
Wanadamu sio watu, wenye utu ndio watu

Muwe watu kwa tabia, wenye nyoyo za Imani  
Njia njema kupitia, pasizuke nuksani  
Hayo ninawaachia, neno UTU mujuweni  
Wanadamu sio watu, wenye utu ndio watu

HATA NAWE!  
Wakosapo sharafa  
Wanapata maafa  
Waovu wanakufa  
Hawajapata tija  
Hata na wewe pia!

Waroho nawaasa  
Kilindi mwajitosa  
Kwa upwamu wa pesa  
Hawajapata tija  
Hata na wewe pia!

Dunia imejaza  
Mazuri na mayaza  
Maovi hupendeza  
Hawajapata tija  
Hata na wewe pia!

Tumeona walafi  
Wezi na wakorofi  
Waso na nia safi  
Hawajapata tija  
Hata na wewe pia!

Majambazi hutwazwa  
Kila adha hujazwa  
Na mbaroni hulazwa  
Hawajapata tija  
Hata na wewe pia!

Ndugu hebu sikia  
Sudiyo shikilia  
Mui huangamia  
Hawajapata tija  
Hata na wewe pia!

## MASWALI YA TANIBIHI

### TENDA HAKI

- 1) Orodhesha kutoka mambo yanayowaghaflisha watu wakakosa kutenda haki.
- 2) Licha ya uovu wa mwanadamu, malenga anakuhimiza utende haki. kwa nini?
- 3) Taja nasaha na maonyo anayokupa msanii katika ubeti wa 2,3 na 4.
- 4) Taja sifa za wanyama hawa na kwa nini wametumiwa? (i). Nungunungu (ii). Kulungu.
- 5) Chambua: umbo, vina, mizani, msamiati na maudhui katika shairi hili.

### ULIMI

- 1) “Ulimi huponza na kutuza”. Eleza ukweli wa kauli hii kwa kutumia dokezi kutoka kwénye shairi.
- 2) Jahili vifungu vifuatavyo:
  - (i). Ni muhimu Zaidi kuwaza kabla ya kulitamaka neno kadamnazi.
  - (ii). Ni bora kunyamaza kuliko kutoa neno la kuudhi hadarani.
  - (iii). Majuto ya mtu huletwa nay eye mwenyewe anapotumia ulimi wake vibaya.
  - (iv). Ulimi ni adui mkubwa na pia ni rafiki halisi

### KESHO WEWE

- 1) Kwa nini ni viaya kumcheka mwenzako anapopatwa na tabu?
- 2) Ni watu gani wenye tabia ya kuwacheka wenzako wakati wa matatizo?  
Thabitisha.
- 3) Je watu wa jamii yako huchukua hatua gani pindi jirani akifikwa na maafa?

- 4) Ubeti wan ne unatoa tahadhari gani?
- 5) Jifunze maneno yote mapya yaliyotumilka katika shairi hill.

#### ASASI

- 1) Taja maafa yanayoweza kuletwa na kutoanza jambo kwa misingi bora.
- 2) Ni “Utenzi” wa nini anaouzungumzia mtunzi katika ubeti wa 4?
- 3) Utaitaje mwundo wa shairi hili?
- 4) Shairi hill lina maana gain kwa jumla?

#### KIBURI

- 1) Tumia Lugha ya mjazo kuelezea ujumbe unaowasilishwa na kila ubeti.
- 2) Eleza vipi mwenye kiburi hawesi kutapana na mwungwana.
- 3) Nini maana ya “uraufu na kiburi, swa maji na mafuta”? (Ubeti wa 3). Taja tashbihi nyingine iliyotumika kumithilisha kiburi na ungwana (ubeti 3).\
- 4) Taja methali yoyote yenye neno ‘kiburi’. Eleza maana na matumizi yake.

#### SIMTUKANE MAMBA

- 1) Fafanua wazi kijembe cha shairi hili.
- 2) ‘Mto’ na ‘Mamba’ ni jazanda mbili katika shairi hill. Eleza jazanda hizo.
- 3) Shairi hill linaweza kutumiwa vipi lwa maisha ya mwanafunzi ambaye angali yu shuleniianasoma?
- 4) Taja wazo kuu katika shairi hii.
- 5) Eleza fani za lugha zilizotumika katika tahajia ya maneno haya:  
(i) Mato (ii). Ng’ambu (iii). Mayuto (iv) ungawanacho (v) nikuelezato (vi) wende

#### NIDHANU SHULENI

- 1) Kwa nini mtunzi anasema elimu pekee haikamilishi utu wa binadamu?
- 2) Taja hasara zinazomkabili mwanafunzi asiyé na adabu shulenii.
- 3) Taha jinsi ukosefu wa adabu unavyoweza kumzuia mwanafunzi mwerevu darasani kuendelea na masoma yake.
- 4) Je nani alaumiwe kutokana na kuzorota kwa adabu za wanafunzi shulenii? Eleza.
- 5) Fanyeni mdahalo kutafuta ukweli juu ya vidondoo hivi:
  - i. Adabu za watoto zimezorota kutokana na wazazi kulegeza sera za malezi.
  - ii. Walimu wapatiwa uwezo kamili na kinidhamu watumie kurekebisha tabia za watoto shulenii.
  - iii. Kuiga tabia za kigeni kumeathiri Zaidi tabia za watu wan chi yetu.

#### SIWANIE UKUU

- 1) (a). Shairi hili ni tarbia. fafanua kwa nini liitwe tarbia

- (b). nakii vina vya ubeti wa kwanza.  
(c). Kimalizio kina mizani mingapi?
- 2) Taja onyo linalotolewa kwa mti mwenye pupa za kuwania ukuu (ubeti wa 3)
  - 3) Taja methai tano zinazowania na shairi hili katika maana.
  - 4) Eleza kini cha: (i). molto wa ubert wa ubter wa tatu. (ii). mlewa wa uberti wa kwanza.  
(iii) ukwapi wa mwanzo, ubert wa pili (iv) utao wa molyo wa ubert wan ne.

### PAMBANO

- 1) Taja mfano unaoletewa na sjairi hili.
- 2) Pambano lipi analolizungumzi msemaji?
- 3) Ubeti wa pili unakupa mfano wa methali gani kuhusu pambano?
- 4) Fafanua kiini cha mkarara kwa kutoa mifano ya ‘Mwanafunzi aingiaye darasabu bila zana za masomo ‘au’ anayefanya mtihani bila kujiandaa kikamilifu’
- 5) (a). Je kuna pambano lolote maishaini lisilohitaji silaha? Eleza.  
(b). Konokono ametumiwa kwa azma gani kwenye ubeti wa sita?  
(c). Taja maneno mengine yenye maana sawa na pambano kutoka shairi hili.

### WASHAIRI HUPENDANA

- 1) Nakili wagomvi wa shairi hili. Unafikiri ni yupi aliyemchokoza mwenzake? Tosheleza jibu lako.
- 2) Taja umuhimu wa hao WANGOZI waliotajwa katika ubeti wa tatu kufungamana na historia ya Kiswahili.
- 3) Taja dhima ya washairi katika nchi yako. Je wanasaidia vipi katika maendeleo ya nchi?

### UNAFIKI

- 1) Eleza jozi ya maana (maana mbili) ya kila neno:  
(a). Pima (b). Sheba (c). Nyuma (d) jaza (e). tama
- 2) Ni ubeti upi katika shairi hili unalobeba uzito wa dhamira ya mtunzi? Eleza.
- 3) Chambua lugha ya shairi hili kwa undani.

### MKATAA PEMA

- 1) Taja kilichomkera na kumkereketa moyo mtunzi hata akaamua kutunga shairi hili.
- 2) Andika mafunzo yote tunayopata tutokana na shairi hili.
- 3) Eleza ufundi uliotumika kulitunga shairi hili.

### KIJUNGU JIKO

- 1) Eleza asili ya kilio kilicho katika shairi hili.
- 2) Simulia kwa kifupi hali ya maisha ya mjini na ya vijini.
- 3) Fafanua kiina cha kituo
- 4) Nini msimamo wa msemaji? Eleza manoi yake kwa maneno yako mwenyewe.

- 5) Tunga insha juu ya ‘masiha ya shambani no bora kuliko ya mjini’ au ‘aito wa turudi mashambani uimarishwe’

### SIWI NAO

- 1) Msemaji hawi na watu gani? Na kwa nini anawachukia?
- 2) Taja usanii wa shairi hili kwa upande wa mpangilio wa umbo, beti, mizani, vina na mishororo.
- 3) (a). Shairi hili ni la bahari gani?
- 4) (b). Eleza tofauti baina ya tungo zifuatazo:  
ukawafi, msuko, kikwamba na pindu.

### KINYWA

- 1) Eleza mawaidha ya shairi hili kwa maneno yako.
- 2) Taja shina la kila neno lilonyambuliwa kwa mujibu wa utunzi:  
Kwa mfano: shina la WAKAKUSHUTUMU ni SHUTUMA. Sasa endelea kuhujumu, zinazonusha, wakakulaumu, huchemsha, kukalimu, kujiirimu, huvusha, kujihimu, sitamke, kuhusumu.

### MWANADAMU SI MTU

- 1) Ni ipi tofauti kati ya mwandamu na mtu? Taja sifa za kila mmoja.
- 2) Shairi hili linatufunza nini?
- 3) ‘Ubora wa mtu ni tabia njema na utu wake’. Fafanua kikamilifu.
- 4) Je, wewe ni binadamu au ni mtu? Jichambue ujitalambue.
- 5) Nini kinyumw cha ‘UBINADAMU’? Eleza sababu halisi.

### HATA NAWE

- 1) Kwa nini shairi hili limpewa jina la HATA WEWE? Eleza kinaganga.
- 2) Hili ni shairi la aina gani?
- 3) Andika kiini cha kila kifungu cha ubeti.
- 4) Mshairi aokeza ni kwa nini watu hawapati tija?
- 5) Umejifunza nini kutokana na shairi hili?

### MASWALI YA ZIADA

- 1) Taja asili ya mashiri ya Kiswahili kisha eleza tofauti kati ya: Mashairi ya Kiswahili na mashiri kwa Kiswahili.
- 2) Taja nguzo mbili kuu za FASIHI. Eleza fani za kila nguzo.
- 3) Eleza jinsi vyombo vifuatavyo vinavyotoa mchango katika kukuza, kutukuza na kueneza Kiswahili.

- (a). redio na televisheni (b). magazeti na majarida (c). vitabu (d) warisha na kongamao  
(e). shule na vuyo (f) wizara (toa mifano) (g) matibaa.
- 4) Utamhakishia vipi mtu aliyepotoshwa anayadhanaia ati chimbuko la lugha ya kisawhili ni mchanganyiko wa kiarabu na kibantu kuwa asili ya Kiswahili papa hapa petu Afriak mashariki wala haikuzaliwa na lugha yoyote ya kigeni kutoka nje?
- 5) Watu wasiokimudu Kiswahili ndio wanaokipinga na kukidhara Kiswahili jadili.
- 6) Eleza maana za vipengele hivi vya taaluma ya ushairi.  
ubeti, ukwapi, kipande, mwandamizi, utao, kekto, vina, utoshelezi
- 7) Eleza tofauti kati ya (a) Utamaduni wa taifa na utamaduni wa jamii (b) Lugha ya taifa na lugha ya kienyeji.

### ZINGUKO NA KUTANABAHISHA

*Katika huku kuishi*

*Maisha siyo aushi*

*Tunupita kama moshi*

*Shika huu uzindushi*

*Dunia cheko na hamaki*

### UTALEMA

Mbona unanyamaza, na una jambo baya?

Dhahiri latokeza, na hutaki zuiya!

Talemewa ujute.

Dogo huzaa kubwa, kweli nakwelezeya

Onapo umekabwa, haraka jitete

Talemewa ujute.

Mengi hutufikia, twabaki kutataya

Kisa nimegundua, yajapo twangaliya

Talemewa ujute.

Bora kufanya hima, kinga kukimbiliya

Tabu haijalema, msada jipatiya

Zuia usijute.

### KIZAZI CHA FEDHEHA

Muole nyuki, mwenye asali  
Hasogeleki, vile mkali  
Anomiliki, ni yake mali  
Anakubali, angafariki  
Mnaumbuka hamuumbiki  
Hana mkuki, nyuki dhalili  
Na husadiki, yake amali  
Kupata dhiki, kwake halali  
Ila asali, yake hufiki  
Mnaumbuka hamuumbiki

Kwa kweli nyuki, ana akili  
Nyuma habaki, kuhami hali  
Mtu hafiki, kwake muhali  
Mwenye akili, fanya ja nyuki  
Mnaumbuka hamuumbiki

Ni unafiki, kwa mwanamwali  
Njia hashiki, hawi mkali  
Mfano nyuki, utu hajali  
Hajisaili, njema tariki  
Mnaumbuka hamuumbiki

Kubwa hilaki, mwali kubali  
Kuwa rafiki, aso halali  
Na kudiriki, kulala chali  
Kama anzali, eti ashiki!  
Mnaumbuka hamuumbiki

Mnashiriki, mengi laili  
Hamkanyiki, wala kujali  
Soni na dhiki, kutozijali  
Utu na hali, za mahuluki  
Mnaumbuka hamuumbiki

Sio riziki, yenu amali  
Bali fasiki, utu kudhili  
Na si laiki, kwa mwe akila  
Kuyakubali, na kushiriki  
Mnaumbuka hamuumbiki

Igeni nyuki, msikubali  
Kuwaafiki, wala asali  
Msije baki, hman hali  
Na idhilali, si stahiki  
Mnaumbuka hamuumbiki

Semeni haki, bila batili  
Kizazi hiki, msiojali  
Je hamtaki, zetu kauli?  
Mtupwe mbali, mjimiliki?  
Mnaumbuka hamuumbiki

**UFUKARA NI WA AKILI**  
Leolewelo oleni, mzame na kufikiri  
Mffikiri kwa makini, kuhusu huyu fakiri  
Msomjua juweni, kinyumeche ni tajiri  
Ufukara wa akili

Akili zikipungua, basi mtu ni fakiri  
Husemwa ameugua, atwawe kwa dakitari  
Hawezi kupangua, na kuyapanga mazuri  
Fukara aso akili

Amba umempa kazi, asonazo tafakuri  
Atafanya banangizi, asifate dasturi  
Na pangine hamalizi, na haikosi dosari  
Ufakiri kwa akili

Aso akili fukara, angakuwa yu tajiri  
Akili ni yetu dira, muongozo wa safari  
Maelekezo huchora, kujua baya na zuri  
Utule ni wa akili

Muole muenda shule, kusoma kunapojiri

Ungapiga makelele, unenayo hafikiri  
Kazubaa kama kole, hajui bali na bari  
Unobe ni wa akili

Tangu enzi za Muyaka, na wahenga mashuhuri  
Wakongwe walotukuka, msemo waliamiri  
Akili mali hakika, alo nazo si fakiri  
Umasikini akili

Enenda ukichunguza, taratibu kwa saburi  
Wenye mali walojaza, si karadha si sihiri  
Akili iliongoza, wakapata kunawiri  
Fakiri aso akili

Kisha rudi nyuma nuyma, kwa watule wa fikiri  
Waliopata neema, ya kujaaza dinari  
Akili zilipohama, na pato likahajiri  
Ulofa ni wa akili

Kutana na punguani, hawezi kujisatiri  
Yu mithili hayawani, jina lake ni fakiri  
Wenye akili oneni, na walivyo mabepari  
Huleta mali akili

#### MAJUTO

Kingurumishwapo chondo, wateja hurandaranda  
Husomewa kandokando, wakaanza kujiwinda  
Wanajua pana ngodo, ngondo kubwa ya kutenda  
Mtenda akishatenda, majuto hufata tendo

Wakisikia mdundo, mdundo wa kirindanda  
Kirindanda cha msondo, sondo kubwa na kinanda  
Hupigana nguo fundo, chapuchapu wakaenda  
Mtenda akishatenda, majuto hufata tendo

Huja mwisho wa kitendo, juto roho limetanda  
Ukafikiri uhondo, waenda kupata tunda  
Vina hasara vishindo, mwenye woga hujilinda

Mtenda akishatenda, majuto hufata tendo

Lau lingekuwa pendo, bora ungalijilinda  
Usiandame mkondo, utapata vy a kuvunda  
Ungawaza wako mwendo, dunia ni njia panda  
Mtenda akishatenda, majuto hufata tendo

Sijiweke roho fundo, vy a wenzako kuvipenda  
Ukaondoka na nyundo, na panga kwenda kumwinda  
Meona wapi mtindo, kuvuna pasi kupanda  
Mtenda akishatenda, majuto hufata tendo

Huwaje mwenye mirando, asiyejua kuunda  
Mtegemea magendo, apawe mali kulinda  
Moyo humuenda shindo, mali kuitia vyanda  
Mtenda akishatenda, majuto hufata tendo

Kaditamati manondo, wenyе roho za kudunda  
Wasiojua upendo, kwa wepesi wa kutenda  
Papara huzua kondo, na mwisho muume vyanda  
Mtenda akishatenda, majuto hufata tendo

**HERI WASICHANA WADOGO**  
Una tijara, udogo, kwenu wasichana  
Kubwa sitara, udogo, tena uungwana  
Ni utu bora, udogo, na mwendo mwanana  
Peke walio bora, wasichana wadogo

Kwenye hadhara, mdo go, shabini manna  
Hawezi kera, mdo go, lau'kutukana  
Adabu bora, mdo go, madharau hana  
Hao walio bora, wasichana wadogo

Zake fikira, ni ndogo, nyendoze si pana  
Kwake dharura, ni ndogo, na tamaa hana  
Tena hasira, ni ndogo, hawezi pigana

Wale walio bora, wasichana wadogo

Habebi sura, mdogo, apate nag'ana  
Hana dhukura, mdogo, ati wamuona  
Hutia fora, mdogo, kwa kutulizana  
Kweli walio bora, wasichana wadogo

Ukubwa dhara, mikogo, pia kupigana  
Tele papara, mikogo, na kusengenyana  
Bongo imara, mikogo, subira hakuna  
Hasa walio bora, wasichana wadogo

#### PATA ELIMU

Haina tama elimu, marefu na mapanaye  
Haikinai utamu, yuko wapi akanaye?  
Maishani ni hatamu, iongozayo badaye  
Anayebeza elimu,achezea maishaye

Mwana hebu ujihimu, usingojee nyumaye  
Nenda shule ufahamu, ya dunia na mamboye  
Naw uwe taalimu, hadhi bora jipatiye  
Anayebeza elimu,achezea maishaye

Maish sasa magumu, hatawe uangaliye  
Yapime kwenye fahamu, upate juu dhikiye  
Soma ili ujikimu, shule usiikimbiye  
Anayebeza elimu,achezea maishaye

Elimu zana adhimu, soma usitayetaye  
Ni wakati wa hukumu, huu siyo baadaye  
Kisomo kwako muhimu, kukikosa kijutiye  
Anayebeza elimu,achezea maishaye

Ola wale mahakimu, nyayo zao ufatiye  
Wanapata darahimu, hawajali ghamamaye  
Elimu ni mlizamu, ni ya aushi majiye

Anayebeza elimu,achezea maishaye

Nyuma utajilaumu, na tena uje ugwaye  
Wakubeze wanadamu, ucheke ama uliye  
Uifuate dawamu, elimu leo kwa seraye  
Anayebeza elimu,achezea maishaye

#### MWANADAMU ALITOKA WAPI?

Kuna ngano kemukemu, za kubuni na za kweli  
Nyinginezo ni vigumu, kuamini bilikuli  
Hata hao watalamu, hawatowi tafsili  
Mwenye akila timamu, awazie jambo hili  
Apekue mwanadamu, alivyo yake asili  
Asili yake ni nini, Uumba au tumbili?

Moyo wanienda kasi, hunikanganga akili  
Kila nikiwadadisi, watalamu wa azali  
Wanipe jibu jepesi, kuhusu wetu usuli  
Sijampata farisi, anayemanya kamili  
Hata wale wa sayansi, wapimao majabali  
Lipi jibu maalumu, Buruhani na tumbili?

Nikisoma Bibilia, vitabu vyote viwili  
Cha ukale kuanzia, kisha hicho cha Injili  
Kurani haingilia, aya zake kutaali  
Vyote vinasimulia, tumeumbwa na Jalali  
Kwa heshima asilia, pamoja sura jamili  
Sasa jibu liko wapi, Huluki au tumbili?

Ukisoma vitabuni, maandiko ya awali  
Vyenye mambo ya zamani, ya wakale na tawili  
Utakuta ubaini, wa maneno ya batili  
Kwamba mtu ndiye nyani, umbo alijibadili  
Akawa sura thamini, uonavyo ana hali  
Mwabali asili yetu, hutokana na tumbili?

Abadani siwabezi, mimi sina ujahili  
Wala mie siwapuzi, ninatafuta ukweli  
Mumesoma mu wajuzi, Misahafu na Injili  
Nataka jibu azizi, moja tosha nikubali  
Msiiitwe watambuzi, kumbe udumakuwili  
Mwajuwa tulikotoka? Kwa mungu au tumbili?

Madai yamedaika, meni yasiyo mithali  
'Dunia ilimegeka, toka kwenye juu kali  
Ndipo ikazizimika, sokwe wakatatawakali  
Hatima wakageuka, binadamu wenyewe hali'  
Hapo ndipo ninamaka, mbona leo sibadili?  
Semeni tulikotoka, kwa Mungu au tumbili?

Ningaomba nitambue, Adamu yule rijali  
Pamoja naye Bibie, Hawa Mama wa awali  
Ni wanasonwe njue, ama kazi ya Jalali?  
La urongo tutangue, liwe mbali na ukweli  
Hakika tusimamie, tusifate njia mbili  
Mwanadamu wakubali, kuwa were ni TUMBILI?

#### SUMU YA MAISHA

Naanzilisha nudhumu, kutangaza ya moyoni  
Utafiti nimetimu, ukweli nikabaini  
Dinia duni ni sumu, huwakebehi hiwani  
Kiumbe nimetambua, yapasayo kufahamu

Maisha huwa matamu, ukiishi kwa Amani  
Uwaonyeshe kaumu, unazo bongo kitwani  
Pia kiasi elimu, japo haba ya utani  
Kuzaliwa baradhuli, maishani huwa sumu

Dunia kazi muhimu, bila kazi hali duni  
Viungo view timamu, upige vita kazini

Upate kula utamu, ujenge siha mwilini  
Ukizaliwa mzembe, maishani huwa sumu

Umekuwa ni ghulamu, au mwari wa nyumbani  
Wazazi wakajijimu, ukasoma mashulenii  
Naw uwe huna hamu, kwenda shule huthamini  
Kutosoma ya shuleni, maishani huwa sumu

Dunia yetu ni ngumu, hutoishi furahani  
Watu watakushutumu, na hawatakuamini  
Uwe bila kujikimu, huwezi pata auni  
Kutegemea wengine, maishani huwa sumu

Wewe mwana wa Adamu, si mnyama wa porini  
Saba inakulazimu, kujihoji akilini  
Usijifanye wazimu, una dhiki tafanyani?  
Kutotumia akili, maishani huwa sumu

Umekuwa wa makamu, kijana bora machoni  
Maisha mambo muhimu, ni matatu duniani  
Kuoa kwakulazimu, na kuolewa kanuni  
Kuishi bila ya ndoa, maishani huwa sumu

Usipende vya haramu, na vya watu sitamani  
Mwenye akili timamu, hawezi shikwa ugoni  
Huwa mtu wa nicdhamu, kwa mke wake nyumbani  
Kutaka mke wa mtu, maishani huwa sumu

Mja ninakuhukumu, kwa zinduo lenye shani  
Fuata utunze damu, isikutoke puanii  
Ujitanibu dawamu, kudokoa mifukoni  
Kuiba mali za watu, maishani huwa sumu

Dunia yetu hudumu, binadamu mapitoni  
Jitengee va sehemu, ule sasa na jioni  
Kisha uombe Rahimu, akupe fungu usoni  
Kutokuweka akiba, maishani huwa sumu

### KUMBE

Majuto huja kinyume, watu wakajijutia  
Ungakaa na upime, mambo bila kupapia  
Majuto huja kinyume!  
Sijigambe nyamaume, kupita ukitishia

Pande zote utizame, ndipo mbele kutembea  
Usione una sime, msitu kuelemea  
Majuto huja kinyume!  
Kuna simba na madume, wawezao kuvamia

Sijifanye wewe mume, hata mume hypotea  
Penye tu usimame, na akili kutumia  
Majuto huja kinyume!  
Mtu siye pakashume, vijinyama kurukia

Jimakini utuame, na kumbe kuliambaa  
Piga mbizi na uzame, pindi juu hujapaa  
Majuto huja kinyume!  
Usilime penye kame, masika yatafatia

Tua mambo uyapime, yapo mengi ya dunia  
Chunga vyanda usiume, mambo yakikuzidia  
Majuto huja kinyume!  
Kumbe wewe gumegume, siyo papap ni dagaa!

### MATENDO MEMA YA WEMA

Sibali kughilibiwa, kwa moto kuzaa jivu  
Au ngomba kutowa, ndizi zake zilo mbivu  
Lakini sijakolewa, chema kuzaa kiovu  
Matendo mema ya wema, maovu ni ya waovu

Tendo hufana asili, kama nyoka na mwanawewe  
Asokuwa na fadhili, lipi jema alitowe?

Ila kero na fidhuli, jinginelo asijuwe  
Matendo mema ya wema, maovu ni ya waovu

Mie ninavyoamini, na vile nilivyoona  
Binadamu mhisani, matendo yake bayana  
Hutoka kwake rohoni, kwenye dhati kiungwana  
Matendo mema ya wema, maovu ni ya waovu

Hata kama ugasoma, kumbukumbu za zamani  
Juu yao watu wema, kabisa utabaini  
Mambo yao ya hikima, matendo ya kihisani  
Matendo mema ya wema, maovu ni ya waovu

Muovu atende nini, cha kuliwaza nafusi  
Damu yake huwa duni, ya vitendo vy a maasi  
Asilani hana soni, hachelei na matusi  
Matendo mema ya wema, maovu ni ya waovu

### SIVYO

Msema Kiingereaza, mwadhani kasoma sana!  
Mmepotea mchana, juu juu laangaza  
Mna macho ya kuona, lakini mwaona giza  
Na giza likishikana, vipi tajielekeza?

Msema kiingereza, mwadhani kasoma sana!  
Kipimo chenu ni dhana, na ambayo hypoteza  
Lugha hiyo siyo shina, ya elimu kuijaza  
Bali ni moja ya zana, za elimu kueneza

Msema kiingereza, mwadhani kasoma sana!  
Hata pengine hapana, moyo unanikataza  
Lugha niyo kuineni, ni sawa na kuigiza  
Mchunguze kwa mapana, mneni hwenda ni boza

Msema kiingereza, mwadhani kasoma sana!  
Hiyo lugha imechina, zama za kujiangoza  
Japo twaitaka sana, maarifa kuongeza

Ila si kama dafina, teule ya kutukuza

Msema kiingereza, mwadhani kasoma sana!  
Najua wengi mwaguna, rai yangu kuibeza  
Na hata kunitukana, kupinga ninavyowaza  
Bali mim chuki sina, nasema nilixhunguza

Msema kiingereza, mwadhani kasoma sana!  
Nimesoma waungwana, pamoja kiingereza  
Ingawa si kulingana, Kiswahili chaongoza  
Nami bila kukinena, watu wanani puuza

Msema kiingereza, mwadhani kasoma sana!  
Kiswahili ni sana, vibarak hunibenza  
Husema sina mwamana, hadhi yangu hupunguza  
Hakuna ninachovuna, mbali na kunichukiza

Msema kiingereza, mwadhani kasoma sana!  
Siachi lugha ya nina, kwa ndimi za kuigiza  
Elimu na uungwana, huvipata mchunguza  
Navyo vinapatikana, kila lugha noweza

### KAMA SISI

Hatuambi mwatukera, na tena mwatughasi  
Hivi twaona ibura, ndaro zenu za kasi  
Kujighani pa hadhara, kuwa nyie wagosi  
Mwatangaza m wabora, mnani hatunasi!

Mwatuona mafukara, nyinyi ndio wakwasi  
Mwola yetu matambara, hamchuji utosi  
Kumbuka mtu ubora, umo kwenye nafusi  
Mwatangaza m wabora, mnani hatunasi!

Muumba ndiye sonara, alofua wanasi  
Kwa akili na busara, tupu bila lebasi  
Lau kama mwajipara, nguo siyo nemsi

Mwatangaza m wabora, mnani hatunasi!

Hatuzwi simba marara, sababu ya utesi  
Kuwaua kina swara, wasojua kisasi  
Kuwa ana makadara, kwetu huo uasi  
Mwatangaza m wabora, mnani hatunasi!

Ilimu haba kudara, mlopata kiasi  
Isiwafanye kubera, mlifikotoka nasi  
Msidhani mumegura, toka gamba jeusi  
Mwatangaza m wabora, mnani hatunasi!

Hifadhi yetu imara, kuhimidi Kudusi  
Aliye mwenye sitara, mavani mahususi  
Dunia si pa kufura, sisi sote mapisi  
Mwatangaza m wabora, mnani hatunasi!

#### UJANA NI KAMA MOSHI

Umbo kazi ya wadudi, na sio wako utashi  
Ungavva maridadi, lebasi njema ya shashi  
Kukongoka huna budi, hata upake marashi  
Ujana ni kama moshi, ukienda haurudi

Sianze kutaradadi, uzee ukakughushi  
Ukapandwa na madadi, ukose ukaramshi  
Lisilo budi hubidi, kabisa hubadilishi  
Ujana ni kama moshi, ukienda haurudi

Ujana kama mikadi, raha yake haichoshi  
Huifariji fuadi, kwa maisha ya fatashi  
Lakini kama midadi, hufutika maandishi  
Ujana ni kama moshi, ukienda haurudi

Tokea kale na jadi, maisha siyo aushi  
Umri unavyozidi, uzee ndio mdoshi  
Uzee ukishitadi, hukaribisha mazishi

Ujana ni kama moshi, ukienda haurudi

Sighasi yako fuadi, kwa kutamani usihi  
Miaka iso idadi, sura yako haichushi  
Hujapata hiyo sudi, ujana wako ni moshi  
Ujana ni kama moshi, ukienda haurudi

Hakuna mtu hadid, katika huku kuishi  
Alo na sura jadidi, isokuwa na tashwishi  
Utauacha baidi, kwa chozi ama ucheshi  
Ujana ni kama moshi, ukienda haurudi

Naeleza makusudi, kuleta hili tamshi  
Wengi wanataradadi, na kupata tetemeshi  
Uzee unapowadi, kwao hauwaridhishi  
Ujana ni kama moshi, ukienda haurudi

Macho yangu ni shahidi, siyaneni ya uzushi  
Kuna hao shugadadi, wanaojitia nakshi  
Eti ujana urudi, wazifanye purukushi  
Ujana ni kama moshi, ukienda haurudi

Ujana sio muradi, au mbinu za kusihu  
Maisha ni maujudi, na Mola ndiye Mlishi  
Ni bora kutabaradi, hadi kwake kwenye arshi  
Ujana ni kama moshi, ukienda haurudi

### YETU MACHO

Husemwa ni dunia, imegeuka, kisa hicho  
Mambo yamezukia, na kwa haraka, kochokocho  
Sisi huangalia, na tukamaka, yetu macho!  
Tu wazee ni balaa

Babu waliusia, wakatoweka, kwa maficho  
Kwamba yakitujia, yenyenye mizuka, fanya kicho  
Kwetu huangalia, na tukamaka, yetu macho!

Elimu kutokea, ina Baraka, kuwa macho  
Ndani man belua, hughafilika, walo nacho  
Sasa huangalia, na tukamaka, yetu macho!  
Kwa wazee ni balaa  
Vijana hupania, huyakiuka, mawazo kocho  
Ambayo ni wasia, wangalishika, wapone gocho  
Haya hungalia, na tukamaka, yetu macho!  
Wana hawa ni balaa

### KILIO CHETU

Kila uchao twalia, matatizi yakithiri  
Twalia twanyong'onyea, kwa machozi furifuri  
Palepale twabakia, bila shwari wala kheri  
Chozi letu lafaani, hatupati manufaa!

Njaa imetvuamia, sote tunazo habari  
Matumbo yanaumia, hayashibishwi vizuri  
Kilio tunaangua, kusubu hii hatari  
Chozi letu lafaani, hatupati manufaa!

Mvua imepungua, ni haba hizi dahari  
Mashamba tukilimia, mimea hainawiri  
Nguvu zimetupungua hasa swiswi mafakiri  
Chozi letu lafaani, hatupati manufaa!

Gharama zimezidia, naswi hatuna dinari  
Hatuwezi kununua, mahindi wala sukari  
Vipi tutaendelea, yatazameni mandhari  
Chozi letu lafaani, hatupati manufaa!

Wapi tunaelekea, ingafaa tufikiri  
Tayari tunaumia, mapema si alasiri  
Ne kesho ikiwadia, ni yepi yatayojiri!  
Chozi letu lafaani, hatupati manufaa!

Leo ati tunalia, sana bila kukadiri  
Na wajao mwadhania, vije watajinusuri?  
Ama mtaniambia, mbele yetu kuna heri?

Chozi letu lafaani, hatupati manufaa!

**MWEMA HAJAZALIWA?**

Wa kuifidi dunia, asilani hajazawa  
Atakayetujia, asema na kusikiwa  
Kwa sababu twasikia, hatutaki kuelewa  
Mtu mwema hajazawa, alo kufu ya dunia?

Mola alitutumia, Yesu mwema wa mtawa  
Ili kututumikia, na madhambi kututowa  
Watu walimchukia, hatima akauawa  
Kwa hakika hajazawa, alo kufu ya dunia?

Mnaweza kunambia ni yupi alo muruwa  
Viongozi mwachagua, kwa hiari sawasawa  
Nyuma mnawapindua, na wengine huuawa  
Anofaa hajawa, alo kufu ya dunia?

Mke wajichagulia, kisha mkafunga ndowa  
Mume unamridhia, bila tabu akuowa  
Punde fujo zatokea, hata mwaka haujawa  
Ni sababu hajazawa, alo kufu ya dunia?

Binadamu anofaa, ni kweli hajazaliwa?  
Mohamadi ni Nabia, salihina tulopawa  
Nduli walimuendea, bali alijiokowa  
Abadani hajazawa, alo kufu ya dunia?

Ni wapi atatokea, mwema wa kushangiriwa  
Aso doa wala toa, mswafi wa kubaliwa  
Wema tunaodhania, bilesi hukataliwa  
Nauliza hajazawa, alo kufu ya dunia?

**DUNIA TAMBARA BOVU**

Dunia tambara bovu, kuraruka si ajabu  
Mja wataka utuvu, kuna mengi masaibu

Jitafutie wokovu, uwe mtu mahabubu  
Kuraruka si ajabu, dunia tambara bovu

Dunia mti mkavu, huvunjika agahalabu  
Sidhanie u mwerevu, kunyenga kustahabu  
Kuwa mtu munagagvu, wakuenzi masahibu  
Kuraruka si ajabu, dunia tambara bovu

Dunia ina maovu, hadaa zenyе harabu  
Ukiwa u mpumbavu, nyuma utastajabu  
Bora ustahimilivu, ili upate thawabu  
Kuraruka si ajabu, dunia tambara bovu

Dunia siyo ya nguvu, isome kama kitabu  
Laha zake neemevu, hufunza na zinatibu  
Kuzisoma kivumvu, ziliwashinda mababu  
Kuraruka si ajabu, dunia tambara bovu

Dunia ni uwekevu, mamboyake taratibu  
Usivimbishe mashavu, timiza wako wajibu  
Si vema ukakamavu, na wenzio kughilibu  
Kuraruka si ajabu, dunia tambara bovu

Dunia walao mbivu, watafutao sababu  
Nao huwa wawekevu, wapacho huhisabu  
Thama ni wavumilivu, wapatwapo na taabu  
Kuraruka si ajabu, dunia tambara bovu

**MTENDA AKITENDEWA**  
Vije leo walalama, kwa yale ulotendewa  
Huyakumbuki ya nyuma, pindi ulipochachawa  
Ulipotenda unyama, uliona ndiyo sawa  
Mtenda akitendewa, hulalama kaonewa!

Ulizusha uhasama, leo wewe wapagawa  
Walia bila kukoma, tungadhani umefiwa  
Sasa huna usalama, huwezi kujiopowa  
Mtenda akitendewa, hulalama kaonewa!

Tenda mambo kwa kupima, usiruke huna mbawa  
Una macho kutazama, na akila umepewa  
Matendo hurui nyuma, atendaye hurudiwa  
Mtenda akitendewa, hulalama kaonewa!  
Dunia haishi njama, sijione umepowa  
Ukadhani u salam, binadamu kuwagawa  
Ukahisi ni wanyama, waso hali kama ngawa  
Mtenda akitendewa, hulalama kaonewa!

Unapotenda zahama, siku yako itakuwa  
Ambapo utaungama, useme umechachiwa  
Na uanze kutetema, ulie umeonewa  
Mtenda akitendewa, hulalama kaonewa!

#### NILIKOZAWA

Naipuiza buruji parapanda ama siwa  
Niwajuvye wasomaji janibu nilikozawa  
Watanabahi kijiji wilaya hata mkowa  
Natongowa nilikozawa

Wengi wananihitaji nitamke sawasawa  
Jina lacho kitongoji na wapate kuelewa  
Kama kweli sio mji wenye watu wa vipawa  
Ninaenzi nilikozawa

Tena huu utungaji vile unavyodhaniwa  
Sharuti uwe mwenyeji wa mwambao mzaliwa  
Ama uwe mkaaji na mwislamu mwelewa  
Nafichua nilikozawa

Pulikizani wambuji tafsili naitowa  
Mimi siye mwanajiji au wa Shimo la Tewa  
Natoka unako maji ya kando kando ya Ziwa  
Masikani nilikozawa

Kiswahili ni siraji sote tunamulikiwa  
Kwenye miji na vijiji toka Lamu hadi Ndhiwa  
Na mimi nilihitaji Zaidi kukielewa  
Ninanad nilikozawa

Huu wangu utungaji hidaya nimepawa  
Niweze kutabalaji Kiswahili kuinuwa  
Kutoka kule rufiji hadi bara kwenye ziwa  
Kwenye maji nilikozawa  
Nyakwere ndicho kijiji majaliwa ya uzawa  
Kadiang'a kitongojia na Nyanza ndio Mkowa  
Na huu wangu ugwiji ni mhanga kujiyowa  
Niinuwe nilikozawa

Mzee mbega siraji mkitaka kumjuwa  
Nimeishi naye mbuji gambera asokuliwa  
Akanipa udibaji wa usanifu muruwa  
Kudariji nilikozawa

Kwa vitabu msomaji ni bingwa wa kuchambuwa  
Navisoma kama jaji mtafiti wa daawa  
Nimeisha matungaji kunga nikazielewa  
Kufaidi nilikozawa

## MASWALI YA MARUDIO

### UTALEMEA

1. Shairi hili limetungwa katika bahair gani?
2. Wahenga walisema: Anayeficha ndwel kilio kitamficha”. Eleza jinsii methali hii inavyokwenda smabamba na maudhui ya shiri hili.
3. Eleza maana na matumizi ya methali hizi:
  - (b) Mdharau mwiba huota tende
  - (b) Usipoziba ufa utajenga ukuta
  - (c). Mficha uchi hazai
  - (d). Udongo uuwahi ungali maji.

### KIZAZI CHA FEDHEHA

1. Fafanua anawani ya shiri hili ‘KIZAZI CHA FEDHEHA’ kisha nukuu fedheha zinazotajwa katika shairi.
2. Jambo gani lililomkera mtuzi hata akaazimia kulitunga shairi hili?
3. Taja nasaha inayotolewa katika ubeti wa nne.
4. (a). Taja baadhi ya vitendo vya vijana wa siku hizi vinavyodhiihiri waxy kuwa hawachelei aibu.  
(b). Nyuki ametajwa katika shairi hili kwa azma gani?

### UFUKARA NI WA AKILI

1. Eleza ni kwa jinsi gani akila ni mali?
2. Msemaji anatoa mfano upi kuhusu mwana –s hule asiye na akili masomoni? Eleza ukifuatilizia lengo la shairi hili.
3. Muyaka ni nani? (ubeti wa 6). Ana numuhimu gani kwa waswahili?
4. Nakili maneno ya Kiswahili cha kale yalotumika kwenye shairi kisha eleza maana ya kila neno.

### MAJUTO

1. Tukitaka kuepukana na majuto ni lazima tufanye mbinu gani? Simulia kwa nini wati hupata majuto?
2. Methali ya ‘ majuto ni mjukuu huja kinyume’. ina mafunzo gani maishani mwetu?
3. Taja ujumbe wa ubeti wa sita.
4. Fafanua dhamira ya mkarara.
5. Jifunze msamiati wa shairi hili.

### HERI WASICHANA WADOGO

1. Taja ukubwa una madhara yapi kwa wasichana?
2. Eleza kwa nini wasichana wengine hurandaranda mitaani badala ya kutulia majumbani kwa wazazi wao? Pendekeza nija ya kukomesha tabia hiyo
3. Chambus Sanaa ya shairi hili.

### PATA ELIMU

1. Taja manufaa ya elimu kama yaliyvodokezwa katika shairi.
2. Taja elimu imefananishwa na nini katika shairi hili?
3. ‘Kisomo kwako muhimu, kukikosa kijutiye’ Fafanua.
4. Eleza tofauti kati ya:
  - (a). Hatamu na hitimu
  - (b). Adhimu na adamu
  - (c). beza na peza

### MWANDAMU ALITOKA WAPI?

1. Taja sababu kubwa inayomfanaya tunzi akanganywe na asili ya mwana damu.
2. Taja muundo wa utungo wa shairi hili.
3. Tunga shairi sanifu la tashlita au tasdisa beti tatu kulijibu shairi hili kwa maoni yako binafsi.

### JISAHIHISHE

1. Msemaji anahimiza masahihisho yapi katika jamii?
2. Kwa nini watu wengine hujiona bora kuliko wenzao?  
je unakubali kuwa binadamu wote ni sawa? thibitisha.

### SUMU YA MAISHA

1. Taja mambo yanayoweza kutatanisha maisha kwa mujibu wa shairi hili.
2. Ubei wa saba unatupa dokezi ya mambo matatu muhimu maishani. Yataje yote.

## KUMBE

1. Je shairi hili lina kiitikio? Taja
2. Baada ya kulisoma shairi hili na kuielewa, basi fafanua maana ya vifungu hivi:
  - i. piga mbizi na uzame
  - ii. sijigambe nyamaume
  - iii. chunga vyanda usiume
  - iv. kumbe wew gumegume, siyo papa ni dagaa

## MATENDO MEMA YA WEWA

1. Msemaji ana imani gani kuhusu matendo ya mtu?
2. Kumbukumbu za zamani zinasema nini juu ya watu wema?
3. Eleza kiini cha kipokeo cha shairi hili.
4. Dhihirisha dhamira ya mtunzi

## SIVYO

1. Msemaji anakana nini kaktika ‘Sivyo’? Je, unakubaliana naye? sema.
2. Kwa maoni yako binadsi, unadhani ni kwa nini mtu akisema kiingereza basi hudhaniwa amesoma sana?
3. Eleza kazi na umuhium wa lugha katika jamii kisha eleza tofauti na uhusiano wa lugfha na elimu.
4. Eleza kwa kirefu (a) umuhimu wa kujua lugha ya taif lako (b) Ubora wa kujua lugha za kigeni – hasa lugha za kimataifa.

## KAMA SISI

1. Shairi hili linawazungumzia watu wenye tabia gani? wamefanya nini?
2. Fafanua maana ya semi hizi:
  - i. kujighani pa hadhara
  - ii. hamchuji utosi
  - iii. endani kama ngisi
  - iv. muumba ndiyе sonara
  - v. sisi sote mapisi
  - vi. nakili maneno yenye vina katika ubeti wa sita

vii. taja mizani ya kituo

3. (a). Nakili maneno yenyе vina katika ubeti wa sita

(b). Taja mizani ya kituo

#### UJANA NI KAMA MOSHI

1. Taja madhara ya ujana na raha ya ujana kwa mujibu wa shairi.

2. Kwa nini mtu akishazeeka hulilia ujana wake urudi? toa maoni yako kuhusu ‘kipindi gani cha umri kilicho na maisha magumu Zaidi kati ya ujana na uzee?’

3. (a). taja vitu vilivyofananishwa na ujana kwenye shairi.

(b). Taja wazo adhimu la mneni katika ubeti wa mwisho.

#### YETU MACHO

1. Taja msimamo wa kila ubeti

2. Taja athari za elimu ya kisasa kwa vizazi wa kisasa.

3. Taja jeribusi wa shairi hili.

4. Unafikiri ni kwa nini vijana wa zama hizi wanakaidi kufuata mawaidha ya wakale? Taja matokeo ya ukaidi wao

#### KILIO CHETU

1. Taja majanga yanayotuliza katika shairi hili.

2. Mtunzi ana rai gani kuhusu dhiki zetu. Thibitisha kutoka kila kibwagizo.

3. Taja njia inayoweza katuondolea kilio chetu

4. Tumia maneno haya katika sentensi kudhihirisha maana zao: kithiri, vamia, kusubu, dahari, madhli, jiri, mandhari, mandarin.

5. Eleza maana ya ubeti wa tano kwa nathari

#### MWEMA HAJAZALIWA?

1. Ni kweli mwema hajazaliwa? toa jibu lako.

2. Taja nia ya mshairi kuwataja manabili aliowatajaa wenyewe shairi hili.
3. Aghalabu washairi hutumia tabdila, inkisari na mazida. eleza fani zilizotumika katika kuyaendeleza maneno haya: hajazawa, alo, kututowa, kunambia, nodwa, tulopawa, mswafi, kushangiriwa.

## DUNIA TAMABARA BOVU

1. Tahadhari gani inayotolewa kuhusu dunia?
2. Kwa nini dunia imeitwa “tambara bovu”?
3. Eleza maana ya msemo wa “dunia mti makvu kiumbe usiulemele”.
4. Ubeti wa mwisho unatufundisha nini?
5. Eleza maan ya maneno haya: bovu, povu, bofu, utovu, utomvu, ukavu, ukafu, ovu, hofu, utuvu, wajibu, mujibu, laha, raha, roho, loho, huwa, hua, mja, mcha.

## MTENDA AKITENDEWA

1. Taja methali moja yenyewe mana sawa na shairi hili.
2. Shairi hili linatufundisha nini katika maisha yetu?
3. Maneno haya yametumiwa kwa maana gani?
  - i. unyama
  - ii. huna mbawa
  - iii. atendaye hurudiwa
  - iv. dunia haina njama
  - v. siku yako itakuwa

## NILIKOZAWA

1. Shairi hili lilitungwa kwa minajila gani?
2. Taja kwa hatua jinsi mtunzi huyu alivyopata utaalam wake wa ushairi.
- 3 (a). Kwa nini watu wengi hufikiri mtaalam wa ksiwahili sharuti aw mwenyeji wa mwambao au mwislamu?  
(b). Eleza tofauti na uhusiano kati ya dini na lugha.
4. Kujifunza jambo lolote kwahitaji nia na uvumulivu, Jadili kauli hii.

## MASWALI YA ZIADA

1. Taja mambo yoyote muhimu yanayounda na kusawiri umbo la shairi ili lionekane tofauti na tungo nyingine za nathair kama vile riwaya, barua, ilani n.k.
  2. Kwa sasa lugha ya kswihili inapata heshima yake inayostahiki nchini Kenya kutokana na hatua mbili maalum zilizochukuliwa na serikali kufanywa kuwa somo la lazima shulenii kote na kutungiwa mitihani katika ngazi zote za elmu, Jadhili ukweli wa rai hii.
  3. Eleza kwa kutoa mifano maana za (a) lugha ya mama (b) lugha ya mawasiliano (c) lugha ya mtaani (d) lugha ya kufundishia (e) Lugha sanifu.
  4. Watunzi wa mashairi hutumia msamaitai kwa wingi tena kutoka lahaja mbalimbali ili kutajirish ana kuhifadhi ukwasi wa Kiswahili. taja lahaja zozote kumi za Kiswahili, uziujuazo na ueleze zinakozungmzwa.
- 5 (a). utenzi ni nini? Eleza aghalabu tenzi hutungwa kwa madhumini ganai?
- (b). Bahari ni nini? Taja sifa za bahari katika utenzi.

## **MALIMWENGU / HEKAYA NA UNYUMBA**

*Vituko vya Ulimwengu  
Ni vingi vyenye uchungu  
Vinaranda kama wingu  
Mara kwako mara kwangu  
Kamwe havikimbili*

### KWA NIN TUNAVAA?

Nina neno limewamba, lakera yangu suduri  
Ambalo limenikumba, sina heri na buheri  
Nahitaji kuliamba, kwa mavazi yalojiri  
Twavaa kujisetiri, au la ni kujipamba?

Siji hapa kuwapemba, najua nyie basuri  
Mwajua udi na vumba, kama shira na shubiri  
Lakini macho mefumba, mavazi kuyakadiri  
Twavaa kujisetiri, au la ni kujipamba?

Mfano mtu wa gimba, wa maungo furifuri  
Huvaa nguo nyembamba, awe kama msumari  
Na janga likimkumba, hawezi kujinusuri  
Twavaa kujisetiri, au la ni kujipamba?

Wengine wetu wembamba, wa umbile la kadiri  
Na vazi ni kama nyumba, amezwa kama kaburi  
Atembea akiyumba, kama mtu wa chakari  
Twavaa kujisetiri, au la ni kujipamba?

Mavazi yanatulemba, tuwile watu guberi  
Sababu tunajigamba, yatuongeza uzuri  
Kondoo haitwi simba, kwa ngozi ya kijeuri  
Twavaa kujisetiri, au la ni kujipamba?

Si mavazi ni mafamba, cunguzeni mtakiri  
Wapo wanaojiremba, kwa marangi na uturi  
Uzuri aliouumba, Muumba wameghairi  
Twavaa kujisetiri, au la ni kujipamba?

Ninaasa si kugomba, afadhali kujibari  
Kwa mavazi ya kasumba, maana tuna hiari  
Kulikoni kujigamba, kufuja zetu dinari  
Twavaa kujisetiri, au la ni kujipamba?

Mitindo mingi twasomba, toka ng'ambo ya bahari  
Ya mavao ya kubemba, mapambo ya kutafiri  
Twasahau kujichimba, yaletwa kutughururi  
Twavaa kujisetiri, au la ni kujipamba?

Visigino ni vyembamba, njuti zao za fahari  
kutembea ni kuyumba, ungamdhani tuyuri  
Laiti ukimkumba, kubwagika ni dhahiri  
Twavaa kujisetiri, au la ni kujipamba?

Shangazi nanyi wajomba, semani kweli tukiri  
Wazi bila ya ufumba, si kuvunja dasturi  
Kwamba vazi la kubemba, lina kubwa tahayuri  
Twavaa kujisetiri, au la ni kujipamba?

Tafadhalii nawaomba, jambo hili mfikiri  
Vazi liwe ni la pamba, katani ama Hariri  
Na lifungwe kwa kamba, bora mwili husetiri  
Twavaa kujisetiri, au la ni kujipamba?

Kwangu limekosa namba, vazi la hizi dahari  
Ni afadhali kilemba, mashati na kanchiri  
Na mengine ya kishamba, ya kufunika kidari  
Twavaa kujisetiri, au la ni kujipamba?

Jinywa langu nalifumba, kunwna mengi hatari  
Walakini nawaomba, ichunguzeni safari  
Msije kugonga mwamba, kwa miigo furifuri  
Twavaa kujisetiri, au la ni kujipamba?

### APENDAYE HANA RAHA

Nakutolea nasaha, ewe mja majisifu  
Ikwelee kwa fasaha, uambae masumbufo  
Usihisi una raha, kumbe una thakilifu  
Apendaye hana raha, kupenda kuna karaha

Kuna tumbi ya karaha, kupenda mdanganyifu  
Ni kizuo cha fedheha, kingiapo kinakifu  
Huupa moyo jaraha, hata mtu huwa mfu  
Apendaye hana raha, kupenda kuna karaha

Sijaona mshabaha, pendo ninavyolihofu  
Awali lina furaha, ukadhani kamilifu  
Kumbe ndani ni usaha, kutumbuka ni harufu  
Apendaye hana raha, kupenda kuna karaha

Ungasaili masheha, walihina adilifu  
Ama watu wa staha, makasisi takatifu  
Watakupa ya nasaha, kutumbuka ni harufu  
Apendaye hana raha, kupenda kuna karaha

Suhuba haina jaha, sijione changamfu  
Hudhwalisha mtu siwa, akonde mpaka pafu  
Nyumaye aje kuhaha, aseme pendo hafifu  
Apendaye hana raha, kupenda kuna karaha

Usibake kwa madaha, kuva kama mkufu  
Penzi lina ndefu jiha, hupitishia vipofu  
Liwazuge wawe juha, uwaishe utukufu  
Apendaye hana raha, kupenda kuna karaha

Lipo pendo la shabaha, liitwalo pendo kufu  
Kidogo lina buraha, kwa sababu maarufu  
Hilio pendo la nikaha, haba lina ashirifu

Apendaye hana raha, kupenda kuna karaha

### SUMU YA NDOA

Wengi nimewasikia, na lawama foriffori  
Wake wamewakimbia, unyumba kuughairi  
Wanapita wakilia, nikaha zina dosari  
Na mwenizo kuachana, ni sumu kubwa ya ndoa

Ndoa hutaka radhia, na tabia ziwe nzuri  
Wawili kufurahia, kupeana mashauri  
Fujo ikiwatokea, asiwepo mjeuri.  
Kutokuaminiana, ni sumu kubwa ya ndoa

Ndoa mbaya natubia, madhararu yakijiri  
Mkeo kumringia, au mume kumwadhiri  
Kumuona ni ghasia, mwenzi wako kwa kiburi  
Kutokuthaminiana, ni sumu kubwa ya ndoa

Kaeni na kutulia, maisha yawe ya shwari  
Mitazame dunia, vita vilivyokithiri  
Vita havina fidia, kupigana na hatari  
Nyumba bila kupendana, ni sumu kubwa ya ndoa

Kosa laweza tukia, hata likazua shari  
Mmoja kujinunia, kunena akaghairi  
Kwenye pendo la murua, samahani ndiyo heri  
Nyumba kununiana, ni sumu kubwa ya ndoa

Pendo nyumba hupambia, mawili mkisubiri  
Shida zinapowajia, mwambiane kila siri  
Kwa pamoja kutatua, daima muwe tayari  
Kutokushirikiana, ni sumu kubwa ya ndoa

Sote tunayasikia, na kuyaona dhahiri  
Matatizo ya dunia, kila nchi huhubiri  
Tamaa zikipungua, maisha huwa mazuri

Kutaka kiso maana, ni sumu kubwa ya ndoa

Mume mke ni maua, tena pambo la Kahari  
Waishi pamwe kwa nia, kuondolea dosari  
Waongeze jumula, wana bora kwenye mbari  
Kutokusikilizana, ni sumu kubwa ya ndoa

#### NDOA SISYO MAHARI

Mkongwe nadamadema, nimechoka ukulivu  
Ingawa ni kugudemba, mwendo wa kivivuvivu  
Bali kitako si chema, na kimya cha unyamavu  
Yanitia ushangavu, ndoa isiyo mahari

Lipalo leo kusema, ni haya maoanivu  
Naona yenda mrama, hayatupi makinavu  
Ndoa bila darahima, si ndoa ni uhizivu  
Mimio yanitia chevu, ndoa isiyo mahari

Pendekezo la Karima, Mola aliye Mnguvu  
Kwetu ni amri tama, na wala si maonevu  
Vyawaje kuikingama, kwa ndeo na ukatavu  
Naiona unyagavu, ndoa isiyo mahari

Wamezuka maulama, ambao ni wapondovu  
Kuziponda hakama, kwa utole na utovu  
Ja nyama kumla nyama, kama chewa na totovu  
Yatileta kivumvu, ndoa isiyo mahari

Vyambiwa visivyo tama, kama inda na ushupavu  
Mwi hafanywaje myema, pepe liwe kinaivu  
Nyumbu kugeuzwa ndama, mwanena si ukosevu  
Katu hainipi hovu, ndoa isiyo mahari

Kamwe haina hishima, ndoa hii ya mabavu  
Hapati taadhima, tungakazana werevu  
Ndoa bila ya gharama, mwatambia si utovu  
Kwangu ina ugagavu, ndoa isiyo mahari

Yatamkwapo kwa kima, mahari kwa uangavu

Haki kwa baba na mama, wazazi wavumilivu  
Mbona mwafanya hikima, na hila za uchekevu  
Yanipa utepetevu, ndoa isiyo mahari

Mwajipandia lawama, na mbele maangavu  
Kuzipindua lazima, kihadaa na utwevu  
Kaditamati nakoma, fungueni masikivu  
Mahari yana nakama, mbele ya Mola Mwekevu  
Na kuyalipa mapema, kabla ya ndoa si chovu  
Haipati usihivu, ndoa isiyo mahari

#### SAHANI ILOFUNKWA

Ficho hufichwa maneno, yaso na njema bishara  
Feli zenda kwa nong'ono, huzinga kama duara  
Nyumba huja kongamano, zikanenwa kwa hadhara  
Matendo yote hung'ara, moyo huficha maneno

Tabia njema mfano, zaweza ficha dhamira  
Usinyoshee mikono, mambo mawi kuyadara  
Pima sana uwiano, usitende yenyeh dhara  
Matendo yote hung'ara, moyo huficha maneno

Heri juwa elewano, kauli tamu ja shira  
Usihamu mapigano, ficha chuki ni sitara  
Kifichwacho huwa vuno, hakina chembe hasara  
Matendo yote hung'ara, moyo huficha maneno

Nahimiza upendano, una wingi wa tijara  
Kondo huzua tengano, sharifu sana fikira  
Fumba mambo kwa mikono, ukiwa una busara  
Matendo yote hung'ara, moyo huficha maneno

Maovu piga mabano, dhihirisha yanokora  
Onesha watu mfano, kuwa wewe mtu bora  
Usilete farakano, ficha yote yanokera  
Matendo yote hung'ara, moyo huficha maneno

Nionapo penye sono, huwajuvya kila mara  
Andazi piko la ngano, pawepo haba hamira  
Mapakizi kwenye chano, ndo nija na yake sera  
Matendo yote hung'ara, moyo huficha maneno

Tamati beti hapano, yanatosha nilochora  
Cha moyoni ficha mno, hasa tendo la kubera  
Waache wenyenye maono, wayaone yanong'ara  
Matendo yote hung'ara, moyo huficha maneno

#### HERI UENDE

Wangu niliyekupenda, leo nitakufukuza  
Kuishi umenishinda, waniletea mayaza  
Ola vile imekonda, jasadi nimepoonza  
Uwache kuniumiza, ni heri mwana kunenda

Ulikuwa wanagu nyonda, huba nikaikoleza  
Kukupenda kama tunda, embe lenye uliwaza  
Ukajigeuza punda, tete umenicharaza  
Uwache kuniumiza, ni heri mwana kunenda

Nimekonda kama ng'onda, mwandani wanilemaza  
Sautiyo ya kinanda, sitaki kusikiliza  
Sikutaki bora kwenda, muhibu wanishangaza  
Uwache kuniumiza, ni heri mwana kunenda

Mengi ulipokwenda, nilidhani kuteleza  
Nalikupa kila gwand, uvae na kupendeza  
Ulikula na kuwanda, kadiri ulivyoweza  
Uwache kuniumiza, ni heri mwana kunenda

Kinyumw ulipokwenda, nilidhani kuteleza  
Na wewe hukujilinda, nyendo mbaya kupunguza  
Cha kuvunda kishavunda, hata ukikifukiza  
Uwache kuniumiza, ni heri mwana kunenda

Mja wewe wanishinda, kwa tamaa wachukiza  
Kila kitu unadanda, kingawa cha kuumiza

Huwi ndani ya kibanda, huishi kujitembeza  
Uwache kuniumiza, ni heri mwana kunenda

NANI MWUAJI?

Nina mke wangu Teri, na mtoto safarini  
Joto likatukithiri, tukaketi kivulini  
Mtoto wetu Kamari, tukamketisha chini  
Ndugu zangu nambieni, aliyemwua Kamari

Tulimkuta Mashaka, yupo pale kivulini  
Hoi akipumzika, na tita lake la kuni  
Tita wima kaliweka, usawa pale shinani  
Washairi nambieni, muuaji kwa hakika

Ajaja Bwana Kubeli, na kondoo mkononi  
Amechoka hana hali, kwa safari ya juani  
Akakabili kivuli, apumzishe maini  
Wasomaji nambieni, aliyeua kwa kweli

Kafika mpitanjia, na mbwa wake njiani  
Kondoo kuangalia, kukimbia katamani  
Hizo fujo za kimbia, akagonga zile kuni  
Wanagenzi nambieni, yupi hasa aloua?

Kuni zile kuanguka, mwana kapigwa kichwani  
Na mara akadodoka, mfu pale mchangani  
Polisi walipofika, sote tukawa nguvuni  
Waswahili nambieni, aliyeua nataka

Ndungu zangu nifanyeyje, nimeitwa barazani  
Muuaji nimatje, hakimu ambaini  
Nimeshindwa nisemeje, name nimewekwa ndani  
Wahisani nambieni, aloua tumtaje

Wa Kisumu na Mandera, Kitale Embu na Pwani  
Nairobi Makadara, josango nijulisheni  
Nakuru Nyeri Kandara, mwasemaje wahisani?

Wachambuzi nambieni, nduli bila ya subira

Vijana mnaosoma, na wazee majumbani  
Akina baba na mama, rai zenu zitoweni  
Msiba naweka nyuma, nimefungwa kizimbani  
Tafadhali nambieni, mbaini kumsema  
Mwauaji naulizia, ni nani hasa semenii  
Yupi mnafikiria, mwenye mbwa au kuni?  
Kama ni kondoo pia, tamkeni nibaini  
Sinyamaze nambieni, nani mwenye hatia?

Namaliza utondozi, nikisubiri maoni  
Amekataa mwamuzi, hakuna kunidhamini  
Ati hadi uchunguzi, ajue mwuaji nani  
Ili nitoke mbaroni, semenii aliyeua.

### TAFUTA SABABU

Baba, hulalama, mtoto wangu sasa kapotea  
Baba, hulalama, mtoto huyu kanigeukia  
Baba, hulalama, mototo kapotezwa dunia  
Tafuta sababu utajua

Baba, walalama, mtoto kweli amekuwa baa  
Baba, walalama, mtoto wako unamlilia  
Baba, walalama, mtoto kwenda shule kakataa  
Tafuta sababu utajua

Baba, hulalama, mtoto amehuni washangaa  
Baba, hulalama, mtoto analewa kwa chang'aa  
Tafuta sababu utajua

Mama, wajiuma, binti nyumba yako kazalia  
Mama, wajiuma, binti hawezi kusaidia  
Mama, wajiuma, binti hajali kukupikia  
Tafuta sababu utajua

Mama, walalama, binti mhuni kupindukia  
Mama, walalama, binti kutwa kiguu na njia

Mama, walalama, binti laity nisingezaa  
Tafuta sababu utajua

Mimi, ninaona, dunia tamaa imechafua  
Mimi, ninaona, dunia wenyepayo husumbua  
Mimi, ninaona, jinyamazie tulia  
Tafuta sababu utajua

Mimi, naelewa, dunia makeke yatapotea  
Mimi, naelewa, dunia hatima kutatulia  
Mimi, naelewa, dunia warukao watalia  
Tafuta sababu utajua

## MASWALI YA MAZOEZI

### KWA NINI TUNAVAA

1. Taja sababu za kuulizia swali hili.
2. Taja hoja za msemaji wa shairi kuhusu mavazi ya kisasa.
3. Kwa jinsi gani unakubaliana na maoni yamtunzi na kwa jinsi gani unampinga?
4. Taja ujumbe wa ubeti wa 3,5,7,8

### APENDAYE HANA RAHA

1. Kwa nini apendaye hana raha? Taja adha za mwenye kupenda.
2. Lipi pendo lenye faida kidogo maishani?
3. Tafautisha: nasaha, fasah, usaha, furaha, jaraha, karaha, buraha, staha, shabaha, bashasha, mkufu, mkufuu, mkufi, dufu, kufu, ufu.

### SUMU YA NDOA

1. Dondoa mambo yanayoathiri ndoa.
2. Siku hizi ndoa imepoteza thamani. Maana yake nini?
3. Taja sifa za mchumba anayefaa kwa ndoa.
4. Eleza maoni yanayotolewa katika kila ubeti.

### NDOA ISIYO MAHARI

1. Eleza maoni ya mtunzi kuhusu mahari.
2. Ni watu gani wanaopinga ada za kutao mahari? Eleza kwa nini wanapinga.

3. Wengine hufikiri kwamba kutoa mahari ni kumnunua mwanamke. Ta fikra mwafaka kuikosoa dhana hiyo. kisha eleza madhumuni hasa ya mahari. Pia ueleze kama ungependelea utoaji wa mahari uendelee au ufe.

### SAHANI ILOFUNKWA

1. Fumbua anwani ya shairi hili.
2. Taja maonyo, mafunzo na mawaidha yatolewayo na shairi hili.
3. Eleza maana za: bishara, kongamano, hamira, sera, kubera, sitara, maono.

### HERI UENDE

1. Taja kinachomkosanisha mse maji na mwensiwe
2. Mstari wa mwisho wa kila ubeti unakupa picha gani?
3. Mtu anayependa kutembea, asiyetulia nyumbani huitwaje?
4. Taja tabia za mlalmikiwa wa shairi.

### NANI MUAJI?

1. Jadili jibu la shairi hili.
2. Kwa nini si rahisi kumpata mwuaji kati ya mwenye kuni, mwenye kondoo na mpitanhia mwenye mbwa?
3. (a). Nini maana ya ‘Kufunga nyama’ (b). Eleza gharadhi ya shairi hili.

### TAFUTA SABABU

1. Taja kiim cha malalamiko ya baba na mama kitika shairi hili.
2. Msemaji asma ni nini asili ya mchafuko wa dunia? Unakubaliana naye?
3. Shairi hili linatutabanahisha jambo gani?
4. Chambua kikamilifu Sanaa iliyotumika kulisanifu shairi hili.

### MASWALI YA ZIADA

1. Shairi ni zinduko, nasaha, fumbo, funzo, onyo, tumbuizo, mchezo na starehe. Simulia kwa ufasaha jinsi shairi linavyotamalkai na kutanda katika Nyanja hizo zote.
2. Eleza kwa nini watunzi wa mashairi mara nyingi hulaximika kukata (Inkisari), kurefusha (mazida) au kubadilisha (tabdila) maneno wanayoyatumia katika mashairi yao?
3. Eleza jinsi shairi lililotungwa kwa kufuata sera za ushairi linavyopendeza na kuvutia kuliko guni? (Ili kutoseheleza jibu lao, tunga ubeti mmoja kwa ufuni na kanuni ilhali ubertui mwingine utunge guni ndipo uzilinganishe beti zote nmbili – ueleze ni ubeti upi ambao umeshughulisha akili zako Zaidi).

4, Simulia jinsi nyimbo za jadi kama zile zinanzoimbwa na manhu wa makabila yetu (kina mzee makongoro, mwinamila, wamuchutthe, okello beluh, apiyo kayieko, atonoyange n.k.) zilivyotoa mchango mkubwa katika kustawisha mashairi na fasihi za Kiswahili?

5. Je, umewisha kuhudhuria tamasha yoyote ya kitamaduni? Eleza uliyoyaona.

6. Kijijini kwenu kuna manju wa kienyenji? Kama yuko, nende ukamtembelee kisha umsihi kwa adabu na heshima akuimbie akali ya nyimbo zake uzilinganishe na mashairi ya Kiswahili kimaudhuia na kimuundo.

### **MAJONZI / MALIWAZO NA MBAWAZI**

*Dunia tele mizozo  
Majonzi yenyeye mikwazo  
Na madhila mzomzo  
Tupateje maliwazo  
Kutakasa zetu dhiki?*

### **KINA CHA UCHUNGU**

Nakutibu, nipuka, ndugu yangu  
Sinisubu, kwa hakika, mwenzi wangu  
Ujaribu, kukumbuka, bwagubwangu  
Nakusihii, ndugu yangu, makinika

Makinika, damu yangu, mahabubu  
Tumetoka, kwenye fungu, la mababu  
Wajuzika, kuja kwangu, taratibu  
Nakusihii, sibaribu, roho yangu

Roho yangu, ni kitabu, cha shufaka  
Una rungu, kujaribu, kunipoka  
Pendo langu, ndo sababu, waudhika  
Nakusihii, muhibaka, tupa rungu

Hunisibu, kwa mashaka, na tewengu  
Kwa sababu, nateseka, kwenye fungu  
La nasabu, mzalika, damu yangu  
Usiue, damu ndugu, ni uchungu

## NUSURA

Mwanangu kua Nusura, mamako kakuachia  
Kua uone ibira, samba amekuchukia  
Dunia ina madhara, maradhi yamemwija  
Nusura kua, uone dunia

Mwana moyo wanikera, sina pa kukimbilia  
Sina njia ya kudara, giza limenizingia  
Umbeki wadorora, mpweke bila radhia  
Nusura kua, uone dunia  
Mama yako amegura, amelala kazimia  
Mamati hana fikira, kaburi achungulia  
Twamwombea kudura, kwa Rahimu wa Jalia  
Nusura kua, uone dunia

Nusura pata nusura, nawe uole dunia  
Si uwanja wa kuchera tungawa tunakalia  
Huku kuna ubapara, na madhili kwa insia  
Nusura kua, uone dunia

Alikuwa na busara, mama yako nakwambia  
Siye mtu wa hasira, mwanamke asilia  
Bali ndwee ina dhara, kanwa imemfungia  
Nusura kua, uone dunia

Ni uwanja wa izara, kua ukifikiria  
Hughulibu madhukura, wengi wakadidimia  
Usiyaone yanang'ara, ya dunia achilia  
Nusura kua, uone dunia

Umesalia fukara, ja yatima na bandia  
Umemkosa kinara, mtu kukuangalia  
Mama ni nguzo imara, kwa mwanawewe kukulia  
Nusura kua, uone dunia

NIMPE MAMA ZAWADI GANI?

Ndugu zangu waadhama, elo nawaulizia  
Mlo Embu na Giriama, wote mpate sikia  
Wazima hata vilema, rai zenu nauia  
Kipi cha kumpa mama, iwe ni yake fidia?

Miezi tisa tamima, tumbo lake nakalia  
Kwa uwezo wa karima, maam akijizalia  
Ni mdogo sijasema, shida zangu ajulia  
Kipi cha kumpa mama, iwe ni yake fidia?

Mate kwake nimetema, mama hakunichukia  
Tumbo langu likiuma, kinyesi namtupia  
Chakula hakuninyima, na dawa ya malaria  
Kipi cha kumpa mama, iwe ni yake fidia?

Ni mtu mwenye huruma, tena wa kuvumilia  
Haa uwe ni yatima, baba amejifilia  
Akufanyia huruma, mradi kutimizia  
Kipi cha kumpa mama, iwe ni yake fidia?

Japo nimpe heshima, sioni kama murua  
Wema wake nikipima, mbali bado huzidia  
Kanipa nyingi huduma, nini nitalipia?  
Kipi cha kumpa mama, iwe ni yake fidia?

Nikimpa darahima, naona sijatimia  
Unga viazi na nyama, sioni kama fidia  
Zawadi zote kipima, ya kumpa sijajua  
Kipi cha kumpa mama, iwe ni yake fidia?

Kwa heshima yake mama, kwaheri nawapungia  
Naondoka hima hima, swali langu nawaachia  
Nenda keti huko numa, jibu lenu nangojea  
Kipi cha kumpa mama, iwe ni yake fidia?

Shairi hili ili limewahil kupata tuzo an juu kabisa katika mashindano mengi. Liliimbwa na Jacob Nyamai Mtula, mwaka wa 1980 katika Sanaa ya Kiswahili Nairobi, likawa nambari moja: Mwaka 1983 na 1984 liliimbwa na kukaririwa na wasichana wa misyanai kwenye music festival machakos, embu na Nairobi. Na likapata ushindi was kwanza mfululizo.

### OKOWA WANADAMU

Uliye Mola Rahimu, Mwenye wingi wa karama  
Waokowe wanadamu, kwa zako nyingi rehema  
Maisha yao magumu, wanao wanaangama  
Rabanafanya huruma, waokowe wanadamu

Wewe uliye hakimu, usikose la kusema  
Watu mui kushutumu, hiyo iwe yako dhima  
Waama toa hukumu, kungali bado mapema  
Rabuka fanya huruma, waokowe wanadamu

Kuna wengi madhalimu, wanaoleta zahama  
Fanya wawe wakarimu, thuma wawe watu wema  
Wenye utu mahashumu, maisha yawe salama  
Wadudi fanya huruma, waokowe wanadamu

Mambo mawi yasidumu, waokowe himahima  
Tiriri ja mlizamu, matata ukitizama  
Waja wako urehemu, kwa mkono wa ghanima  
Rabahu fanya huruma, waokowe wanadamu

Wakati umeshatimu, kuomba zako rehema  
Watu wa kila hirimu, janga limewasakama  
Hawafuati nidhamu, huzuzuka hizi zama  
Jalali fanya huruma, waokowe wanadamu

Zaghilibu darahimu, huwahadaa mtima  
Watu wana ruhu ngumu, pato linawasukuma  
Wanyonge wanahujumu, wapate tele ndarama  
Mulungu fanya huruma, waokowe wanadamu

Tizama wenye elimu, Mungu wameacha nyuma

Wajizuga kuhitimu, fani zote taaluma  
Halali wanaharimu, tufate zao hikima  
Nyasaye fanya huruma, waokowe wanadamu

Hapa naisha nudhumu, Rabbi unipe neema  
Unipe Jahanamu, ukiona sina wema  
Unitwae marehemu, ilikiwa na siaf njema  
Muumba fanya huruma, waokowe wanadamu  
**DHILA**

Mimi nahimidi Mola, ajue nina heshima  
Kwanu atenda jamala, nipushie zahama  
Tabu kunifunga jela, naomba niwe salama  
Kufurahika mtima, kuwa mbali na madhila

Huua watu madhila, mwenye dhila ni kilema  
Angakuwa kabaila, ana ndwele si mzima  
Bora kukosa chakula, ila niwe na hekima  
Nifurahike daima, niwe mbali na madhila

Hili dhila linowala, akina baba na mama  
Waliokiuka mila, kwa sababu ya kusoma  
Na kuishi shelabela, macho pima yatizama  
Wafurahike nasema, wawe mbali na madhila

Huku kuishi holela, si kwa watu ni kwa moma  
Ndito kuwa wanazala, nyumba ya baba na mama!  
Pekua kila mahala, matokeo siyo mema  
Kufurahika kanama, tuwe mbali na madhila

Wazazi mwaleta dhila, kukimya pasi kusema  
Mwana uliyembayala, akose unatazama!  
Ni kujongeza machela, hatima ulie nyuma  
Kufurahia kusoma, kuwa mbali na madhila

Hawa wana wanokula, peremenda wakisema  
Wasio jail himila, naomba Mungu karama  
Sinilete mkabala, kupata huo ulema  
Tufurahike kuhema, tuwe mbali na madhila

### UKUBWA JAA

Dunia yetu dunia, watu wanakufitini  
Dunia huna udhi, watu wanakulaani  
Dunia huna hatia wabebeshwa kila zani  
Dunia unaonewa, umetenda kosa gani!

Dunia umenyamaza, umetua kwa makini  
Dunia vitu mejaza, watu wanataka nini?  
Dunia wanakucheza, binadamu maliuni  
Dunia unaonewa, umetenda kosa gani!

Dunia mtu akose, hukutia mdomoni  
Dunia hebu waase, hao watu mafatani  
Dunia chuki mpuse, muipate afueni  
Dunia unaonewa, umetenda kosa gani!

Dunia una lawama, za uongo si yakini  
Dunia wanokusema, ni manjunju si razini  
Dunia huna hasama, waja ndio kisirani  
Dunia unaonewa, umetenda kosa gani!

Dunia kuharibika, hayo amezusha nani?  
Dunia watu humaka, hao wanaokuhini  
Dunia umejazika, kila tuna ya thamani  
Dunia unaonewa, umetenda kosa gani!

Dunia unatulisha, bwere bila undani  
Dunia unatkosha, maji tele baharini  
Dunia unaotesha, mimea tosha shambani  
Dunia unaonewa, umetenda kosa gani!

Dunia hujageuka, tangu umbwe na manani  
Dunia watu ndo nyoka, mahaini na wahuni  
Dunia una barak, mwenye pupa hazioni  
Dunia unaonewa, umetenda kosa gani!

### PIGO KUBWA AFRIKA

Roho zinasononeka, tumepata pigo kali  
Samora kututoweka, kwenye kifo cha ajali  
Si pengo la kuzibikam, aloacha bara hili  
Kufa Samora Masheli, pigo kubwa Afrika

Pigo kubwa Afrika, ni hasara bilikuli  
Shujaa aloteseka, bila bomu kuzijali  
Msumbiji kukomboka, Mreno akenda mbali  
Kufa Samora Masheli, pigo kubwa Afrika

Tunalia Afriak, kumpoteza Masheli  
Kiongozi msifika, mjasiri kila hali  
Udhalimu kufutika, likuwa yake kauli  
Kufa Samora Masheli, pigo kubwa Afrika

Msiba umetufika, toka Kenya hadi Mali  
Hodari asoshituka, kupigania ukweli  
Tnagu hatamu kushika, kunyayaswa hakubali  
Kufa Samora Masheli, pigo kubwa Afrika

Tumechoka na mahoka, wadhalimu baradhuli  
Kaburu na vibaraka, watawala wadedhuli  
Unyama tumetosheka, tupigane vita kali  
Kufa Samora Masheli, pigo kubwa Afrika

Tunalia tukimaka, kwa machozi ya maswali  
Ndege kupata ajali, kwetu ni kitendawili  
Angani pa Afrika, pa makaburu manduli  
Kufa Samora Masheli, pigo kubwa Afrika

Alotenda Afrika, kusahau ni muhali  
Wajibu Kuunganika, kukomesha majangili  
Makaburu kuwasaka, kwa heshima ya masheli  
Kufa Samora Masheli, pigo kubwa Afrika

Hapa mwisho nimefika, twambombea Jalali  
Milele kumkumbuka, Samora mwana Masheli  
Vita bado vitawaka, kondoa ukatili  
Kufa Samora Masheli, pigo kubwa Afrika

Samora Mosese machel in rais wa kwanza wa msumbiji. Alifariki kwa ajali ya ndege mnamo tarehe 19/10/86, siku ya Jumapili. Yaokim Chisano akashika wadhifa wa urasi baada ya kifo chake. Sahiri hili lilisomwa Sauti ya Kenya Redioni kuomboleza kifo cha Ndugu Samora, Jumamosi usiku, 13.12.1986

### MASWAHABA

Msiniache wendani, mlo wangu masahibu  
Nakuja mniauni, nina tumbi masaibu  
Sina gange wala peni, na njaa inasibu  
Mwasemani maswahaba!

Tulikuwa wa pamoja, nikiwa sina saibu  
Mali yangu tukafuja, chonde msinisubu  
Nipani name faraja, ndu zangu msinisubu  
Mwasemani maswahaba!

Msinache kuteseka, mimi sikuwaghilibu  
Ngwenje nilipozishika, niliwaita karibu  
Zikawa zinatumika, pasipo hata hisabu  
Mwasemani maswahaba!

Msidhani ni ujinga, kukirimu masahibu  
Utu wangu nilijenga, kuwaiga kina babu  
Ndiposa nikajiunga, kuwa nanyi madhehebu  
Mwasemani maswahaba!

Aliyekupa humpi, wew siyo mahabubu  
Utu wako ni mfupi, u tamthili wa dubu  
Kwani umeona wapi, ujima sio wajibu  
Mwasemani maswahaba!

Nauacha unenaji, ninyamae kama bubu  
Alo basuri na gwiji, achuje nilogutubu  
Marafiki wanyonyaji, si watu wa kusuhubu  
Mwasemani maswahaba!

## CHEMICHEMI

Naalika watekaji, wenyе kiu, na vichomi  
Wote wenyе mahitaji, ya ukuu, hata nyemi  
Fikani mteke maji, muda huu, mjihami  
Jina langu chemichemi, nikitekwa sishi maji

Nikitekwa sisihu maji, kwa bunguu, silalami  
Mnitwike kwenye paji, juu juu, maulami  
Huo sio ufujaji, ni juzuу, ya uchumi  
Mimi ndiyo chemichemi, nikitekwa sishi maji

Wakulima wapandaji, vitunguu, siwanyimi  
Pamwe nyinyi wavunaji, karafuu, sina kemi  
Yachoteni haya maji, kwa vifuu, nazo ndimi  
Sifa yangu chemichemi, nikitekwa sishi maji

Sina inda ni mpaji, kwa shafuu, si mnyimi  
Najua mwayahitaji, mashekuu, na naumi  
Na hamna wagawaji, wa nafuu, kama mimi  
Mniite chemichemi, nikitekwa sishi maji

Katu sinayo magwaji, na makuu, arihami  
Raha yangu ufunzaji, wajukuu, na maumi  
Napuliza maleleji, wende juu, kwa usomi  
Kweli mimi chemichemi, nikitekwa sishi maji

Wachoti hawanifuji, jungu kuu, halivumi  
Kutoa ndiyo faraji, yangu kuu, sijumi  
Mlo mbali nataraji, kunukuu, langu tumi  
Mimi yenu chemichemi, nikitekwa sishi maji

Naenda kutafaraji, Ziwa Kuu, kula mumi  
Nanyi twaeni ulaji, wa bufuu, kwa uchumi  
Mtumie ni siraji, vunja nguu, haizami  
Jina langu chemichemi, nikitekwa sishi maji

### MBONA WALIA?

Kitu gani chakukera, kwa utungu unalia  
Hutaka moyo imara, wa kuhimili dunia  
Dunia tufe duara, hizinga mema na baa  
Nakuona unalia, wew walilia nini?

Kilio chako ishara, kuwa wewe walegea  
Hela kuwa na subira, fanya mambi kwa hatua  
Keti uvute fikira, mambo yakikutatia  
Nakuona unalia, wew walilia nini?

Waliapo vibapara, wenyе navyo hushangaa  
Kingumw huja dharura, na malofa hukenyua  
Dunia ina ndarira, muhali kubashiria  
Nakuona unalia, wew walilia nini?

Nakwambia ni hasara, matozi kuyaatia  
Mikasas siyo dhamira, ya mja kujitakia  
Aghalabu ni kudgura, yake Mola kupangia  
Nakuona unalia, wew walilia nini?

Hakileti hali bora, hiw twiba ukilia  
Na usifanze papara, janga likikufikia  
Kulila mtu humdara, mambo mawi ya dunia  
Nakuona unalia, wew walilia nini?

Lau tozi ni tijara, semani nikasikia  
Nimevuka hadi bara, kwenye baa na belua  
Watu mato yamefura, hulia pasi fidia  
Nakuona unalia, wew walilia nini?

Beti saba nimechora, nyamaeni mnolia  
Mnajitia izara, kilio katu si ndia  
Hutakikana busara, mazonge kuzongelea  
Nakuona unalia, wew walilia nini?

### TABU KWA UZIMA

Kwa shairi nitasema, sana hadi kusikika  
Hali nimeitizama, ukweli ukafichuka  
Hata wew ukipima, utaona ni hakika  
Watu wanataabika, kwa sababu ya uzima

Huwezi ukaterema, pasipo kutaabika  
Kuufariji mtima, ayami ni heka heka  
Mara upate kuchuma, punde chumo hutoweka  
Mimi ninataabika, kwa sababu ya uzima

Madhila na ultima, abadi zikikushika  
Uhai utasimama, hata jina hutoweka  
Sharuti ufanye hima, kujidhili na kusaka  
Wewe unataabika, kwa sababu ya uzima

Katu usibaki nyuma, rizikiyo kuisaka  
Huyapati yalo mema, kwa kuhanja na kuruka  
Inuka na kuinama, maisha ni patashika  
Nyinyi mnataabika, kwa sababu ya uzima

Binadamu hujinyima, mengi yalomzunguka  
Kusudi kujisukuma, atende yenye fanka  
Yaliyojaa huduma, muhimu ya kufurika  
Ndipo anataabika, kwa sababu ya uzima

Wengine wenda kusoma, miaka hata miaka  
Tena ukiwatazama, hawana ngwenje hakika  
Huuza hata vinyama, nyuma waje nufaika  
Wote wanataabika, kwa sababu ya uzima

Nimeona kina mama, baba hata kina kaka  
Dawamu wanayoyoma, hakuna wa kushikika  
Nyoyo zao hutetema, ni viyi watatosheka!  
Kutwa wanataabika, kwa sababu ya uzima

### BARUA YA KIBARUA

Nilipoanza kuwaza, maneno ya kunifaa  
Halafu nikanyamza, akili zikatulia  
Nilijiongelea meza, kalamu kushikilia  
Nikaandika barua, ya kutaka kibarua

Si barua ya kitoto, wala siyo ya mapenzi  
Tena siyo ya masuto, ni barua ya kikazi  
Nikapamba kwa uzito, kwa mawazo ya ombezi  
Nikaandika barua, ya kutaka kibarua

Nikaenda kuituma, ifike kule endako  
Kwa mabwana wa heshima, nilipata sikitiko  
Majibu yao kusoma, yasema kazi haiku  
Ndilo jibu la barua, ya kutaka kibarua

Twende wapi penye haki, dunia inatatiza!  
Vije tupate riziki, nafusi kujiliwaza!  
Kusoma tulishiriki, elimu tukamaliza!  
Barua zetu mwabeza, za kutaka kibarua

Nanena nasikitika aliye juu yu juu  
Mwenye meno akicheka, kibogoyi si naduu  
Nolidhani tungefika, pamoja wakati huu  
Mwaonaje hali yetu, ya kutaka kibarua?!

Lilikaririwa katika kipindi cha Sanaa ya Kiswahili televisheni mwaka 1983 na Joyce Njeri wa shule ya misyani, kangundo.

### KILIO SI DAWA

Shida zikukabili, ni heri utuze moyo  
Bora kustahimili, siwe mtu mwenye payo  
Usiwe roho sahani, kupaparia kiliyo  
Haiwi dawa kiliyo, tabu zikikukabili

Kulia usikubali, chozi kuwa kimbiliyo

Dunia ni idhilali, ngumu sana fanikiyo  
Kupata haja muhali, pasi nia na bidiyo  
Haiwi dawa kiliyo, tabu zikikukabili

Kama kipato dhalili, usinague kiliyo  
Ujifanye u jabali, si legevu wayowayo  
Heri upate kalili usukumie sikuyo  
Haiwi dawa kiliyo, tabu zikikukabili

Kila nchi ni kitali, hawasongi kwa kiliyo  
Walioyajaza mali, sio wenyenye jakamoyo  
Ni tatizo kutojali, wakahodhi walo nayo  
Haiwi dawa kiliyo, tabu zikikukabili

Ni mtoto si rijali, aliaye mbiyombiyo  
Umekua na akila, kaa nazo fikiryo  
Wapaswa kutaamali, sijitie bambaliyo  
Haiwi dawa kiliyo, tabu zikikukabili

Shida yako ni amali, hupati ukafaayo  
Si vizuri kujidhili kwa kiliyo na kijoyo  
Ridhia kuwa hamali, ungoje siku ijayo  
Haiwi dawa kiliyo, tabu zikikukabili

Nafunga shairi hill, msibere ninenayo  
Waliolia awali, walikosa fanikiyo  
Subira ndiyo aali, ndiyo heri ya dhikiyo  
Haiwi dawa kiliyo, tabu zikikukabili

### MKULIMA NA UZIMA

Mkono wa mkulima, ni mgumu kama chuma  
Chakula cha mkulima, ni maharage na sima  
Mtazame mkulima, hapendezi haan dhima  
Bali huyu mkulima, ndiye chanzo cha uzima

Maisha ya mkulima, ni ya dhiki na nakama  
Kibanda cha mkulima, huvuja na kutetema  
Mgongo wa mkulima, daima umeinama  
Bali huyu mkulima, ndiye mama wa uzima

Mke wake mkulima, si wa pambo, wa huduma  
Huyu mke mkulima, hana muda wa kusoma  
Halalami mkulima, hunywa maji ya kisima  
Bali huyu mkulima, ndiye nguzo ya uzima

Nafasi ya mkulima, aghalabu ni ya nyuma  
Magarini mkulima, hadhi yake kusimama  
Hadharani mkulima, huambiwa haan jema  
Bali huyu mkulima, ndiye nguvu ya uzima

Elima ya mkulima, si kusoma si kupima  
Lugha yake mkulima, si kizungu ni ya mama  
Sayansi ya mkulima, kupanda nyanya nan duma  
Bali huyu mkulima, ndiye raha ya uzima

Hunyanyaswa mkulima, ofisi akijitoma  
Anabezwa mkulima, na watu waliosoma  
Akiuma mkulima, hata dawa wamnyima!  
Bali huyu mkulima, ndiye ngao ya uzima

Huyo ndiye mkulima, mjueni mkulima  
Akigoma mkulima, nani atakayepuma?  
Namsifu mkulima adhaniwaye wa nyuma  
Kumbe huyu mkulima, ndiye chanzo cha uzima

### WEMA WANGU

Wema wangu mahabubu, kwa nini unaniponza?  
Hadhani wewe sahibu, kumbe wewe ndiwe funza!  
Leo hivi wanisibu, mwendani nilikutunza  
Umenipa masaibu, kwa mahasidi na wenza  
Wema wangu waniponza, kwangu huna matulubu!

Wengi niliwaheshimu, sina nilompuuza  
Kwangu niliwakirimu, kwa dhifa za kupendeza  
Kumbe wanihasimu, lao kuniangamiza

Shukrani zao sumu, mbaya za kuteketeza  
Wema wangu waniponza, kwa wabaya wanadamu

Masikini wema wangu, ungacha kujitokeza  
Ukae tu ndani yangu, bila ya kujipenyeza  
Kwenda kwa vinungungu, miba yao huumiza  
Inafuma kwa uchungu, kwenye damu na kuoza  
Wema wangu waniponza, hupendeki mwenzi wangu

Kitu gani nichopata, nilikokuelekeza?  
Ila watu kunisuta, simango na kunibeza  
Nikidhani ungeleta, faraja na maliwaza  
Si lolote ni salata, bure kunisheheneza!  
Wema wangu waniponza, kuenda penye matata

Nilotenda ya maana, yamendapi nauliza  
Kwa moyo wa kiungwana, mengi niliyatimiza  
Kwa wazee na vijana, mashaibu na ajuza  
Msema ‘heko’ hakuna, lau wa kunipongeza  
Wema wangu waniponza, kuzuru wenye fitina

Wema lipi tutendane, la faida ya kujaza!  
Ili kwamba tufaane, na hadhi yangu kukuza!  
Singetaka nikuone, wenda kwa wa kunipuza  
Au sivyo tuagane, bora ni kukufukuza  
Wema wangu waniponza, jifiche wasikuone

#### SIKU YANGU

Siku moja itafika, nijifungie safari  
Safari ndefu hakika, isiyotaka magari  
Magari hayatafika, wala meli za bahali  
Siku yangu.

Siyo nadhiri naweka, katu siyo ubashiri  
Ni mwendo ulopangika, ni muhali kughairi  
Kuenda nawajibikwa, kubeta sina hiari  
Siku yangu.

Roho inanitutika, kulia nikitatfakuri  
Ziara sio shirika, hata akhi hujibari  
Wanabaki kuteseka, na kunipami kwaheri  
Siku yangu.  
Siku itakapofika, zamani za kuabiri  
Kutazuka hekaheka, kibuhuti cha suduri  
Na mwinci mno wahaka, kwa wendani na wa mbari  
Siku yangu.

Ziara itafanyika, na Mola ndiye sayari  
Ngia itanimulika, nfike pasi usiri  
Niwache mkitamka, mabayangu na mazuri  
Siku yangu.

Binadamu hutoweka, siku yake ikijiri  
Ugeni una mipaka, name leo nahajiri  
Mipaka yangu yafika, Mungu amenihitari  
Siku yangu.

Sina budi kuitika, wito huu wa kahari  
Ziara kukamilika, moyoni sifanyi ari  
Naenda zangu haraka, bila tadi na kiburi  
Siku yangu.

Wallah sasa naondoka, ni mja sina hiari-  
Huko nitasetirika, dahari hata dahari  
Buriani wahibaka, na maswahaba kwaheri  
Siku yangu.

## MASWALI YA MAZOEZI

### KINA CHA UCHUNGU

1. Taja kiini cha unxhungu wa msemaji
2. Mshororo wa pili wa ubeti wa pili unakupa fununu gani?
3. Taja nasaha anayotoa mshairi katika kituo cha ubeti wa mwisho.
4. Taja jina la shairi hili kisha ufanue maana ya: ukwapi, uato, na mwandamizi.

### NIMPE MAMA ZAWADI GANI?

1. Taja fadhila za mama katika shairi hili.

2. Jahili au ntunga shairi sanifu umjibu mtunzi kumweleza zawadi bora Zaidi ya kumpa mamake ili aridhike.
3. Taja dhana kubwa ya shairi hili.

### OKOWA WANADAMU

1. Kwa nini wokovu wa Mungu unahitajika sana na wanadamu?
2. Taja sababu za maasi ya wanadamu duniani.
3. Eleza maana ya;
  - a) Karama
  - b) dhima
  - c) zahama
  - d) thuma
  - e) mambo mawi
  - f) hirimu

### UKUBWA JAA

1. MBAazi ukikosa maua husingizia mvua'. Thibitisha ukweli wa methali hii kwa kuzingatia yanayosemwa katika shairi hili.
2. Kwa nini watu hutupia dunia lawama zote?
3. Shairi hili lina sifa tatu kubwa kutokana na muundo wake. Taja moja moja sifa hizo na mikondo yake.
4. Shairi hili linadhihiriha huka gani ya mwanadamu?
5. Nini maana ya vifungu hivi?
  - a) dunia yetu dania
  - b) binadamu maliuni
  - c) dunai unatukosha
  - d) dunia watu ndo nyoka.
6. Taja dhamira ya mtunzi kulirudarudia neno "Dunia"?
3. Chanbunga keteto za shairi hili.
4. Tunga insha juu ya "Mvumilivu hula mbivu".

### MKULIMA NA UZIMA

1. Taja adha za mkulima. Nini asili ya adha hizo?
2. Taja fahili na numuhimu wa mkulima katika jamii.
3. Tumia ubeti wa mwisho kufafanulia na kutosheleza kauli hii: MKULIMA NI UHAI".
4. Tunga mjadala kuhusu "Yupi bora Zaidi kati ya mkulima na afisa"? au "Kilimo ni uhai wa Taifa".

### WEMA WANGU

1. Taja msemaji ana daawa gani na wema wake?
2. Eleza kwa nadharia taarifa ya kila ubeti.
3. Eleza msemaji amefanaisha wema wake n nini?
4. Kwa nini tunaweza kuliita shairi hili TAKHMISA?

#### SIKU YANGU

1. Msanii anaongelea safari gani katika shairi?  
Aanaifurahia ziara hiyo au al? Thibitisha kutoka shairi hili.
2. Tajaa kwa mandhair gani shairi hili huhuzunisha?
3. Fafanua maneno haya: nadhiri, kughairi, kubeta, akhi, kuabiri, wahaka, mbari, sayari, ngia, usiri, dahari, wahibaka.

#### MASWALIYA MSETO

1. Taja kirefu cha mashirika haya yanayoshughulikia ukuzaji wa Kiswahili barani afrika na uelezee kila shirika linapatikana wapi?  
(a) CHAKIKE (b) BAKITA (c) UKUTA (d) CHAKA (e). NAKITA (f). TUKI
2. Eleza tofauti kati ya fasihi simulizi a fasihi anadishi.
3. Je, ugumu wa shairi hubabaihw na nini?  
(a). Eleza kwa nini watunzi wengine wa siku hizi hawataki kufuata kanuni za awali za kutunga mashairi?  
(b). Eleza tofauti kati ya mashairi ya Kiswahili na mashairi ya kizungu. (zingatia Zaidi Sanaa).

#### MASWAHABA

1. Maswahaba ni watu gani? Kwa nini mtunzi amewatunga shairi?
2. Msemaji aliwafaa vipi wenziwe katika ubeti wa tatu?
3. Ubeti wa nne na wa tano zinasema nini?
4. Onyo gani linalotolea katika ubeti wa mwisho?

#### CHEMICHEMI

1. Linganisha shairi la chemichemi na la maswahaba kwa upande wa (a) mundo (b) maudhui
2. Taja ni maji gani ambayo watu wanaalikwa kuyateka (ubeti wa 1)?
3. Kwa jinsi gani msanii amejimithilisha na chemichemi?
4. Hawa ni watu gani: maulami, mnyimi, arihami, maumi, wachoti, wajukuu.

#### MBONA WALIA?

1. Kwa nini mtunzi anakuiwaza usilie?
2. Ubeti upi unaokuonyesha kuwa tabu ni ya watu wote – tajiri kwa maskini?
3. Tunaambiwa mtu apaswa kufanya nini anapopatwa na tabu? Taja ubeti unaokupa dokezo hilo.
4. Bainisha unaani wa shairi hili.

### TABU KWA UZIMA

1. Eleza maana ya kibwagizo xha kwanza cha shairi hili.
2. Mshororo wa kwanza wa ubeti wa pili unatukumbusha methali gani?
3. Fichua kiina cha shairi hili kwa jumla
4. Eleza jinsi msemo wa “Panda pesa uvune pesa” unavyodokezwa kwenye shairi.
5. Taja maneno mengine yenye maana sawa na: Ukaterema, mtima, chumo, hima, ultima, kuhanja, ngwenye, dawanu.

### BARUA YA KIBARUA

1. Eleza maana ya “Barua ya kibarua”.
2. Toa tafsili ya (a) kusoma tulishiriki, elmu tukamaliza (b) aliye juu yu juu (c) kibogoya si nafuu.
3. Eleza sababu ya tatizo la uhaba wa kazi nchini. toa pendekero kuhusu njia za kulitatu tatizo hili.

### KILIO SI DAWA

1. Kwa nini watu haulia wanapopata taabu?
2. Msemaji ana maan gani anaposema “Kilio si dawa” unakubali kweli kilio si dawa? Fafanua kwa kiredu.

### VIJEMBE NA KUPIGIA MIFANO

*Ushairi niupambe*

*Nibelegheshe ujumbe*

*Kwenye mbinu za vijembe*

*Kuvinenesha viumbe*

*Jamii ya mahuluki*

### NAHODHA

Safari yetu majini, nyoyo zatetema  
Tuko tutwe jahazini, pepo zarindima  
Kasikazi na kusini, dhoruba zavuma  
Jahazi landa mrاما!

Roho zetu mikononi, haba usalama  
Sote tumo hatarini, mauti I nyuma  
Maji yaja jahazini, wimbi la mlima  
Jahazi landa mrاما!

Kutumbukia majina, papa kaashama  
Chuchunge singe domoni, tayari kufuma  
Nahodha kashika kani, chombo chamlema  
Jahazi landa mrama!

Sasa tupo kileleni, majini kuzama  
Nahodha yumo shakani, ulimi kauma  
Usukani mkononi, hoi kwa kuhema  
Jahazi landa mrama!

Mauti tungojeeni, tufe twatazama  
Nahodha haiamini, yetu taaluma  
Na mwenye kumlaani, lindini hutoma  
Jahazi landa mrama!

#### PANYA

Uwe tuli, nakwambia, wacha kujifanya bunga  
Afadhali, kutulia, utatupiwa mzinga  
Ufedhuli, ni balia, paka nyuma akuwinga  
Hakuna paka mjinga, panya tua, huna hali

Huna hali, na afia, ungali babdo mchanga  
Sipojali, tajifia, usambe ninakukenga  
Kutobali, utalia, panya utavunjwa nyonga  
Hakuna paka mjinga, panya kua, na akili

La ukweli, nakugea, shika usipige chenga  
Paka nduli, anagalia, kwa panya na vifaranga  
Kwa ukali, huwabwia, wote wakitangatanga  
Hakuna paka mjinga, panya juu, jambo hili

Kula wali, na bajia, vyote paka kuvipinga  
Bilikuli, hunyatia, hadi panya kumnyonga  
Si kejeli, jifungia, usihidai nyakanga  
Hakuna paka mjinga, panya kaa, jisaili

Kwa kitali, ni waria kwenye ardhi na anga  
Hana hili, hurarua, mapanya kama kipanga

Kaa tuli, narudia, utavunjwa mtulinga  
Hakuna paka mjinga, panya poa, kwa umbali

Shika hili, lakufaa, kama unataka kinga  
U dhalili, kama bua, na akili hujajenga  
Kuwa mbali, kwenye njia, pale paka hujipanga  
Hakuna paka mjinga, panya chau, si jabali

Sikubali, ukatoa, sauti yako kijingga  
Na mahali, unajua, pana paka wa kimanga  
Si laili, penye jua, dawamu ni kujichunga  
Hakuna paka mjinga, panya nywea, sikauli

Shimo hili, unokaa, nakwambia siyo kinga  
Humo huli, wajitoa, kwenye jiko le unga  
Na halali, husikia, paka pale ukisonga  
Hakuna paka mjinga, yake njia, huwa mbali  
Hakujali, ungalia, panya hunao uganga  
Paka kweli, kaapia, umezwe pasi kuunga  
Pilipili, na dania, hana muda kukaanga  
Hakuna paka mjinga, kwa mamia, ni katili

Atifali, na dhuria, u mahiri kuwachenga  
Kila hali, wategua, mitego ya kukufunga  
Ni muhali, kukuua, kwa marungu na mapanga  
Hakuna paka mjinga, ungalia, hawajali

Onyo hili, naishia, hamnazo zina janga  
Kutojali, nausea, majuto yatakutinga  
Paka kweli, ni shujaa, ungaona amekonga  
Hakuna paka mjinga, fikiria, onyo hili.

### CHUMVI

Chumvi kiungo chema, watumika kila kona  
Kwa mboga na kwenye nyama, huwezi kukosekana  
Hata mapishi hukwama, kama chumvu hakuna

Chunguni huna salama, walaji hufurahika

Sijaona hata moja, wala kusijia jina  
Angaa watu kutaja, kule chumvi hakuna  
Chumvi ndiwe faraja, hawapo wa kukukana  
Wapikaji hukufuja, walaji hufurahika

Kote unahitajika, kwa maredu na mapana  
Na kila anayepika, ni lazima kukuona  
Ndipo chungu huinjika, apike bila hiana  
Hapo unapoyayuka, walaji hufurahika

Sisi kwetu twakuita, munyu jina jema sana  
Kuonyesha wamemeta, kisha wewe ni hazina  
Watu wakikukamata, midomo inarambana  
Ladha murua waleta, walaji hufufurahika

Na kwako kuna kiaga, cha uuzwe tu mchana  
Usiku sisi waoga, jadi ya ushirikina  
Waitwa dawa ya mboga, kuagua subiana  
Wachemka kutuaga, walaji hufurahika

Unapendwa kwa hakika, wazee hata vijana  
Lakini wadamirika, kinywa kikikutafuna  
Wafa bila kufufuka, mlizi wako hapana  
Kwenye mlo wachemka, walaji hufurahika

Mimi nimeshagundua, sina budi ya kunena  
Binadamu akuua, huku akicheka sana  
Sione kukusifia, nia yake kukuchana  
Na wewe unapolia, wenyewe hufurahika

## KIMBA

Kimna kimya huna neno, waliao, wana tabu  
Hulia kusaga meno, wenzio, wakisubu  
Walakini huna guno, wala mwao, taratibu  
Masahibu, hulilia marejeo

Kimba huna majivuno, faraguo, hata jibu

Huna nguvu za mikono, ja wendeo, mahabubu  
Ungapata wezekano, angalao, kuhutubu  
Weni wako, hulilia uwe nao

Kimba huna chukizano, wasemao, sihisabu  
Hulaani farakano, wa umeo, na kidhabu  
Kwa wema huna mfano, neno nao, wakujibu  
Nudugu zako, hulilia ule nao

Kimba usiye maneno, mwenye tuo, kama bubu  
Ufanye uwezekano, wa upeo, na ajabu  
Waliapo toa neno, nena nao, wakujibu  
Unadhani, watalia au mbio?

Apendaye tangamano, na ambao, ni wajibu  
Aje kwa uelewano, alo nao, ja swahibu  
Asaidie hawano, waishio, wenye tabu  
Muungwana, hulilia alo nao

UMETIMU HUJAHITIMU  
Mhairiri massumu, leo tena nimefika  
Kubarizi na kaumu, pasi kero na wahaka  
Kunyamaza kwangu sumu, ilhali nakereka  
Ushindwe kuua nyoka, nguchiro katakadamu

Nguchiro katakadamu, kinyama kiso dhihaka  
Kuajizi hana hamu, nyoka akichacharika  
Mwambaje wataalamu, kijinyama kula nyoka?  
Ushindwe kuua nyoka, nguchiro katakadamu

Nina kisa maalumu, sidhani nimepotoka  
Sineneshi kiwazimu, kughilibu sijataka  
Kwani sisi binadamu, twashindwa kumakinika  
Ushindwe kuua nyoka, nguchiro katakadamu

Mwole keremkeremu, penye nyuki akifika  
Nyuki wote kiwazimu, kughilibu sijataka

Kwani sisi binadamu, twashindwa kumakinika  
Ushindwe kuua nyoka, nguchiro katakadamu

Vije wewe taalimu, msomi wa kusifika  
Tena uliyehitimu, chuo hadi Amerika  
Tati linaposakimu, u papo kufedheheka  
Ushindwe kuua nyoka, nguchiro katakadamu

Si mwalimu si hakimu, wa pale kubabaika  
Hawaeshi kushutumu, taka likiwataika  
Hawatumii ilimu, watu wakafaidika  
Ushindwe kuua nyoka, nguchiro katakadamu

Naishiliza nudhumu, miye mwana mteseka  
Ninakerwa ni ilimu, isoweza kutumika  
Mwabeteani jukumu, si ndaro tunayotaka  
Ushindwe kuua nyoka, nguchiro katakadamu

**AFRIKA INA HOMA**  
Afrika ina homa, inaumwa homa kali  
Taabani yatetema, zizimo la mwili  
Wenye macho hutazama, hii hali  
Na hawana la kusema, kweli  
Afrika ina homa!

Ina ndwele ya hujuma, hasama za majangili  
Na vikwazo vya kuchuma, vinavyotudhili  
Maradhi yanayochoma, bilikuli  
Dawa za usalama, ghali  
Afrika ina homa!

Huku roho zinauma, tepetevu maduhuli  
Viwanda bora vya chuma, bidhaa aali  
Vyauza kutoka nyuma, kule mbali  
Kunyonya wetu uzima, nduli  
Afrika ina homa!

Tungalima na kuchuma, kwa juhudhi na idili  
Twaase kina mama, kwenda spitali  
Kuzipata taaluma, mbalimbali  
Kizazi kipate kima, mali  
Afrika ina homa!  
Twakwaruzwa kama uma, usokuwa na makali  
Tunachinjwa kama nyama, mlo wa ugali  
Hatuna mbele na nyuma, bila hali  
Kusiwepo kusimama, tuli  
Afrika ina homa!

Homa hii ina njama, siyo tukubali  
Mabepari wako nyuma, siha kutudhili  
Gharadhi tukose nema, na akili  
Amkeni wana wema, ‘tali  
Afrika ina homa!

NDEGE HUYU NDEGE GANI?  
Natega kitendawili, bingwa aje kutegua  
Atoe hibu la kweli, pewe heko na halua  
Ndege huyu ndege gani?

Aruka kila mahali, Kenya pote anatua  
Mbawa zake mahemeli, humemeta kwenye juu  
Ndege huyu ndege gani?

Hendi pole kama meli, mwendo kasi hutimua  
Mbio zake za mshali, mbawa akipepetua  
Ndege huyu ndege gani?

Kitaka ardhibiali, ndege huyu nfaunu  
Si nisai si rijali, ni vigumu kung’amua  
Ndege huyu ndege gani?

Anapendwa kwa ukweli, hapana asomjua  
Hukalia mihimili, na mitini pa maua  
Ndege huyu ndege gani?

Kwenye upopo mkali, mbawa zake hutaua  
Hujirusha kulihali, hudhandi tjinasua  
Ndege huyu ndege gani?

Kutua chini muhali, penye tope la mvua  
Wakadha jua hajali, wala mbio kutimua  
Ndege huyu ndege gani?

Hachelei mvua kali, bega Lake Hubetua  
Hufurahi kama mwali, damu yake hugandua  
Ndege huyu ndege gani?

Ndege huyu sikejeli, apaapo unatua  
Kujidai humjali, rahisi kukulipua  
Ndege huyu ndege gani?

Taswira yake medali, huwezi kuibandua  
Ni ishara ya fadhili, uzalendo kufichua  
Ndege huyu ndege gani?

Miguu yake miwili, wakaini hana pua  
Mbawa zake siyo mbili, mmoja wa kumwinua  
Ndege huyu ndege gani?

Mwomo wake si kamili, kama wa mwewe na hua  
Anishi japo hali, bali hewa hupumua  
Ndege huyu ndege gani?

Kulala kwake laili, kiota akifungua  
Hukunja mbawa na mwili, huwezi ukamjua  
Ndege huyu ndege gani?

Mwili wake rangi ghali, mgong hadi kifua  
Ana pambo la gololi, bora la kusisimua  
Ndege huyu ndege gani?

Rangi zake za asili, nne ukimchungua  
Ya kaniki na awali, kwa fahari na murua

Ndege huyu ndege gani?

Michirizi ya miali, weupe wa kung'amu  
Ndiyo rangiye ya pili, endapo hujatambua  
Ndege huyu ndege gani?

Utaona kwa umbali, rangi yake ya kifua  
Wekundu wa pilipili, humeta na kumetua  
Ndege huyu ndege gani?

Ya ukomo ndiyo mali, ya majani ya mabua  
Ndege amezihimili, huwazi kuzipambua  
Ndege huyu ndege gani?

Ndege huyu ni dhalili, bali hutomdekua  
Nundu yake ni jabali, kinga ya kukulipua  
Ndege huyu ndege gani?

Bingwa jibu swalii hili, ndege huyu kugundua  
Amewashinda manduli, kwa bunduki kumuua  
Ndege huyu ndege gani?

Nafupiliza kauli, ndege shani kuchambua  
Mwenye jibu sizohali, kuja mbele kufichua  
Ndege huyu ndege gani?

### CHURA

Chura uambiwe, pasipo hata kunyamaziwa  
Mfano ujuwe, na upate kufahamikiwa  
Utendayo wewe, hayana budi kushutumiwa  
Ninafikiri umpeagawa, nenda upungiwe

Mbonawe kuvimba, kisikia shindo kwenye bwawa  
Huchi hata mamba, na wanaovua kwa ngalawa  
U kando ya mwamba, na macho pima kuyakodowa  
Na hutamani kujiipodowa, kosha lako gamba

Wateki wakija, kuyateka maji ya kunawa  
Waonya kioja, unakithirisha kuchachawa

Wanyosha mapaja, na kuchupachupa kama njiwa  
Maji unapenda kuchafuwa, kwetu yana tija

Mwenzio samaki, taaluma hamjaelewa  
Mbichi hamliki, ni kwa uchafu mlgiojawa  
Tena hamtaki, magamba yenu kuyasuguwa  
Kuishi majini mumepewa, na hayatumiki

Chura wanitisha, tafadhali toka kwenye bwana  
Tumbo kuvimbisha, gharadhi yako sijatambuwa  
Kweli unachusha, kulinda maji hujaelewa  
Ulinzi wako uliopewa, bure wajichosha

### MLINZI

Mlinzi linda dafina, jukumu hilo ni lako  
Katu usiwe fitina, timiza wajibu wako  
Linda japo ni mchana, na usiku ukiweko  
Ulinzi ni dhima yako

Unapolinda hazina, tumaini letu kwako  
Na ukifanya hiyana, litazuka didimiko  
Linda tupate kuvuna, isiwepo sokomoko  
Ulinzi ni dhima yako

Mlinzi bora nis hina, huimarisha anguko  
Akosapo uungwana, husikika mibomoko  
Vema kuaminiana, hamnazo isiweko  
Ulinzi ni dhima yako

Amia nyuni kwa zana, wasimalize limbuko  
Zuia nyoka na ngwena, wasiletete hangaiko  
Linda nyama walonona, faru ndovu na kiboko  
Ulinzi ni dhima yako

Ulindapo hebu nuna, usizoe kciheko  
Walindwa watajazana, kuharibu kazi yako  
Hata kama mwakosana, zingatia dhima yako  
Ulinzi ni dhima yako

### WARIDI LENYE FUNZA

Muaridi watu huukuza, kote maskani  
Na maji tele huyanyunyiza, usawa shinani  
Kwenye ardhi yajipenyeze, hadi mizini  
Hatima mti ukachipuza, uale tawini

Waridi jema hujitokeza, au la thamani  
Lenye uzuri wa kuteuza, kwa yake launi  
Apitaye au hukonyeza, nuru na gizani  
Kwa umaridadi napongeza, waridi yakini

Waridi ua la kupendeza, halina kifani  
Kila kiumbe hulitukuza, wadudu na nyuni  
Na mwana Adamu hulitunza, pendo la moyoni  
Lakini hungiliwa funza, ndani kikonyoni

Linanyauka na kupooza, lapindia chini  
Uzuri wake laupoteza, mdudu yu ndani  
Kasoro hii huuchakaza, uzuri wa shani  
Waridi likiingia funze, uzuri sioni

Mdudu huyu analiponza, letu tumaini  
Ambalo huwa linaliwaza, kwa rihi na sini  
Halina sura linachukiza, litupwe jaani  
Waridi lishaingia funza, halina thamani

Hata kama ukilifukiza, udi na ubani  
Usidhanie litapendeza, lilivyo zamani  
Ni buu lile limeshafyonza, nguvu za kiini  
Kanama hadhiye kupoteza, waridi mtini

### TANGAWIZI

Tangawizi kikolezi, waliwa wapata nini  
Kwene chai u kipenzi, ladha yako burudani  
Lakini yangu mayonzi, waisha huonekani

Yu wapi wa kukuenzi, akulinde maishani  
Wote ni waangamizi, wanakutwanga vinuni

Wakuungie mchuzi, upotelee tumboni

Ola hiyo yako kazi, aghalabu ni motoni  
Wapishi na wanunuzi, wakupendea kanwani  
Au kwenye yao pumzi, kwa rihi njema puani

Unaliwa tangawizi, wewe dawa ya insani  
Unaponya kikohozi, na vidonda makooni  
Lakini huna hijazi, upatacho sikioni

Vipiwe hujikatazi, ukikorogwa majini  
Motoni kwa patilizi, wachemshwa hujioni  
Kisha yako mabakizi, hutupiliwa jaani

Mtumikishi azizi, na tuagane mwendani  
Ningawa nina mbawazi, siwezi kukupa auni  
Metupwa na wachuuzi, kote kote masokoni

#### VIUNGO VYANGU AZIZI

- |  |   |
|--|---|
| 1. Nivineneshe viungo<br>Si vin viungo vy a kaango<br>Bali vy a mwili na bongo<br>Viono na kusikia | 2. Viungo hivi adhimu<br>Ndizo Nyanja maalumu<br>Kwetu sisi binadamu<br>Maisha kuonhozea      |
| 3. Vyataka uangalizi<br>kwenye yao matumizi<br>visiletanagamizi<br>kila tukivitumia                | 4. Vionginevyo havioni<br>Walakini ni vihuni<br>hudaka kila ya fani<br>mazuri nay a balia     |
| 5. Kuna visivyo na woga<br>havina machugachuga<br>hutoka bila kuaga<br>vy a watu kurandia          | 6. Na vingine vina nguvu<br>Nyingi kama zake ndovu<br>hutubeba kavukavu<br>mpaka penye ghasia |
| 7. Kwa sasa ninavitaja<br>viungo vygangu wateja<br>kabla vyao vioja<br>asaa nitajiokoa             | 8. Nakuasa jicho langu<br>Tafadhali dira yangu<br>usitue penye chungu<br>la hilaki na udhia   |

- |   |  |
|---|--|
| 9. Wew ndio muangaza<br>farisi kujipenyeza<br>hata kulikobanza<br>upate kuchungulia               | 10. Na ukishapia tochi<br>ndipo moyo hauachi<br>tamaaaye haifichi<br>mate yakehumezea        |
| 11. Na kwa hivyo langu jicho<br>uonapo ya maficho<br>hebu uingie kicho<br>sidiriki kuzengea       | 12. Moyo wangu nakusihu<br>usipende kujiwahi<br>kutamani ikirahi<br>nisije kuangamia         |
| 13. Ukitua kwenye kitu<br>ambacho mali ya watu<br>kukitaka sithubutu<br>moyo wangu nisikia        | 14. Nakurai jiheshimu<br>moyo uwe na nidhamu<br>uonavyo sivihamu<br>ulofa wangu nachia       |
| 15. Natosheka nivyo navyo<br>Ndivyo mola agawavyo<br>hapana pato la ovyo<br>nakuomba kutulia      | 16. Ukitamani kimono<br>cha mwengine kwa mfano<br>utasabiki mkono<br>kuenda kukichukua       |
| 17. Mkono ninakukanya<br>usije kuijdanganya<br>maisha kuparanganya<br>vya wengine kuvibwia        | 18. Kitanga fumba vidole<br>usije vinyosha mbele<br>kuvidara vitu vile<br>bila idhini kutwaa |
| 19 Vidole vikishabeba<br>vimbi vilivyo na mbia<br>matokeo ni msiba<br>kwenye tumbo kuingia        | 20. Na kinywa usikubali<br>kutafuna pilipili<br>na vinginevyo vikali<br>vyakula visivyofaa   |
| 21. U kipito chake tumbo<br>si vewa kula makombo<br>yenye uvundo na shombo<br>yalotupwa penye jaa | 22. Tamponza mwenzi wako<br>tumbo ni mtambo wako<br>ukimjaza ukoko<br>maradhi wamletea       |
| 23. Na kutoa kadhalika<br>makini sana pulika<br>usitoe ya dhihaka<br>maneno ya kujutia            | 24. Mshike sana ulimi<br>aliye wako msemini<br>mjaribu kunihami<br>kwa hoja za kuvutia       |

- |   |  |
|---|--|
| 25. Maneno huponza damu<br>yasotoka kwa nidhamu<br>na kurudi ni vigumu<br>pindi ukiyaachia      | 26. Mguu mbeba mwili<br>Ulio nyingi redtili<br>nakuomba tafadhali<br>sinifishe pa ghasia       |
| 27. Niambaze penye kondoo<br>palipojaa vishindo<br>nan yoyo zenye mafundo<br>miguu acha kwendea | 28. Kunifisha kama hapo<br>nitapatwa na upapo<br>wa sauti zenye pepo<br>kwa watu wa kuchochaea |
| 29. Nachelea kusikiza<br>Sauti za kuchukiza<br>zinazoweza umiza<br>ruhuni zikingia              | 30. Kwa hivyo langu siko<br>usipige kimbilio<br>ukabeba machukio<br>ukaja kunijazia            |
| 31. Kamata sauti njema<br>za wazuri wenyewe wema<br>wanaojua la kusema<br>siyo payo na hadaa    | 32. Ulimi wangu nakata<br>mzua mangi matata<br>hufanya watu kujuta<br>wakikosa kutumia         |
| 33. Bongo langu linitue<br>na akili zitulie<br>viungo mnisikie<br>msije kunikosea               | 34. Ni nyie mkiteleza<br>mie kuniangamiza<br>ndipo nikawaliwaza<br>msifanye maasia             |
| 35. Mimi nimeshawaona<br>wanadamu wengi sana<br>walopoteza majina<br>viungo kuwachongea         | 36. Nisiwa mmoja wao<br>ningawa mjaa kamao<br>sifa mbaya siyo nago<br>haiwezi saidia           |
| 37. Kwaherini washisani<br>viungo vyangu wendani<br>mzidi kuniauni<br>hadi rudu kunipaa         |  |

## MASWALI YA UTONDOTI

### NAHODHA

1. Taja hatari zote zinazowakabili mabaharia wa shairi hili. Nini chanzo cha hatari hizo?
2. Kwa nini mabaharia wasimsaidei nahodha kuokoa chomba hatarini? thibitisha jibu lako.
3. Taja jambo la kijinga ambalo limefanywa na nahodha linaloolekea kumwangamiza hata yeye mwenyewe.
4. Taja funzo la shairi hili.
5. Eleza maana ya semi hizi:
  - a) jahazi lenda mrاما
  - b) roho zetu mikononi
  - c) nahodha kashika kani
  - d) hoi kwa kuhema
  - e) ulimi kauma

### PANYA

1. Eleza kisa cha paka na panya katika shairi hili.
2. Unafikiri shairi hili limefumba ukweli gani wa maisha? Eleza kinagaubwaga.
3. Panya huwa na furaha wakati gani? Taja methali mbili zinazohusu panya nap aka.
4. Kwa nini panya anaambiwa “Hakuna paka mjinga”? Ni kweli?
5. Jifunze msamiati wa shairi hili ukitumia sherehe na kamusi.

### CHUMVI

1. Tegua kitendawili cha shairi la chumvi
2. Toa maoni yako kuhusu furaha ya walaji wa chumvi.
3. Eleza Imani ya ushirikina unaopatikana katika ubeti wa tano. Je, jamii ya kabilia lako pia wana Imani kama hiyo? sema.
4. Jifunze misemo hii:
  - i. ukiona taa inawaka ujue mafuta yanateketea
  - ii. kuwaka kwa mshumaa ndiko kwisha kwa mshumaa
  - iii. kufa kufaana
  - iv. kufa kwa jamaa arusi
  - v. mkuki kwa nguruwe, kwa binadamu mchungu
5. Taja ukweli unaofichuliwa katika ubeti wa mwisho.

## KIMBA

1. Mshairi ana maoni gani kuhusu kumlilia mfu?
2. Wadhani kwa nini watu hulia wanapofiya na mwenzi wao?
3. Taja wazo kuu katika ubeti wa nee.
4. ubeti wa mwisho unatoa mawaidha gani?
5. Tuliiane tukiwa hai. Jadili

## UMETIMU HUJAHITIMU

1. Watu wepi wanaokejeliwa katika shairi hili? na ni kwa nini?
2. Eleza jinsi anwani ya shairi hili inavyochukuna na maudhui ya shairi.
3. Taja sifa za viumbe hivi kisha ueeze kisa cha mtunzi kuwatumia kwenye shairi: nguchiro, keremkeremu, nyuki, nyoka.

## AFRIKA INA HOMA

1. Afrika ina homa gani? Taja kuanzia ukoko hadi utando.
2. Ni mkondo gani wa usanii uliotumika katika kutunga mashairi ya:
  - a) panya
  - b) kimba
  - c) afrika ina homa?
3. (a). Taja mambo makubwa yanayotatiza na kuyumbisha uchumi wa bara la afrika kisha upendekeze mbinu zinazoweza kutumika kutatatu matatizo hayo.  
(b). Wito gani unaotolewa kwa wana wa afrika kutoka shairi hili?

## NDEGE HUY NDEGE GANI?

1. Fumbua fumbo la shairi hili. kwa nini watu humheshimu sana ndege huyu?
2. Eleza tafsoro za rangi zilizotajwa kuwa ndege anazo.

## CURA

1. Tabaia za chura katika shairi hili zinatupa picha ya mtu wa hali gani katika mazingira yetu?
2. Taja maneno yenyе vina katika kila.
  - i. ukwapi wa ubeti wa pili
  - ii. utao wa ubeti wa nne
3. Eleza sababu za mshairi kuandika:
  - i. ....ujuwe, (ubeti 1), badala ya ... ujue
  - ii. ....mobonwe, (ubeti 2 ), badala ya ...mbona wewe.
  - iii. ....waonya, (ubeti 3), badala ya ....waonyesha.
4. Licha ya chura na samaki, orodhesha jamii tano tofauti za viumbe wa majini.

## MLINZI

1. Mlinzi anawezaje kuleta hasara na maanguko katika umma?
2. Mlinzi bora ana sifa zipi? Taja sifa nne kutoka ubeti wa tatu (3).
3. Taja majina mengine ya viumbe hivi: nyuni, nyoka, ngwean, faru, ndovu

## WARIDI

1. Kwa mujibu wa shairi hili, kwa nini watu hulipenda waridi?
2. Eleza kuponzeka kwa waridi.
3. Eleza mpangilio wa mizani ya shairi hili.
4. Tumia methali hizi kulifafanulia shairi la waridi:
  - a) la kuvunda halina ubani
  - b) nazi mbovu harabu ya nzimaa
5. Taja fumbo la maumbile lililofumbwa kватика shairi hili. Toa mfano maridhawa kuhusu urembo, tabia, ubora, wema n.k

## TANGAWIZI

1. Taja dhiki na hilaki za tangawizi katika ‘TANGAWIZI’.
2. Orodhesha matumizi ya tangawizi katika maish yetu ya kawaidi.
3. Taja jinsi uhai wa tangawizi unavyoathiriwa na mapenzi ya watu kwake.
4. Kwa jinsi gani mtunzi ameifananisha tangawizi na mwandamu? Fichua dhamira.

## VIUNGO VYANGU AZIZI

1. Eleza tofauti kati ya shairi la utenzi na thani. Toa mfano wa kila utungo.
2. Taja nasaha zinazotolewa kwa kila kiungo. je, unakubali kwamba mwanadamu huponzwa na kusalitiwa na viungo hivyo vilivyotahwa tu? Toa hoja zako.
3. Eleza jinsi sura pekee inavyoweza kumponza mtu.
4. Huwa tunamaanisha nini tukisema “Fulani ana damu ya kunguni”?

## MASWALI YA NYONGEZA

1. Taja namna taalum zifuatazo zilivyotumiwa kufunza na kujenga tabia na adabu za watoto katika jamii za kiafrika:
  - a) ushirikina
  - b) methali
  - c) vitendawili
  - d) ngano na hadithi
  - e) nyimbo na ngoma
2. Eleza ni kwa sababu gain kubwa masimulizi ya ngano za kael yalitumia majina na hulka za wanyama kama vile sungura, fisi, simba, ndovu, kobe n.k.?
3. Eleza jinsi tunavyoweza kuhifadhi na kudumisha faishi na utamaduni wetu.

4. (a). Nini maana ya ngonjera? Eleza mashairi ya ngonjera hutungwa kwa madumuni gani?  
(b). Taja tofauti na mlandano kati ya ngonjera na tamthilia.

### **UMALENGA NA KUTUKUZA USHAIRI**

*Tusharifu Umalenga  
Tukiwalunga wahenga  
Waliowahi kutunga  
Ushairi wenyе kunga  
Kwa muwala stahiki*

### **MFANO**

Ni wano, akishakupa, mtu utafuata  
Kinzano, utaihepa, ufile kileleta  
Mavuno, ya chapachapa, wazi utayapata

Pendano, ndilo humpa, mtu kuyapata  
Maneno, yalonenepa, na dhamiri kukita  
Kwa ngano, bila ya pupa, akakaa kuchota

Tatano, hima husapa, wanaobwatabwata  
Kwa guno, na kujitapa, huonywa na kupita  
Mi mno, ni wa kunyapa, hadi tija kuleta

Maono, pale na hapa, na mifano kakata  
Lumbano, sikuogopa, kwa wazee jikunyata  
Changano, limeshanipa, nichotaka kupata

Tamano, nililojipa, tangu sijajivuta  
Ni ono, lililonipa, kutunga kujikita  
Mifano, ikawa tupa, kunoa nikapata

### **KALAMU YANGU**

Kalamu yangu ndhifu, tafadhali niridhia  
Mimi ni mtu dhaifu, sina nguvu na afia  
Fanya niwe maarufu, nudhunu kunandikia

Kalamu nionye njia, nitunge tungo sanifu

Nondoshea thakilifu, njia nyofu ninyoshea  
Nitunge kwa ukamilifu, bila vina kukosea  
Beti zangu ziwe afu, na mizani kuelea  
Kalamu nionye njia, nitunge tungo sanifu

Nifanye mtu raudu, anojua kutongoa  
Siniache niwe dufu, niikirihi dunia  
Nipa sifa za sarafu, mitaji kujipatia  
Kalamu nionye njia, nitunge tungo sanifu

Nipa sifa maradufu, kalamu yangu sikia  
Ziwe sifa za siafu, kutenda pasi kutua  
Nipate pato sufufu, matilaba kukidhia  
Kalamu nionye njia, nitunge tungo sanifu

Sitokuwa badhirifu, tija ukiniletea  
Nitauni vipofu, wazazi na wenye njaa  
Na mimi nile nikifu, maisha kufurahia  
Kalamu nionye njia, nitunge tungo sanifu

Ewe wangu mwadilifu, kalamu yangu adia  
Maisha kama turufu, nipe ree kushindia  
Nasema bila kuhofu, pasu wewe naghumia  
Kalamu nionye njia, nitunge tungo sanifu

Mimi sio mhalifu, jina langua natetea  
Nitajwe mtu arifu, kila pembe ya dunia  
Nitunge tungo tukufu, vizazi kufaidia  
Kalamu nionye njia, nitunge tungo sanifu

Kaditama kusarifu, tabaruku nangojea  
Naomba kula minofu, Kiswahili kuchumia  
Nisiile mbofuwafu, tumboni nikaumia  
Kalamu nionye njia, nitunge tungo sanifu  
**UKALE UNA MAELEKEZO**

Mto mai hupitia, na hayakwwi vilele  
Mwata ndia hupotea, akiiza ya wakale

Ajibwade yu waria, sana kuliko wavyele!  
Tungo tukidhamiria, tuwafuate wakale

Sao ndio walovyaa, nudhumu pindi tulele  
Hatuyaola dunia, wakitunga misemele  
Pamoya nyiso na nyia, ili tue tuziole  
Tungo tukidhamiria, tuwaige na wakale

Mwana alo muelea, hajiatui vidole  
Hulunga alomyea, mayaza asilemele  
Mazoge kuzongolea, humuiga yuleyule  
Tungo tukidhamiria, tutukuze ya wakale

Leyo wengi hutwambia, ya usuli yapitile  
Wanataka kuzumbua, mbinu zawo watumile  
Ushairi hukosea, wana mato wasiole  
Gungo tukidhamiria, tutukuze za wakale

Yuzi imetupitia, na ndiyo yana ivyale  
Yana imetuletea, lelo naswi tuikale  
Tusambe lelo murua, kuliko yana vivile  
Tungo tukidhamiria, tupitiye za wakale

Tusizire yanofaa, ja mahuwa alofile  
Tulokuta kubeua, maizi tushapotele  
Tuande kuyafufua, njeo size tutumile  
Tungo tukidhamiria, tubukue za wakale

Watunzi mlozukia, kuzipinga za ukale  
Msambe mumetimia, kwenda ng'ambu sifikile  
Kwenda mbee ni hatua, n anima sisahawile  
Tungo tukidhamiria, tuembeko za wakale

USHAIRI NI SANA  
Mhairiri mahabub, hebu nipa upenyezi  
Kunyamaza kama bubu, au mwenye gugumizi

Hakika nimejaribu, walakini sijiwezi  
Watungao siku hizi, hawasani huharibu

Hawasani huharibu, tungo sizo kama hizi  
Hata siko kujaribu, bali ni ung'ang'anizi  
Kazi mbovu ni harabu, hazifaidi vizazi  
Watungao siku hizi, si watanzi wa kutibu

Si watanzi wa kutibu, ninenayo wamaizi  
Wanatunga maghusubu, mali ghafi ya dokoz  
Wazeni mashaibu, malenga watangulizi  
Watungao siku hizi, si watanzi hulaabu

Si watanzi hulaabu, pulikani pulikizi  
Shairi silo lakabu, isimu za upazhizi  
Twataka tungo twaibu, za uketo na ujuzi  
Watungao siku hizi, si lolote hughilibu

Si lolote hughilibu, hawana jema pambizi  
Mizani wanaharibu, kwa maneno ya gegezi  
Na vina hawaratibu, beti zina uchafuzi  
Watungao siku hizi, mwawaonaje mababu?

Mwawaonaje mababu, ati hawa ndo wajuzi  
Waliozuka karibu, na nudhumu za uchizi  
Zisofata taratibu, za kunga na utondozi  
Watungao siku hizi, ni watanzi wa lakabu

Ni watanzi wa lakabu, wasokuwa na ujuzi  
Wangeacha kulaabu, lugha yataka panuzi  
Ukweli nawahutubu, na wasifanye ajizi  
Watungao siku hizi, watanzi wa kuharibu

Watunzi wa kuharibu, walahi wanatuhi  
Wanagafata, taratibu, sio huu uvamizi  
Mashairi merikebu, ya kuvusha matumizi  
Watungao siku hizi, hawafai uhatibu

Hawafai uhatibu, hususan pande hizi  
Tungalipo matabibu, magwiji wa uchambuzi  
Ndiyo yetu maarubu, hatupendi banangizi  
Watungao siku hizi, si watunzi mjarabu

Si watunzi majarabu, kunga hawafatilizi  
Kuasana ni wajibu, kwa atakaye panuzi  
Si hivyo kimya cha bubu, au ghedhi za mkizi  
Watungao siku hizi, watunga tungo za ghubu

Watunga tungo za ghubu, wanojita “chipukuzi”  
Hazifiki ughaibu, na hapa hazipendezi  
Hawachelei aibu, kuzitowa kwa wajuzi!  
Watungao siku hizi, tungo zao za ajabu

Tungo zao za ajabu, hao “wanamapinduzi”  
Kama ustaarabu, siyo yawe mageuzi  
Jadi huwa ni adabu, si uasi na igizi  
Watungao siku hizi, namaliza kuhutubu

### KAMANGE

Mzee nina mazonge, matatuzi ndiwe wewe  
Ndiwe wewe sijitenge, babu sina mwenginewe  
Mwenginewe anigunge, ni wewe Mbega mwenyewe  
Mwenyewe peke kamange, nanadi watu wajuwe  
Kombo zangu ninyoshewe, mie mwana si kamange

Siniache nibanange, tungo mbovu nizomewe  
Nizomewe kwa unyonge, na mashuara kamawe  
Kamawe sivungevunge, mweledi usikuliwe  
Usikuliwe unichonge, kwa makali uninowe  
Makosa unikosowe, bado mwana si kamange

Katu ningi si chungunge, bwawa moja wawekewe  
Wawekewe na matonge, wale hadi wavimbiwe  
Kuvimbiwa wajunge, kwogelea wabaliwe  
Kubaliwa wasiringe, kina ningi sichachawe  
Sipendi nilanumiwe, mimi mwana si kamange

Gharadhi yangu nitunge, tungo njema zipitiwe  
Upitie uzipange, vikeukweu utowe  
Utowe zote varanage, gengeni nisitolewe  
Wasinitowe magunge, kwamba heko ninipewe  
Mnyama kunga ni wewe, mimi mwana si kamange  
**MCHEZA KWAO HUTUZWA**  
Kulia aliye mwelewa, aghalabu hupongezwa  
Hupongezwa na kupawa, tunu bora ya kutuzwa  
Kutuzwa na kuambiwa, wanasi wamependezwa  
Mcheza kwao hutuzwa, au la hushangiriwa

Au la hushangiriwa, bila hata kupuuzwa  
Kupuuzwa atakuwa, simanzi tele kajazwa  
Kajazwa pia ukiwa, badala ya kuhimizwa  
Mcheza kwao hutuzwa, au la hushangiriwa

Au la hushangiriwa, bingwa ni wa kutukuzwa  
Kutukuzwa ni kujawa, ari ya kuendelezwa  
Kuendelezwa muruma, kuliko kutelekezwa  
Mcheza kwao hutuzwa, au la hushangiriwa

Au la hushangiriwa, moyo hamu huongezwa  
Huongezwa kuelewa, mchezo mwema kuchezwa  
Kuchezwa akanogewa, kila mtu kuliwazwa  
Mcheza kwao hutuzwa, au la hushangiriwa

Au la hushangiriwa, kwa shangwe pasi kubezwa  
Kubezwa ni kuonewa, si vizuri akitwezwa  
Akitwezwa hughumiwa, na juhudi hupunguzwa  
Mcheza kwao hutuzwa, au la hushangiriwa

Au la hushangiriwa, mbinu zake zikakuzwa  
Zikakuzwa na kipawa, alo nacho kuenezwa  
Kuenezwa kwa vizawa, vya usoni wakafunzwa  
Mcheza kwao hutuzwa, au la hushangiriwa

Au la hushangiriwa, nisemayo yangemezwa  
Yangemezwa na kupewa, satua ya kutukuzwa  
Kutukuzwa maridhawa, tungo hizi bila puzwa

Mcheza kwao hutuzwa, au la hushangiriwa

UPEO

Kua.

Sikia.

Angalia.

Bongo tumia.

Hadaa dunia.

Mwelevu hutulia.

Mwenye pupa hummia.

Papariko zina udhia.

Sura si kitu kujivunia.

Ukiwa hujafa hujatimia.

Mcheza na tope humrukia.

Asiyetosheka mtumwa wa dunia.

Rodo mtoro ipendapo hukimbilia.

Sudi si ya kulilia, sikuye huwadia.

Watu wote ni sawa hakuna dunia kwa Jalia.

Achekapo mwenye meno kibogoyo huungulia.

Zaidi mt apatavyo ndivyo tamaa huzidia.

Uangaliapo mbele yako na kando yako angalia.

Katika kusihi na wenzetu, sharti tuwe twavumilia.

Hakuna mtoto wa haramu vitendo ndivyo haramia.

Pasi na viganja viwili kofi haliwezi kulia.

Sikiliza ya wengi bali lako peke shikilia.

Binadamu ni wa ila hapana alotimia.

Asiyeridhika ni fukara kupindukia.

Uongo sawa, ukweli watu hususia.

Hakuna raha kamili kwenye dunia.

Ajali huwezi kuitambikia.

Ungali hujatenda fikiria.

Maisha ni ya kuyanyatia.

Mali siyo ya kuringia.

Utu bora ni tabia.

Dhiki kuvumilia.

Sipende kulia.

Shika wasia.

Fikiria.

Wazia.

Tua.

### KUFU YA UMALENGA

Tunu hii ya johari, mwatuzaje umalenga?

Masombo nimejifunga, kusawiri mistari

Mistari ya kutunga, nudhumu za umahiri

Nami nilunge wahenga, makungwi wa ushairi

Tunu hii ya johari, mwatuzaje umalenga?

Ningawa siye nyakanga, kama wale wa dahari

Lakini namanya kunga, za kusana na urari

Akali nikibananga, nikaonywa sikasiri

Tunu hii ya johari, mwatuzaje umalenga?

Miiko yakwe nachunga, nisiende mashazari

Mizani vina hapanga, kwa idadi ya fahari

Beti nazo haziunga, kwa muwala wa nadhari

Tunu hii ya johari, mwatuzaje umalenga?

Sikuzawa huko tanga, ama kando ya bahari

Wala kwetu siko Vanga, kwenye watanzi hodari

Elami nimejiunga, na wambujia wa ushairi

Tunu hii ya johari, mwatuzaje umalenga?

Havua yangu maninga, bongo pamwe tafakuri

Hayachuja na kuchunga, telezi zenye dosari

Ziletazo kubananga, utunzi wa mashairi

Tunu hii ya johari, mwatuzaje umalenga?

Kwenye nyamba hajigonga, na siatuki suduri

Na tati zakunitinga, vile vile zakithiri

Lakini ruhu hafunga, nizitunge tungo nzuri

Tunu hii ya johari, mwatuzaje umalenga?

Kaida sipigi chenga, chambueni mtakiri

Ningawa mbuji mchanga, tungo njema nathitari

Sipendi kuvungavunga, amali ya uayari

Tunu hii ya johari, mwatuzaje umalenga?  
Taji hii umalenga, mngasema nikadiri  
Namna mnavyopanga, hadi mkamhiari  
Kuwa mutu ametunga, aipate ni hodari.  
Tunu hii ya johari, mwatuzaje umalenga?  
Si nasaba si kuhonga, ufundi ukishamiri  
Kufata sera na kunga, mwala vina na urari  
Kwa fikira za kupunga, ndivyo ninavyofikiri

Tunu hii ya johari, mwatuzaje umalenga?  
Shairi natia nanga, umalenga nasubiri  
Nipani pasi kuunyenga, kufu yangu ikirari  
Nimetunga na kugunga, hima tieni muhuri.

## MASWALI YA MARUDIO

### MFANO

1. Taja tabia za msemaji zinavyodhiihirishwa na shairi lake.
2. Taja nyenzo zilizomwezesha msemaji kuwa mtunzi kiwango hichi.
3. Taja mtingo uliotumika kwenye nudhumu hii.
4. Kamilisha maendelezo ya:
  - i. mi
  - ii. nichotaka
  - iii. tamano
  - iv. changano

### KALAMU YANGU

1. Fichua ardhilihali ya mtunzi katika shairi hili.
2. Nini (a) kilio na (b) matazamio ya mtunzi katika beti za shairi hili?
3. Taja istiarar katika shairi hili.

### UKALE UNA MALEKEZO

1. Taja maelekezo ya ukale kwa mintarafy ya sahiri hili.
2. Mtunzi ana wito gani kwa watungaji wa mashairi? Simulia dhahiri shairi.
3. Hasara kubwa hutufika kwa kudhania ati mambo ya kale hayana faida yoyore kwetu. Eleza kwa kirefu kalima hii.
4. Kufungamana na mawaidha ya shairi hili, ratibu mahimizo ya utunzi bora yanayokaririwa katika shairi la USHAIRI NI SANAA.

## KAMANGE

1. Eleza maana ya “Mie mwana si kamange”. kisha taja mtuzi atoa mifano ipi kuonyesha yeye ni mwana si kamanage?
2. Taja risala ya shairi hili inaelekezwa kwa nani na ni kwa nini?
3. Shairi hili limetungwa kwa ufundi wa namna tatu. Taja taaluma hizo kwa maelezo ya kutosheleza.

## MCHEZA KWAO HUTUZWA

1. Kwa nini mcheza kwao hustahiki tuzo? Na asipotuzwa matokeo huwaje?
2. Pambanua kila ubeti kwa natharia.
3. Taja methali yene maana sawa na anwani ya shairi hili.
4. Shairi hili lina lengo gani kulingana na sulubu za utunzi wa mashairi?

## UPEO

1. Shairi la UPEO lina upeo gani? Taja
2. Eleza utoshelezi wa kila Mshororo yoyote mitano ueleze mafunzo uyapatayo kutokana nayo.

## KUFU YA UMALENGA

1. Umalenga ni nini? Na malenga ni nani? Fafanua.
2. Eleza jinsi tunu ya umalenga inavyotuzwa. Je msanii wa diwani hii anastahiki kuitwa malenga? Jadili.
3. Mshairi asema: :Lakini namanya kunga … (ubeti 2). “Miiko yakwe nachunga” (ubeti 3). Taja kunga na miiko ya ushairi ambayo mtunzi wetu amanya na kuchunga.
4. GUNI ni nini? Eleza kwa kutoa mifano kamili.
5. Hawa ni kina nani na wana umuhimu gani katika faihi, mila na utamaduni wetu? wahenga, makungwi, naykanga, kamange, wambuji, sogora, manju, ngoi.

## MASWALI YA HIMITISHO

- 1 (a). Taja vigezo vitatu vya mwaidha ya kimaendeleo yanayotolew katika tahakiki ya kitabu hiki.  
(b). Vijana wanaweza kupata motisha gani kutokana na tahaiki hii?
2. Tunga shairi moja kila wiki umpe bingwa aliye karibu nawe kulihariri kisha uwe ukituma nakala gazetini gazetini na redioni. Wakati huo huo jitahidi kuyahi fadhu sana yatakuufaa. (Usinakili shairi la mtu).